**OORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/JimbolaTumbatu |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/Jimbo la Ziwani. |
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |

| | |
|---|---|
| 13.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais. |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais. |
| 18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni. |
| 19.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando. |
| 20.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi. |
| 21.Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni. |
| 22.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole. |
| 24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka. |

| | |
|---|---|
| 25. Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake. |
| 26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake. |
| 28.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi. |
| 29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni. |
| 30.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae. |
| 31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake |
| 32.Mhe. Said Hassan Said | Mwanasheria Mkuu. |
| 33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 34.Mhe. Abdalla Moh’d Ali | Jimbo la Mkoani |
| 35.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 36.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |
| 37.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 40.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |

| | |
|---|---|
| 43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 44.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 45.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 46.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 47.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 48.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 49.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 53.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kuteuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 58.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |
| 60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi | Jimbo la Chambani |
| 61.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |

| | |
|---|---|
| 65.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 66.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 69.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 70.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 71.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 75.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | Jimbo la Jang'ombe |
| 78.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

**Ndugu Yahya Khamis Hamad** **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

**Kikao cha Ishirini na Tano - Tarehe 18 Juni, 2015**

*(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma Dua*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba kuweka mezani hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2015/2016. Naomba kuwasilisha.

**Mhe. Asha Abdu Haji: (Kny. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo):** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuweka mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2015/2016. Naomba kuwasilisha.

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka 2015/2016**
**Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko**

**Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:** *Audhubillahi Minashaittani Rajiim, Bismillahi Rahmani Rahiim.* Mhe. Naibu Spika, naomba kwa heshima zote kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu sasa likae kama Kamati ya Mapato na Matumizi kwa ajili ya kupokea, kuzingatia, kuchangia na hatimae kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwezesha kufika hapa katika ukumbi huu hii leo ni tarehe mosi ya mwezi mtukufu wa Ramadhani tukiwa wazima na afya njema Alhamdulillahi. Aidha, naomba kuchukuwa fursa hii kukushukuru wewe binafsi pamoja na wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa mashirikiano makubwa, michango na ushauri mliotupatia kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa malengo ya Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na kwa kipindi chote kuanzia mwaka wa 2010.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii pia kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein kwa kuongoza nchi yetu kwa uadilifu, hekima na upendo

mkubwa ulioziwezesha nchi yetu kuwa na amani, utulivu na mshikamano uliowafanya wananchi kuendelea kutekeleza shughuli zao za kiuchumi, biashara na uwekezaji bila wasiwasi wowote.

Aidha, nachukua fursa hii kukupongeza wewe binafsi Mhe. Naibu Spika, pamoja na Mhe. Spika, na uongozi wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inawatumikia wananchi kwa usawa bila ya ubaguzi au upendeleo. Kadhalika, nachukua fursa hii kuwapongeza Makamu wa Kwanza wa Rais, Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad na Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi kwa jitihada zao za dhati wanazozichukua za kumsaidia Mheshimiwa Rais wa Zanzibar katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, napenda vile vile kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati ya moyo wangu Naibu Waziri wangu Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi, Katibu Mkuu Ndg. Julian Banzi Raphael, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Said Seif Mzee, Wakurugenzi pamoja na Viongozi wote wa taasisi na mashirika yaliyo chini ya Wizara yangu pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa juhudi zao kubwa za kuchapa kazi pamoja na mashirikiano makubwa wanayonipatia. Hakika bila ya msaada wao ingeniwia vigumu kutekeleza majukumu yangu.

Mhe. Naibu Spika, matayarisho ya bajeti hii yamezingatia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020, Mpango wa Ukuzaji Uchumi na Kuondoa Umasikini Zanzibar (MKUZA), Maelekezo ya Serikali pamoja na ukomo wa bajeti. Kadhalika, mapendekezo haya yamezingatia muongozo wa utayarishaji bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Tume ya Mipango ambao umesisitiza utayarishaji wa bajeti kwa kuzingatia changamoto zifuatazo:

i. Kushuka kwa mapato ya ndani;

ii. Kusita au kupungua kwa misaada ya kuendesha bajeti;

iii. Kudhoofika kwa sarafu ya Tanzania; na

iv. Kujitokeza matumizi muhimu ya Serikali na yale ya dharura.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na mazingatio ya hapo juu, utayarishaji wa mapendekezo haya ulizingatia pia matukio mbali mbali yaliyojitokeza ulimwenguni ambayo yamekuwa na athari za moja kwa moja katika mwenendo wa biashara na uchumi duniani. Matukio hayo ni kama vile mwenendo wa uwekezaji duniani, biashara, fedha na pia machafuko ya kisiasa katika baadhi ya maeneo duniani.

Mhe. Naibu Spika, kama kawaida, mapendekezo ya bajeti hii yamepitia katika ngazi mbali mbali za uzingatiaji wa awali ikiwemo Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi. Naomba pia kuchukua fursa hii kuishukuru sana Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi inayoongozwa na Mhe.Hija Hassan Hija Mwakilishi wa Jimbo la Kiwani, kwa kuchambua mapendekezo ya awali bajeti hii na hatimae kuridhia kuwasilishwa mbele ya Baraza lako Tukufu kwa kujadiliwa na kuidhinishwa.

Mhe. Naibu Spika, Katika hotuba yangu hii, nitaanza kwa kufanya mapitio ya jumla kuhusu mwenendo wa biashara duniani, mwenendo wa biashara Zanzibar, mapitio ya hali ya viwanda, utekelezaji wa malengo ya bajeti ya Wizara kwa mwaka 2014/2015, hali ya mashirika na taasisi zinazosimamiwa na Wizara, kubainisha changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza bajeti ya mwaka 2014/2015 na hatimae kubainisha Programu za Wizara kwa mwaka 2015/2016.

## II. MWENENDO WA BIASHARA:

### Hali ya Biashara Duniani:

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla hali ya biashara duniani iliendelea kuimarika hadi kufikia asilimia 2.8 mwaka 2014 ikilinganishwa na asilimia 2.1 mwaka 2013. Ukuaji huo hata hivyo bado uko chini ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 5.1 katika kipindi cha 1993 – 2013. Hivyo basi kwa ujumla ukuaji wa biashara duniani bado haujatengemaa na kurudi katika kiwango chake cha miaka ishirini iliyopita.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na ukuaji huo, wastani wa usafirishaji bidhaa kutoka nchi zinazoendelea ulikuwa kwa wastani wa asilimia 3.3 ikilinganishwa na usafirishaji bidhaa kutoka nchi zilizoendelea ambao ulikuwa wa wastani wa asilimia 2.2 kwa mwaka 2014 (Mchoro Nam.1).

### Usafirishaji Bidhaa Duniani:

Mhe. Naibu Spika, taarifa za biashara ya kimataifa za mwaka 2014 zinaonesha usafirishaji ulifikia *USD* 18,427 bilioni kwa mwaka 2014, ambapo nchi za Ulaya ziliongoza kwa kusafirisha bidhaa zenye thamani ya *USD* 6,736 bilioni sawa na asilimia 36.5 ya usafirishaji wote duniani, zikifuatiwa na nchi Asia zilizosafirisha bidhaa zenye thamani ya *USD* 5,916 bilioni sawa na asilimia 32.1 ya usafirishaji wote. Marekani ya Kaskazini imekuwa ni nchi ya tatu ikisafirisha bidhaa zenye thamani ya *USD* 2,495 bilioni, sawa na asilimia 13.5 ya bidhaa zote zilizosafirishwa. Nchi za Afrika zilisafirisha bidhaa zenye thamani ya *USD* 557 bilioni sawa na asilimia 3.0 ya usafirishaji wote.

**Uagiziaji Bidhaa Duniani:**

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa uagiziaji bidhaa duniani, jumla ya bidhaa zenye thamani ya *USD* 18,574 bilioni ziliagizwa kwa mwaka 2014. Nchi ambazo ziliongoza katika uagiziaji huo ni za Ulaya (*USD* 6,717 bilioni), nchi za Asia (*USD* 5,874 bilioni), na Marekani ya kaskazini (*USD* 3297 bilioni). Katika uagiziaji huo wa bidhaa, nchi za Afrika ziliagiza bidhaa zenye thamani ya 647 bilioni kwa mwaka 2014.

**Hali ya Biashara Zanzibar:**

**Usafirishaji Bidhaa:**

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Zanzibar kwa mwaka 2014, mwenendo wa usafirishaji bidhaa uliendelea kuimarika kwa kuuza nje bidhaa zenye thamani ya TZS 133,591.7 milioni kutoka bidhaa zenye thamani ya TZS 87,799.6 milioni mwaka 2013 sawa na ongezeko la asilimia 52.14. Usafirishaji huo umechangiwa kwa kiasi kikubwa na mazao ya mwani na karafuu ambayo usafirishaji wake umefikia TZS 103,979.2 milioni kutoka TZS 75,392.6 milioni mwaka 2013. Hili ni ongezeko la asilimia 77.8 ya usafirishaji wote kwa mwaka 2014.

Mhe. Naibu Spika, Nchi ambazo Zanzibar imesafirisha bidhaa zake kwa wingi ni India (TZS 63,539.7milioni), Comoro (TZS 17,780.7 milioni), Singapore (TZS 14,119.9 milioni), *UAE* (TZS 9,797. 9 milioni) na Kenya (TZS 6,068.2 milioni).

**Uagiziaji Bidhaa:**

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Uagiziaji bidhaa kwa kipindi cha mwaka 2014, jumla ya bidhaa zenye thamani ya TZS. 279,552.8 milioni ziliagizwa ikilinganishwa na uagiziaji wa TZS. 208,051.9 milioni mwaka 2013.

Mhe. Naibu Spika, Pamoja na mwenendo mzuri wa usafirishaji bidhaa nje, urari wa bidhaa kwa usafirishaji nje bado umeendelea kuongezeka dhidi ya Zanzibar. Urari huo unaongezeka zaidi tunapozingatia mwenendo wa uagiziaji wa mafuta ya nishati. Uagiziaji wa mafuta ya nishati umeongezeka kutoka TZS 109,169.0 milioni mwaka 2013 hadi kufikia TZS 126, 227 milioni mwaka 2014. Jadweli Nam. 1 linachambua mwenendo wa uagiziaji mafuta ya nishati nchini.

**Biashara Baina ya Zanzibar na Tanzania Bara:**

Mhe. Naibu Spika, biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara inahusisha bidhaa zinazozalishwa Zanzibar na kuuzwa katika soko la Tanzania Bara na bidhaa

zinazoagizwa kutoka nje na kuhaulishwa kwenda Tanzania Bara, kwa upande mmoja na bidhaa zinazotoka Tanzania bara kuja katika soko la Zanzibar kwa upande wa pili. Kwa mwaka 2014, Zanzibar ilisafirisha bidhaa zenye thamani ya TZS 366,354.2 milioni kwenda Tanzania Bara, ikilinganishwa na usafirishaji wa bidhaa zenye TZS 501,204.2 milioni kwa mwaka 2013. Aidha, kwa upande wa Uagiziaji bidhaa kutoka Tanzania Bara, Zanzibar iliagiza bidhaa zenye thamani ya TZS. 64,296.4 milioni kwa mwaka 2014 ikilinganishwa na Uagiziaji wa bidhaa zenye thamani ya 61, 869.3 milioni kwa mwaka 2013.

Kutokana na mwenendo huo, Mhe. Naibu Spika, urari wa biashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara uliendelea kuwa mzuri kutoka nakisi ya TZS 3,341.1 milioni ya mwaka 2011 hadi ziada ya TZS 302,057 milioni mwaka 2014, kama inavyoonekana katika Jadweli Nam. 2.

## III. HALI YA MASOKO:

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar imekuwa inafanya biashara na nchi mbali mbali zikiwemo zile za Kikanda na Kimataifa. Nchi ambazo ziliongoza katika kufanya biashara na Zanzibar kwa mwaka 2014 zilikuwa India, Singapore, *UAE*, na Marekani ya Kaskazini. Mauzo ya bidhaa katika soko la India yaliongezeka kutoka bidhaa zenye thamani ya TZS 35,489.9 Milioni katika mwaka 2013 hadi bidhaa zenye thamani ya TZS 63,539.7 milioni mwaka 2014. Kwa upande wa soko la *UAE* mauzo ya bidhaa kutoka Zanzibar yalipungua kwa mwaka 2014 hadi kufikia TZS 9,797.9 milioni kutoka bidhaa zenye thamani ya TZS 18,961.8 milioni mwaka 2013.

### Mwenendo wa Bei za Chakula Duniani:

Mhe. Naibu Spika, hali ya uzalishaji chakula duniani kwa mwaka 2014 iliendelea kuwa ya kuridhisha na kupelekea bei ya vyakula kama mchele, sukari na ngano kuteremka bei katika soko la dunia. Aidha, kuendelea kushuka kwa bei ya mafuta duniani kuliongeza kuwepo kwa mwenendo mzuri wa bei za bidhaa hizo.

Hata hivyo, zipo dalili za kuwepo kwa ongezeko bei ya mafuta katika soko la dunia, na hivyo kuathiri mwenendo wa bei ya bidhaa hiyo. Vikwazo vya kibiashara iliyoekewa Urusi na Jumuiya ya Ulaya vitaweza kuathiri mwenendo wa upatikanaji mazao ya nafaka hasa ngano katika soko la dunia na hivyo kuathiri bei zake. Mwenendo wa bei za chakula katika soko la dunia kwa sasa unaonekana katika Jadweli Nam. 3.

**Mwenendo wa Uagiziaji na Bei za Chakula katika Soko la Ndani:**

Mhe. Naibu Spika, hali ya uagiziaji wa chakula muhimu hapa Zanzibar, ilionesha kuwepo kwa wastani wa tani 124,189 za chakula muhimu (Mchele, Sukari na Unga wa Ngano) kwa ajili ya matumizi ya soko la ndani hadi kufikia mwezi Machi, 2015. Jadweli Nam. 4 linachambua hali ya uagiziaji chakula katika kipindi cha mwaka 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa mwenendo wa bei za bidhaa hizo za chakula muhimu uliendelea kuwa wa utulivu kutokana na Serikali kuendelea na hatua za kisera za kusimamia bei za chakula muhimu kwa kushirikiana na wafanyabiashara. Hata hivyo, katika kipindi cha mwezi wa Mei, 2015 kulijitokeza upandaji wa bei za bidhaa muhimu za chakula uliosababishwa na kupanda kwa thamani ya dola ya kimarekani ambayo ilichangia kushuka kwa Shilingi ya Tanzania. Sababu nyengine ni athari zilizotokana na mvua ya masika kwa upande wa bidhaa zilizotoka Tanzania Bara. Hata hivyo, bei hizo za chakula muhimu katika soko la Zanzibar ziliendelea kuwa na utulivu katika kipindi cha mwaka 2014/2015 kama inavyoonekana katika Jadweli Nam. 5.

**Mwenendo wa Bei ya Karafuu na Mwani:**

Mhe. Naibu Spika, wizara yangu imeendelea kufuatilia mwenendo wa bei za mazao ya mwani na karafuu ambayo huzalishwa na kusafirishwa na Zanzibar. Katika kipindi cha mwaka 2014, bei ya karafuu katika soko la dunia ilikuwa kati ya *USD* 9,000 hadi *USD* 11,500 kwa tani. Kwa upande wa soko la ndani, Serikali bado inaendelea kutoa asilimia 80 ya bei ya kuuzia karafuu nje kwa wakulima wa zao hilo. Kwa upande wa zao la mwani, bei katika soko la dunia imekuwa kati ya *USD* 0.5 hadi *USD* 2.5 kwa kilo moja katika soko la dunia. Aidha, bei ya zao hilo katika soko la ndani imekuwa ikiuzwa kati ya TZS 450 na TZS 500.

**Mazingira ya kufanya Biashara:**

Mhe. Naibu Spika, Serikali imeanzisha Mpango wa Matokeo kwa Ustawi *(Results for Prosperity – R4P)* ulioanza kutekelezwa mwaka jana kwa ajili ya kuimarisha na kukuza sekta ya utalii. Ili kutekeleza Mpango huo ililazimika pia kuimarisha mazingira ya biashara na ukusanyaji rasilimali fedha. Hivyo, mpango huo licha ya kuzingatia sekta ya utalii ulihusisha pia programu nyengine mbili ambazo ni uimarishaji mazingira ya biashara na ile ya ukusanyaji wa rasilimali fedha.

Mhe. Naibu Spika, katika utekelezaji wa Mpango huo Wizara yangu ina jukumu la kusimamia uimarishaji wa Mazingira ya Biashara kwa kuzingatia taarifa ya tathmini ya Benki ya Dunia ya mwaka 2010. Katika hatua za awali, Wizara yangu

kwa kushirikiana na taasisi nyengine za Serikali na sekta binafsi imepangiwa kutekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kuandaa Sera na Sheria ya kuendeleza ujasiriamali;
ii. Kuanzisha vitamizi (*incubators*) tatu kwa kuendeleza wajasiriamali;
iii. Kuanzisha vituo vitano (5) vya kutoa huduma kwa wajasiriamali*(Business Development Services);*
iv. Kutoa elimu ya taratibu za usajili wa biashara;
v. Kuanzisha mfumo wa usajili wa biashara kwa njia ya elektroniki;
vi. Kuandaa mpango wa kuanzisha mitaala ya ujasiriamali katika maskuli; na
vii. Kutafiti njia ya kuwezesha wajasiriamali kupata mikopo hasa kwa kutumia mali *(Asset – based financing).*

**Urahisishaji Biashara (*Trade Facilitation*)**

Mhe. Naibu Spika, urahisishaji Biashara (*trade facilitation*) ni moja kati ya maeneo muhimu ya kuzingatiwa katika suala zima la ukuzaji biashara katika nchi. Ukuaji wa biashara unaojumuisha kuongezeka kwa usafishaji na uagiziaji wa bidhaa pamoja na ukuaji wa biashara ya ndani unategemea sana uondoshaji wa vikwazo vya biashara na kuwepo urahisi katika kufanya biashara. Upatikanaji wa huduma na miundombinu muhimu kama vile bandari, barabara pamoja na viwanja vya ndege ni eneo muhimu katika kukuza biashara katika nchi.

Mhe. Naibu Spika, katika kufikia lengo la kukuza biashara, Shirika la Biashara Duniani (*WTO*) lilifanya mkutano wake huko Singapore ulikuja na maeneo ambayo yalijuilikana kama " *Singapore issues*". Maeneo hayo yalijumuisha mambo yafuatayo:

i. Urahisishaji biashara (*trade facilitation*);
ii. Uwekezaji (*investment*);
iii. Uwazi katika masuala ya ugavi (*transparency in government procurement*); na
iv. Ushindani (*Competition*).

Mhe. Naibu Spika, nchi nyingi wanachama wa umoja huo zimetekeleza masuala ya uwekezaji, uwazi katika ugavi na ushindani katika kiwango kizuri. Hata hivyo, suala la urahisishaji biashara halijatekelezwa vizuri hadi sasa. Kutokana na ugumu wa utekelezaji wa suala hili nchi wanachama zimelazimika kufanya tathmini ya jinsi zitakavyoweza kutekeleza suala hili kwa kuzingatia uwezo wa kitaalamu, kifedha, kisheria na matumizi ya teknolojia ya mawasiliano.

Mhe. Naibu Spika, tathmini iliyofanywa imegawa utekelezaji suala katika maeneo matatu ambayo kundi A litakalohusisha maeneo yatakayoweza kutekelezwa na nchi wanachama mara kwa haraka zaidi. Maeneo hayo ni pamoja na haki ya kukata rufaa, taarifa, na adhabu (*right to appeal, notification, penalty* na *risk management*). Kundi B litahusisha maeneo ambayo utekelezaji wake unahitaji muda. Maeneo hayo ni pamoja na fursa ya kutoa maoni kabla ya Mkataba, mashauriano, zuio na malipo kwa njia ya elektroniki (*opportunity to comment before entry into force, consultations, advance rulings, detention, electronic payment*), na kundi C litahusisha maeneo ambayo utekelezaji wake unahitaji msaada wa kiufundi na kifedha. Maeneo hayo yanajumuisha uchapishaji wa taarifa, upatikanaji wa taarifa kupitia tovuti, sehemu za maulizo, taratibu za uchunguzi, uwekaji mzuri wa bidhaa zinazoweza kuharibika mapema, utumiaji wa viwango vya kimataifa, na uwepo wa sehemu moja ya masuala ya forodha (*publication, information available through internet, enquiry points, test procedures, handling of perishable goods, use of international standards, single window at customs*).

Mhe. Naibu Spika, hatua ambao zinazohitajika kutekelezwa katika suala zima urahishaji biashara ni pamoja na:

i. Kutoa elimu na uhamasishaji kwa wadau wengi zaidi wa taasisi za serikali na sekta binafsi kuhusu urahisishaji wa biashara ili kukuza uchumi;
ii. Kuandaa miradi ya kisekta inayohusiana na urahisishaji biashara ambayo itahitaji misaada ya kifedha; na
iii. Kuunda mfumo wa usimamizi utakaowezesha utekelezaji wa suala hili.

## MAENDELEO YA VIWANDA

Mhe. Naibu Spika, thamani ya bidhaa zilizozalishwa viwandani imeongezeka kutoka TZS 128.9 bilioni mwaka 2013 hadi kufikia TZS 136 bilioni mwaka 2014. Hili ni sawa na ongezeko la asilimia 5.5. Ongezeko hilo limechangiwa kwa sehemu kubwa na viwanda vya kati vya usafishaji nafaka, usindikaji maziwa, uzalishaji sukari na maji ya kunywa. Kadhalika, uzalishaji katika viwanda vidogo vidogo kama vile utengenezaji wa sabuni, bidhaa za viungo uliendelea kuimarika na kuchangia katika thamani ya bidhaa za viwanda.

Pamoja na ukuaji huo Mhe. Spika, mchango wa sekta ya usarifu wa bidhaa (*manufacturing*) katika Pato la Taifa (*GDP*) uliongezeka kufikia asilimia 9.9 mwaka 2014 kutoka asilimia 6.9 mwaka 2013.

Mhe. Naibu Spika, nafahamu vilivyo uwepo wa shauku kubwa miongoni mwa Waheshimiwa Wajumbe na wananchi kwa ujumla ya kutaka kuwepo kwa kasi zaidi ya ujenzi wa viwanda ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi, ajira, kupanuka kwa wigo wa mapato ya Serikali na ustawi wa wananchi kwa ujumla. Jukumu la Serikali katika lengo hili ni kuhakikisha kuwa mazingira ya uwekezaji katika viwanda yanaimarishwa ili kuiwezesha sekta binafsi kushiriki kikamilifu kuchochea kasi ya uimarishaji na uanzishaji wa miradi ya viwanda.

Kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, Serikali inaendelea na juhudi za kuandaa Sera ya Maendeleo ya Viwanda pamoja na kuandaa Sera ya Maendeleo ya Sekta binafsi na mkakati wa utekelezaji wake.

## UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2014- 2015:

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya utangulizi pamoja na mapitio ya hali ya biashara na viwanda, naomba sasa kufanya mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2014/2015.

### Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa matumizi, wizara ilitengewa jumla ya TZS 5,864.30 milioni kwa ajili ya kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2014/2015. Kati ya fedha hizo TZS 2,486.3 milioni kwa kazi za kawaida, TZS 2,335.7 milioni kwa kazi za maendeleo na TZS 1,042.3 kwa ajili ya ruzuku kwa taasisi zilizopo chini ya Wizara. Mgawanyo wa matumizi hayo ulikuwa kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| i. | Matumizi ya Kawaida TZS (mil) | |
| | a. Mishahara | Shs. 1,240.40 |
| | b. Matumizi mengineyo | Shs. 1,245.90 |
| | **Jumla** | **Shs. <u>2,486.3</u>** |
| ii. | Matumizi ya Maendeleo | Shs. 2,335.7 |
| iii. | Ruzuku | Shs. 1,042.3 |
| | **Jumla** | **Shs. <u>5,864.30</u>** |

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2015, wizara iliingiziwa jumla ya TZS 2,621.24 milioni, ambazo zilikuwa ni sawa na asilimia 65 ya fedha zilizopangwa kutumika kwa kipindi hicho ambacho ni sawa na asilimia 45 ya bajeti ya mwaka. Mchanganuo wa matumizi hayo unaoneshwa katika Jadweli Nam. 6 na Nam 7 zilizoambatishwa katika hotuba hii.

**Ukusanyaji wa Mapato:**

**Mhe. Naibu Spika,** katika mwaka wa fedha 2014 - 2015, wizara yangu ilipangiwa lengo la kukusanya mapato ya TZS 100.0 milioni kutoka katika vianzio vyake mbali mbali. Hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2015, jumla ya TZS 84.8 milioni zilikusanywa na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

**Utekelezaji wa Malengo ya Bajeti:**

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2014 - 2015 wizara ilijipangia kutekeleza malengo 36, ambayo ufafanuzi wake unafanywa kiidara kama ifuatavyo:

**IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI:**

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ilijipangia kutekeleza malengo tisa (9). Utekelezaji wa malengo hayo ni kama ifuatavyo:

**i. Uandaaji wa Sera ya Kumlinda Mtumiaji na Sera ya Maendeleo ya Viwanda:**

Mhe. Naibu Spika, dhana ya kumlinda mtumiaji ni pana na inahusisha mkusanyiko wa Sheria na vyombo mbali mbali vya udhibiti wa usalama na ubora wa bidhaa na huduma zinazopatikana katika soko. Ili kujenga mfumo bora wa usimamizi na kumlinda ntumiaji (*Consumer Protection Policy*) wizara yangu imeanzisha juhudi za kuandaa Sera kwa madhumuni hayo. Uandaaji wa sera hiyo utahusisha taasisi mbali mbali za Serikali pamoja na sekta binafsi. Katika kutekeleza lengo hili, Wizara imeshachukua hatua za awali za kuandaa dhana ya Sera yenyewe ambayo itatumika kushirikisha wadau wengine katika mchakato wa kuandaa sera yenyewe.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa uandaaji wa Sera ya Maendeleo ya nilieleza katika hotuba yangu ya 2014/2015 kuwa Serikali inashirikiana na Shirika la Viwanda la Umoja wa Mataifa (*UNIDO*) kuandaa Sera ya viwanda ambapo hatua hizo zinaambatana na uimarishaji wa uwezo wa wataalamu wa ndani katika kuandaa Sera hiyo. Kazi hii bado inaendelea ingawa kasi yake ni ndogo.

**ii. Mapitio ya Sera ya Wafanyabiashara wadogo wadogo (*SMEs*):**

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza lengo hili, Idara inaendelea kukusanya taarifa muhimu za utekelezaji wa Sera hiyo na kutathmini mafanikio na matatizo yake.

**iii. Sheria ya Maendeleo ya Wafanyabiashara wadogo wadogo (*SMEs*)"**

Mhe. Naibu Spika, katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka jana nililiarifu Baraza lako kuhusiana na azma ya Serikali ya kuweka mfumo wa kisheria utakaosimamia maendeleo wajasiriamali kwa kuandaa Sheria ya Maendeleo ya wajasiriamali. Utayarishaji wa sheria hiyo umeanza na itazingatiwa pamoja na Sera ya ukuzaji ujasiriamali inayoendelea kutayarishwa.

**iv. Kufanya utafiti wa bidhaa;**

Mhe. Naibu Spika, Idara ilijipangia lengo la kufanya utafiti wa uzalishaji na upatikanaji wa masoko kwa mazao mawili ya mananasi na viazi vitamu. Katika kutekeleza lengo hili, Idara imekamilisha kazi ya ukusanyaji wa taarifa muhimu za awali zikiwemo za hali ya uzalishaji wa mazao hayo pamoja na ukubwa wa maeneo ya uzalishaji. Hata hivyo, hatua inayofuata katika kutekeleza lengo hilo ni kukusanya takwimu za masoko ya bidhaa hizo ambazo zinazalishwa kwa msimu maalum hapa nchini.

**v. Uratibu wa Utekelezaji wa Mkakati wa Usafirishaji Bidhaa Nje (*National Export Strategy – NES*):**

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika hotuba zangu zilizotangulia kuhusiana na suala hili la uratibu wa Mkakati wa Usafirishaji Bidhaa Nje kuna mafanikio na changamoto ambazo zinazoikabili kazi ya uratibu huo. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na upelekaji wa umeme kisiwani Pemba, kufanya matengenezo ya uwanja wa ndege wa Zanzibar, kufanya utafiti wa Eneo Tengefu la Uchumi la Zanzibar, kuanzisha Taasisi ya Viwango ya Zanzibar, Kuanzisha chombo cha kusimamia utaoaji wa leseni za biashara, kufanya mapitio kwa Sheria za Biashara, na Kuandaa na kutekeleza Mkakati wa Maendeleo ya Karafuu. Hatua hizo zilizotekelezwa ni moja wapo wa njia za kuengeza usafirishaji wa bidhaa. Aidha, Mkakati huo pia unabiliwa na changamoto ni pamoja na ukosefu wa fedha pamoja na ushiriki mdogo kwa taasisi zinazohusika na utekelezaji wa Mkakati huo.

Mhe. Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto za utekelezaji wa Mkakati huo, wizara imeuingiza Mkakati huu kati Mradi wa "*Enhanced Integrated Framework Tier 1*" (*Capacity Building for Trade Mainstreaming*) ili kuweza kufanikisha utekelezaji wake. Moja ya shughuli ambazo zitafanyiwa kazi katika kutekeleza Mkakati huu katika kipindi cha mwaka 2015/2016 ni kuufanyia mapitio kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Katika kufanikisha kazi hiyo ya mapitio, wizara imekusanya takwimu za utekelezaji wa Mkakati ambazo zilipelekea

kuandaa dhana ya awali ambayo iliwasilishwa Wizara ya Viwanda na Biashara, Tanzania Bara kwa ajili ya kuandaa dhana moja ya Tanzania itakayopelekwa Benki ya Dunia kwa kuanza taratibu za ufanyaji wa mapitio.

**vi. Uandaaji wa Bajeti ya Wizara:**

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza lengo hili, Idara imeandaa taarifa mbali mbali za utekelezaji wa malengo ya bajeti iliyopanga kutekeleza katika kipindi cha mwaka 2014/15 ambazo zimewasilishwa katika Kamati za Baraza la Wawakilishi. Aidha, Wizara imeandaa vipaumbele na makisio ya ukusanyaji mapato pamoja na kuandaa taarifa ya mapato na matumizi kwa mwaka 2015/16, kama itakavyoelezwa huko mbele.

**vii. Ushiriki wa Mikutano ya Kikanda, na Kimataifa inayohusiana na Sera, Sheria na taratibu za kibiashara:**

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza lengo hili Wizara ilishiriki katika mikutano saba (7) ya majadiliano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*). Mikutano hiyo ilizungumzia masuala ya Uondoshaji wa Vikwazo vya biashara baina ya nchi wanachama ambapo kazi ya kuainisha vikwazo ambavyo vinazorotesha biashara katika Jumuiya inaendelea kufanyika. Aidha, majadiliano ya utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuandaa Mpango utekelezaji wa Itifaki hiyo. kwa upande wa majadiliano kati ya *EAC* na Jumuiya ya Ulaya umekwishatiwa saini.

**viii. Ulinzi wa Zao la Karafuu:**

Mhe. Naibu Spika, katika kuendelea na ulinzi wa zao la karafuu, Wizara imeratibu shughuli za Kikosi Kazi maalum kilichoanzishwa kwa ajili ya ulinzi dhidi ya magendo ya zao la karafuu. Mikakati hiyo ilikuwa ni pamoja na kuweka kambi za ulinzi (*detach*) katika maeneo yenye uwezekano mkubwa wa kutoroshea karafuu, kuweka vizuizi barabarani (*Roadblocks*), na kuendesha doria.

**ix. Utekelezaji wa Masuala Mtambuka (*Cross – Cutting Issues*):**

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza lengo hili, Wizara imeshiriki katika mikutano miwili inayohusiana na Jinsia na masuala ya maambukizi ya *HIV* na UKIMWI. Aidha, Idara imeandaa kikao kimoja kinachohusiana na utoaji wa uelewa kuhusiana na Taasisi ya Kupambana na Rushwa kwa uongozi wa Wizara.

**MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2014/2015**

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2014/2015 wizara ilitekeleza miradi minne (4), ambayo utekelezaji wake unasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Utekelezaji huo ni kama ufuatavyo:

**Mradi wa Mkakati wa Kuendeleza zao la Karafuu**

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza Mradi huu wa Mkakati wa kuendeleza zao la karafuu, masuala yafuatayo yalitekelezwa:

i. Taarifa kuhusu umuhimu wa karafuu kiuchumi na matumizi yake (*Inspiration Book*) imeandaliwa;

ii. Maandalizi ya viwango na uthibitishaji wa karafuu (*standards and certification*) yanaendelea;

iii. Kanuni za Sheria ya kulinda Haki za Tasnia ya Mali za Ubunifu Nam. 4 ya 2008 zimekamilika;

iv. Kituo cha kufanyia ufungashaji wa bidhaa za viungo kimetayarishwa katika eneo la Saateni na tayari kimeanza kazi; na

v. Hati ya uthibitisho wa Kilimo hai (*Organic Certificate*) imetolewa na *Tancet* kwa ajili ya eneo *ambalo* litatumika kwa ufungashaji wa bidhaa za viungo.

**Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kukondoesha Biashara Zanzibar**

Mhe. Naibu Spika, katika hotuba yangu kama hii kwa mwaka 2014/2015 nililiarifu Baraza lako tukufu kuwa serikali kwa kushirikiana na Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (*UNDP*) chini ya mradi wa kukondoesha biashara (*Trade Mainstreaming*) inaandaa Mpango Mkuu (*Master Plan*) ya uendelezaji wa kituo cha maonesho ya Biashara.

Naomba kuarifu kuwa Mpango Mkuu huo tayari umekamilika na kuwasilishwa Serikalini kwa mazingatio. Kadhalika, chini ya mradi huu hatua ya kuimarisha

uwezo wa baadhi ya vyombo vya Serikali zilichukuliwa kwa kuandaa mafunzo katika maeneo yafuatayo:

i. Uibuaji wa miradi, usimamizi, ufuatiliaji na tathmini;

ii. Kuimarisha uwezo wa kuchambua takwimu za biashara kwa kutumia vifurushi vya takwimu (*Statistical Packages*)

Mafunzo hayo yalitolewa kwa maofisa wa wizara na sekta binafsi Unguja na Pemba. Kadhalika, ziara maalum za mafunzo nje na ndani ya nchi ziliandaliwa chini ya mradi huu.

**Mradi wa Kuimarisha Taasisi ya Viwango (*ZBS*)**

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza mradi huu Taasisi ilijipangia kuandaa michoro ya ujenzi wa Makao Makuu ya Ofisi na maabara katika eneo la Maruhubi pamoja na ununuzi wa vifaa kwa ajili ya maabara hizo. Hatua ya utayarishaji wa michoro pamoja na gharama za ujenzi wa Makao makuu na Maabara zimekamilika. Aidha, katika hatua za utekelezaji wa shughuli za msingi, Taasisi inaendelea na hatua za kukamilisha ujenzi wa vyumba viwili vya maabara za chakula na Kemikali katika eneo ziliopo ofisi hizo kwa sasa huko Amani.

**Mradi wa Programu ya Mazingira Bora ya Biashara**

Mhe. Naibu Spika, nilieleza katika kifungu cha 23 cha hotuba hii kuhusu hatua za awali zilizopangwa kutekelezwa na wizara yangu katika mradi huu. Naomba kutoa maelezo ya utekelezaji wa hatua hizo kwa mwaka 2014/2015 kama ifuatavyo:

i. Idara ya Mipango Miji na Vijiji ni moja ya taasisi zinazotekeleza Mpango wa Serikali wa Kuimarisha Mazingira ya Biashara. Kwa upande wake Idara hii ilikuwa na jukumu la kuharakisha ukamilishaji wa Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi.

   Katika kutekeleza jukumu hilo, Idara hiyo ilifanya warsha mbili za wadau, moja Unguja na moja Pemba, kwa ajili ya kuwasilisha

rasimu ya Mpango wa Matumizi ya Ardhi wa Zanzibar ambapo rasimu hiyo imejadiliwa na kuchangiwa na wadau husika;

ii. Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto ilikuwa na jukumu la kuanzisha vitamizi (*incubators*) vitatu.

   Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara hiyo, imeanzisha vitamizi (*incubators*) viwili vya Utalii na *ICT* katika eneo la Taasisi ya Sayansi na Teknolojia (*KIST*) ambapo vikundi mbali mbali vya wajasiriamali vimejisajili na vinaendeleza na mafunzo. Kwa sasa vikundi kumi na tatu (13) vinaeendelea na mafunzo hayo.

iii. Kuanzisha vituo vya kutoa huduma kwa wajasiriamali katika maeneo ambayo vitamizi vya *ICT* na Utalii vimeanzishwa;

iv. Wakala wa Usajili wa Mali na Biashara alipewa jukumu la kutoa elimu ya kusajili biashara. Katika kutekeleza jukumu hilo, wakala imeandaa Rasimu ya Kanuni ya Sheria ya Usajili wa Biashara na Mali ambayo itaweka taratibu za kusajili biashara hapa Zanzibar;

v. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilikuwa na jukumu la kuanzisha mitaala ya ujasiriamali katika maskuli na vyuo vikuu. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara hiyo, imeandaa warsha juu ya uelewa wa ujasiriamali pamoja na kutoa mafunzo ya walimu ambao watasomesha masomo ya ujasiriamali. Aidha, hatua za utayarishaji wa rasimu ya mitaala ya ujasiriamali itakayotumika kwa maskuli na Vyuo Vikuu zinaendelea kuchukuliwa;

## IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Uendeshaji na Utumishi ilijipangia kutekeleza malengo sita (6). Utekelezaji wa malengo hayo ni kama ifuatavyo:

### i. Kuimarisha Rasilimali Watu

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Idara ilipanga kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi 17. Hadi sasa Idara imewapatia wafanyakazi kumi na moja (11) mafunzo ya muda mrefu katika fani ya uchumi, Utunzaji kumbukumbu, manunuzi, Biashara, Technolojia ya Habari, pamoja na wafanyakazi tisa (9) mafunzo ya muda mfupi. Idara pia imetoa mafunzo ya Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka ya 2011. Aidha, Idara imeendelea kufuatilia wafanyakazi waliopo masomoni pamoja na kuwalipia ada za masomo wafanyakazi wanaoendelea na mafunzo ya muda mrefu katika vyuo viliopo Tanzania.

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi hiki, jumla wafanyakazi saba (7) walistaafu na wafanyakazi wanne (4) walihamishiwa wizarani wakitokea katika Shirika la Magari. Aidha, wafanyakazi 35 walipewa likizo zao za kawaida, wafanyakazi wanne (4) walipewa likizo za uzazi, na wafanyakzi 9 walipewa likizo za dharura.

### ii. Kuajiri wafanyakazi wapya:

Mhe. Naibu Spika, idara ilipanga kuajiri wafanyakazi kumi na moja (11) wa fani za Mizani na Vipimo, Sheria, Uchumi, Ujasiriamali na Biashara. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015 Idara haikufanya uajiri wa wafanyakazi wapya. Aidha, wafanyakazi ambao waliajiriwa katika kipindi kilichopita wamepatiwa mafunzo ya awali pamoja na majukumu yao ya kazi.

### iii. Ukarabati wa majengo na matayarisho ya ujenzi wa Ofisi Kuu Pemba:

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Idara ilikusudia kufanya ukarabati wa majengo yake matatu pamoja na kutayarisha michoro ya ujenzi kwa ajili ya Ofisi Kuu ya Wizara iliopo Pemba. Katika kutekeleza lengo hilo, idara iliendelea na ukarabati wa majengo yake ya Makao Makuu na Idara ya Viwanda, ambapo ukarabati huu umefikia hatua nzuri na sasa majengo hayo yanatumiwa na wafanyakazi. Aidha, wizara pia ilipanga kuyafanyia ukarabati majengo yake mawili ya Bizanje lililopo eneo la Malindi Mizingani na jengo la kituo cha biashara lililopo Darajani ambapo kazi hizi hazikuweza kufanyika kutokana na uhaba wa fedha uliojitokeza.

Mhe. Naibu Spika, aidha, kwa upande wa ujenzi wa ofisi kuu ya Pemba wizara inaendelea kukamilisha taratibu za kuanza ujenzi wa jengo hilo kisiwani Pemba, ambapo rasimu ya awali ya michoro na gharama za ujenzi (*BOQ*) imeandaliwa na kuwasilishwa wizarani.

**iv. Uandaaji wa Mpango wa Ununuzi**

Mhe. Naibu Spika, kwa madhumuni ya kuweka utaratibu mzuri wa matumizi ya rasilimali fedha, idara iliandaa mpango wa manunuzi ya wizara kwa kipindi cha mwaka 2014/2015 ambao ulibainisha mahitaji ya manunuzi ya vifaa vya ofisi na huduma ulitumika kulingana na Sheria za Manunuzi ya Zanzibar. Aidha, idara ilitangaza tenda 6 zenye thamani ya shilingi 549.73 milioni kwa ununuzi wa bidhaa na tenda kumi (10) za utoaji wa huduma zenye thamani ya shilingi 380.78 milioni zilitangazwa.

**v. Kuimarisha vitengo vya Ukaguzi wa Ndani na Elimu Habari na Mawasilisano**

Mhe. Naibu Spika, wizara ina jukumu la kutoa taarifa zinazohusu masuala ya Biashara na Viwanda kwa wananchi kwa wakati. Kwa kuzingatia jukumu hili la msingi, wizara inatambua umuhimu wa matumizi ya TEHAMA katika kupokea, kutunza na kusambaza taarifa mbali mbali zinazohusu sekta hizi mbili.

Kwa mwaka wa Fedha wa 2014/2015 wizara imekiimarisha kitengo chake cha elimu, habari na mawasiliano kwa kukamilisha ujenzi wa maktaba na kununua vifaa vya ofisi hiyo. Aidha, kwa upande wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, wizara imekifanyia ukarabati pamoja na kukiwekea vifaa katika ofisi ya kitengo hicho.

**vi. Ushiriki wa Viongozi wa Wizara katika mikutano ya Nje**

Mhe. Naibu Spika, kwa madhumuni ya kuimarisha na kukuza masoko ya bidhaa zinazozalishwa hapa Zanzibar, wizara yangu ilijipangia kushiriki katika majadiliano ya Kikanda na Kimataifa kwa ajili ya kufikia lengo hilo. Katika kutekeleza lengo hili, idara iliratibu ushiriki wa safari tatu (3) za viongozi wa Wizara katika mikutano ya kikanda na Kimataifa. Mikutano hiyo ilikuwa na lengo la kuiwezesha nchi yetu kukuza fursa za kibiashara, masoko ya kikanda na yale ya kimataifa.

**IDARA YA BIASHARA NA UKUZAJI MASOKO**

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko imepangiwa kutekeleza majukumu kumi (10) kama ifuatavyo:

**i. Ukaguzi wa Mizani, Vituo vya Mafuta na Viwanda:**

Mhe. Naibu Spika, kazi hii katika kuangalia usahihi wa vipimo idara imefanya ukaguzi wa mizani, vituo vya mafuta, matangi ya mafuta, magari ya mafuta na mita za mafuta kama ifuatavyo:

| **Eneo la Ukaguzi** | **Lengo 2014/15** | | | **Utekelezaji** | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Unguja** | | **Jumla ya Zanzibar** | | | **Jumla ya Zanzibar** | |
| Mezani | 1960 | | 3460 | | | 2448 | |
| Vituo v | 41 | | 52 | | | 52 | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ya Mafuta | | | | | | | |
| Matangiya Mafuta | 36 | | 36 | | | 23 | |
| Magariya Maf | 12 | | 20 | | | 8 | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| uta | | | | | | | |
| Mitaza mafuta | 9 | | 12 | | | 12 | |

Aidha, Idara ilifanya mapitio ya kanuni zake za vipimo ambazo zilionekana kuwa zina upungufu na kukwaza utekelezaji sahihi wa kazi zetu au Sheria ya Mizani na Vipimo ya mwaka 1983. Hivyo, idara hii kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa serikali imetayarisha kanuni tisa (9) ambazo zinasimamia ukaguzi wa vipimo mbali mbali vya biashara.

**ii. Ukaguzi wa Maduka, Maghala, Bekari na Maduka Makubwa:**

Mhe. Naibu Spika, kwa madhumuni ya kusimamia mwenendo wa biashara na kumlinda mtumiaji idara inafanya ukaguzi wa bidhaa ili kubaini ubora wake pamoja na bei za bidhaa hizo. Katika kutekeza lengo hili Idara imefanya ukaguzi katika maeneo mbali mbali kama inavyoonesha hapo chini.

| **Eneo l** | **Lengo 2014/15** | | | **Utekelezaji** | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | [illegible] | | **Jumla** | [illegible] | | **Jumla** | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| a ukaguzi | a | | ya Zanzibar | a | | ya Zanzibar | |
| Maduka | 3,000 | | 3,800 | 2,081 | | 3,381 | |
| Maghala | 20 | | 30 | 20 | | 30 | |
| Bekari | 30 | | 61 | 30 | | 45 | |
| Ma | 0 | | 11 | 5 | | 10 | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | duka makubwa | | | | | | |

Mhe. Naibu Spika, katika ukaguzi huo bidhaa zenye thamani ya shilingi 8.25 milioni zilipatikana zikiwa zimepitwa na muda wake wa matumizi, ambapo bidhaa hizo ziliangamizwa kulingana na Sheria ya Kumlinda Mtumiaji. Bidhaa hizo zilizokamatwa ni pamoja na bidhaa za makopo, *diapers*, vyakula, bidhaa za matumizi ya nyumbani, mitumba na magodoro.

**iii. Elimu kuhusu Sheria Mpya ya Biashara ya mwaka 2013, na Kumlinda Mtumiaji:**

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza lengo hili, Idara iliandaa mpango kazi wa kutoa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya Sheria za Biashara. Katika kutekeleza mpango huo, vipindi vinne (4) vilirushwa ambavyo vilihusiana na mazungumzo ya moja kwa moja na wananchi kupitia televisheni. Aidha, mazungumzo na waandishi wa habari, pamoja na mikutano ya wadau wakiwemo *ZNCCIA*, *ZRB*, *TRA*, Manispaa, na Halmashauri za Wilaya, Ofisi ya Mrajisi wa Mali na Makampuni, Bodi ya Chakula, Madawa na Vipodozi yalifanyika.

**iv. Tamasha la Biashara:**

Mhe. Naibu Spika, kwa madhumuni ya kuhamasisha biashara na kuwakutanisha wanunuzi na wauzaji bila ya kuwepo mtu wa kati, Idara iliandaa tamasha la pili la biashara, lililofanyika sambamba na maadhimisho ya Sherehe za miaka 51 ya Mapinduzi. Tamasha hilo lilihudhuriwa na wafanyabiashara wapatao 140 kutoka Zanzibar na nje ya Zanzibar. Jumla ya biashara zenye thamani ya Shilingi 136. 9 milioni ilifanyika na maombi mapya (*orders*) yenye thamani ya Shilingi 35.0 milioni yaliwasilishwa kwa wafanyabishara.

**v. Maonesho ya Biashara na Misafara ya Kibiashara:**

Mhe. Naibu Spika, idara ilijipangia kushiriki na kuandaa maonesho mawili ya biashara, moja wapo ikiwa ni kuratibu ushiriki kwa Zanzibar katika Maonesho ya 38 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (*38 TH DTIF*) na kuandaa maonesho ya *Eid El Fitri*. Katika kutekeleza hilo, idara iliratibu ushiriki wa Zanzibar katika maonesho ya 38 ya kimataifa ya biashara yaliyofanyika huko Dar es Salaam katika mwezi wa July 2014, ambapo wajasiriamali 38 na Taasisi 3 za Serikali ziliweza kushiriki katika maonesho hayo. Idara pia kwa kushirikiana na *TANTRADE* ilifanikiwa kuandaa maonesho ya *Eid El Fitri* ambayo yalifanyika katika viwanja vya Maisara katika mwezi wa Agosti mwaka jana. Maonesho hayo yalikuwa maalum kwa ajili ya maandalizi na kusherehekea Sikukuu ya *Eid El Fitri*.

Mhe. Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa bidhaa za Zanzibar hasa zinazozalishwa na wajasiriamali na pia kuhakikisha kuwa wajasirimali wa Zanzibar wanapata fursa ya kutoka nje, idara ilipanga kuandaa msafara wa kibiashara mmoja kwa wajasiriamali kwa ajili ya kwenda kujifunza mbinu za biashara na masoko nje ya Tanzania. Kwa kutekeleza hilo, idara ilishiriki katika msafara ulioratibiwa na Wizara ya Uwezeshaji kuwapeleka wajasiriamali 38 wa Zanzibar kwenda nchini Rwanda kwa ajili ya kushiriki katika maonesho ya Juakali ya Afrika Mashariki.

**vi. Ushiriki wa Zanzibar katika Maonesho ya Milan (*Expo Milan*):**

Mhe. Naibu Spika, katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka jana nilizungumzia suala la ushiriki wa Zanzibar katika Maonesho makubwa ya Dunia yanayotegemewa kufanyika nchini Italia mwezi wa Mei–Oktoba mwaka 2015. Idara inaendelea na uratibu na maandalizi kwa ajili ya ushiriki wa Zanzibar ambapo washiriki wanane (8) wamejitokeza kushiriki. Aidha, idara imetayarisha filamu ambazo zitatumika kuonesha mnyororo wa thamani wa biashara ya viungo Zanzibar.

**vii. Ushiriki wa Zanzibar katika Mikutano ya Kibiashara ya Kimataifa:**

Mhe. Naibu Spika, katika kuimarisha biashara za kimataifa na kutanua wigo wa masoko, wizara ilipangia kushiriki mikutano 20 ya Kikanda na Kimataifa. Katika vikao hivyo kwa upande wa Afrika Mashariki wizara ilihudhuria katika Mkutano wa kumi na sita (16) wa Viongozi Wakuu wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na kikao cha thalathini (30) cha dharura cha Baraza la Mawaziri wa nchi wanachama kilichokutana kulizungumzia na kujadili masuala na taarifa mbali mbali za utekelezaji na programu zinazoendeshwa na Jumuiya hizo.

Aidha, idara ilishiriki mikutano miwili ya (*SADC*) iliyokuwa na maudhui ya kuendelea na majadiliano ya utekelezaji wa Itifaki ya Biashara ya Huduma kwa nchi wanachama kufunguliana milango ya kibiashara katika sekta za Mawasiliano, Fedha, Utalii, Uchukuzi, Nishati na Ujenzi.

**viii. Kurasimisha wafanyabiashara wadogo wadogo:**

Mhe. Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wadogo wadogo wa Zanzibar wanarasimishwa biashara zao, wizara ilipanga kuwapatia mafunzo jumla ya wafanyabiashara wadogo wadogo 1,000 wa Wilaya ya Kaskazini ‘B’ pamoja na Wilaya ya Mkoani kwa awamu ya kwanza. Na kuwapatia tena mafunzo kwa awamu ya pili kwa wafanyabiasha 50 ambao wanatoka katika Wilaya ya Kaskazini, Kusini, Magharibi na Mjini.

Katika kutekeleza lengo hili Wizara kwa kushirikiana na Mpango wa Kurasimisha Ardhi na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) imewapatia mafunzo wafanyabiashara 487 wa Wilaya ya Kaskazini 'B' na wafanyabiashara 500 wa Wilaya ya Mkoani katika awamu ya kwanza na kati ya hao, wafanyabiashara 50 ndio ambao hadi sasa wameweza kurasimisha biashara zao.

Mhe. Naibu Spika, aidha wizara kwa Kushirikiana na MKURABITA iliwapatia wafanyabaishara 50 mafunzo katika awamu ya pili kwa lengo la kuwawezesha kusajili biashara zao. Wafanyabiashara hao walipatiwa mafunzo yanayohusiana na uwekaji wa kumbukumbu za biashara, mafunzo ya uendeshaji wa biashara, mafunzo ya urasimishaji wa biashara na mafunzo yanayohusiana na masuala ya kibenki. Katika mafunzo hayo wafanyabiashara walipatiwa fomu za urasimishaji biashara na kati wafanyabiashara 50 waliopatiwa mafunzo hayo, 10 wamesharudisha fomu hizo kwa ajili kumaliza taratibu za usajili huo.

**ix. Kuhamasisha Matumizi ya Alama za Mistari (*Barcodes*) kwa Kampuni na Wazalishaji:**

Mhe. Naibu Spika, wizara katika kutekeleza hili na kwa kushirikiana na Jumuiya ya Wafanyabiashara, wenye Viwanda na Wakulima (*ZNCCIA*) iliendelea kuhamasisha wafanyabaishara kuhusu umuhimu wa matumizi ya alama za mistari kwa lengo la kukuza masoko ya bidhaa zao. Uhamasishaji huo ulifanyika kwa njia za mikutano, vipindi vya redio na katika majarida. Jumla ya alama (*Barcodes*) 205 zimeshatolewa kwa makampuni 25 hapa Zanzibar kwa mwaka 2014/15 ukilinganisha na alama 10 tu zilizokuwa zimetolewa hapo kabla.

**x. Kukusanya ada ya Shilingi 100.0 Milioni:**

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2014/2015, wizara ilikadiria kukusanya jumla ya Shilingi 100.0 milioni kutokana na ada za kazi za ukaguzi wa mizani na vipimo, vituo vya mafuta, ukaguzi wa magari ya mafuta na bidhaa zilizofungashwa katika viwanda (*pre-packed goods*). Hadi kufikia mwezi wa Mei, 2015, kiasi cha Shilingi 84.8 milioni zilikusanywa na kuingizwa katika mfuko wa Serikali. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 84.8 ya makadirio yote ya mwaka.

**IDARA YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UKUZAJI UJASIRIAMALI**

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Maendeleo ya Viwanda na Ukuzaji Ujasiriamali ilipangiwa kutekeleza malengo kumi (10), ambayo utekelezaji wake ni kama ufuatavyo:

**i. Mapendekezo ya Miradi ya Viwanda inayoweza kuwekezwa na Sekta Binafsi;**

Mhe. Naibu Spika, katika utekelezaji wa lengo hili, idara ilitathmini tafiti kumi na mbili (12) za viwanda kwa lengo la kukuza usarifu wa bidhaa. Kutokana na tathmini hiyo, jumla ya maandiko sita (6) ya miradi yametayarishwa. Maandiko hayo yanahusisha miradi ifuatayo:

i. Bekari ya biskuti (*Biscuit making plant*);
ii. Mradi wa kuchoma *chips* za mbatata, za ndizi na za muhogo (*Potato/banana/cassava chips plant*);
iii. Mradi wa kuzalisha *Tomato/chilli sauce plant;*
iv. Mradi wa kusarifu embe, mapapai na mananasi (*Mango, pawpaw and pineapple pulp & juice making plant*);
v. Kiwanda cha fanicha za mbao (Mradi wa *Wooden furniture making plant*);
vi. Mradi wa bidhaa za usumba (*Coconut coir products*); na
vii. *Tofee* na peremende

**ii. Kukuza Ujasilimali na Maendeleo ya Viwanda:**

Mhe. Naibu Spika, katika kuwasaidia wajasiriamali, idara imeendelea kutumia vigezo vinavyoeleweka katika kuwatambua wajasiriamali kwa ajili ya kuwasaidia. Vigezo hivyo ni pamoja na:
i. Uwepo wa wajasiriamali katika kikundi, ushirika au kongano (*cluster*)ambao wameonesha juhudi zao katika kuanzisha na kuendeleza miradi;

ii. Wajasiriamali ambao wamesajiliwa rasmi ndani ya Zanzibar na kufanya shughuli zao za uzalishaji hapa Zanzibar;
iii. Wajasiriamali wafungue akaunti (*account*) katika Benki yoyote hapa nchini;
iv. Wajasiriamali wapata msaada kutoka taasisi nyengine kwa haja hiyo hiyo wanayotaka kusaidiwa;
v. Kuwepo na kumbukumbu za mapato na matumizi za angalau miaka miwili;
vi. Mradi uwe wa uzalishaji endelevu wenye tija na wenye mchango mkubwa kwa jamii; na
vii. Mradi uwe wa uzalishaji na siyo biashara ya kuuza na kununua.

Misaada inayotolewa inajumuisha fedha taslimu, vitendea kazi pamoja na vifaa vya ujenzi.

Mhe. Naibu Spika, idara pia inaendelea kuandaa utaratibu mzuri wa kuwapatia vifungashio kwa urahisi na bei nafuu kupitia *"packaging scheme"*, ambapo hadi sasa, aina ya vifungasho vinavyotumiwa kwa wingi imeainishwa. Watengenezaji na wasambazaji wa vifunganisho hivyo wameshatafutwa na Wakufunzi watakaosaidia kutoa mafunzo kwa wajasiriamali wameshapatikana.

Mhe. Naibu Spika, kwa madhumuni ya kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya viwanda, idara imeandaa mapendekezo ya vivutio mahsusi kwa miradi ya viwanda ambayo yatazingatiwa na vyombo husika vya serikali. Miongoni mwa vivutio hivyo vinavyopendekezwa ni utaratibu rahisi wa kupatikana maeneo ya kujenga miradi ya viwanda, misamaha ya kodi kwa mashine, mitambo, malighafi na vifungashio vinavyohitajika viwandani na kudhibiti ulipaji kodi na ushuru kwa bidhaa shindani zinazoingizwa nchini.

**iii. Programu ya vifunganisho kwa wajasiriamali:**

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza lengo hili, idara imeainisha bidhaa zinazozalishwa kwa wingi na wajasiriamali wa hapa Zanzibar. Wajasiriamali hao huzalisha kwa wingi bidhaa za viungo, achari, sabuni za vipande na za maji, na jamu. Kutokana na wingi wa aina za bidhaa, wizara kwa kuzingatia au kwa kuanzia imeainisha vifungashio aina ya chupa na vikopo ambavyo vinatumika zaidi.

Madhumuni ya kuanzisha programu hii ni kuwarahisishia wajasiriamali kupata vifungashio kwa bei nafuu. Hata hivyo, pamoja na kutambua aina ya bidhaa na vifungashio hivyo, hatua ya ununuzi na usambazaji bado haijafanyika kutokana na uhaba wa fedha.

**iv.Utafiti wa Mchango wa Sekta ya Usarifu Bidhaa (manufacturing) katika uchumi wa Zanzibar:**

Mhe. Naibu Spika, idara imekamilisha utafiti wa mchango wa sekta ya usarifu bidhaa. Matokeo ya utafiti huo yanaonesha kwamba thamani ya bidhaa zilizozalishwa katika mwaka 2014 zilikuwa na thamani ya Shilingi 136.0 bilioni, ikiwa ni ongezeko la asilimia 5.5 kutoka mwaka 2013. Aidha, taarifa ya utafiti huo zimefanyiwa uchambuzi na hatimae kuwasilishwa kwa Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa ajili ya utoaji wa takwimu rasmi za serikali.

**v.Usajili na Ukaguzi wa Miradi ya Viwanda (*Industrial DataBase*):**

Mhe. Naibu Spika, katika kuisaidia miradi midogo midogo ya wajasiriamali, idara ilifanya ukaguzi wa miradi 221 Unguja na Pemba kwa lengo la kuangalia ubora na usafi katika uzalishaji wa bidhaa unaofanyika katika miradi hiyo. Kati ya miradi hiyo, mitano ni ya wakulima wa chumvi waliotembelewa ili kuona namna wanavyoyatumia mafunzo yaliyotolewa na *TIRDO* kuhusu njia bora za uzalishaji chumvi. Jumla ya miradi 86 mipya ilisajiliwa na kuingizwa katika daftari la usajili la viwanda. Baada ya ukaguzi huo, ushauri wa njia bora za kuzaalisha bidhaa zao ulitolewa na wajasiriamali waliahidi kuufanyia kazi.

**vi. Uratibu wa utekelezaji wa Sera ya Ujasiriamali (*SMEs*):**

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2013/2014, wizara yangu imepewa jukumu la uratibu wa utekelezaji wa Sera ya *SMEs*. Katika kutekeleza lengo hilo, Idara ya Maendeleo ya Viwanda iliendelea kufanya uratibu kupitia Kamati ya Ushauri inayojumuisha wajumbe kutoka Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

Pamoja na mambo mengine, kamati imeweza kuzitambua taasisi zote zinazojishughulisha na masuala ya maendeleo ya ujasiriamali ikiwemo kutoa mafunzo na mitaji. Aidha, kamati imeandaa orodha ya wakufunzi wote wa mafunzo hayo. Kwa sasa kamati inaendelea na kazi ya kuandaa mitaala ya pamoja ambayo itatumika na taasisi zote zinazotoa mafunzo ya ujasiriamali hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, idara inaendelea kushirikiana na taasisi mbali mbali katika utekelezaji wa Sera ya *SMEs* hapa nchini. Baadhi ya matukio ya mashirikiano ni ugawaji wa vihori kwa ajili ya kuvunia mwani, Unguja na Pemba. Aidha, kufanyika kwa kikao cha pamoja na Uongozi wa Jumuiya ya Wafanya Biashara Wenye Viwanda na Wakulima (*ZNCCIA*) juu ya uanzishwaji wa program ya kuwatumia wazalishaji wadogo wadogo kutoa huduma katika miradi mikubwa (*sub-contracting partnership exchange – SPX*).

Programu hiyo tayari imeshaanza ambapo Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Viwanda (*UNIDO*) linashirikiana na taasisi mbali mbali ikiwemo *ZNCCIA*, Wizara ya Uwezeshaji, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko katika kuwajengea uwezo Wajasiriamali wa kuzalisha bidhaa zenye ubora, kutafuta masoko ndani na nje ya nchi na kuomba zabuni kwenye makampuni na kutoka serikalini.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na juhudi zinazochukuliwa na wizara yangu katika kuwasaidia wafanyabiashara wadogo wadogo, ikiwemo misaada ya fedha, vitendea kazi, vifaa vya ujenzi, mafunzo ya ujasiriamali, masoko ya bidhaa zao kupitia safari za maonesho ya ndani na nje ya nchi, bado kuna changamoto nyingi zinazowakabili. Miongoni mwa changamoto hizo ni:

i. Mitaji midogo ya kuanzisha na kuendeleza miradi hiyo;
ii. Kasoro katika mafunzo wanayopatiwa wajasiriamali;
iii. Uwezo mdogo wa wazalishaji;
iv. Upatikanaji wa mikopo kutoka katika taasisi za fedha;
v. Taaluma ndogo katika mbinu za utafutaji masoko; na
vi. Kiwango kikubwa cha riba.

**vii. Mafunzo kwa Wajasiriamali:**

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza lengo hili idara ilitoa mafunzo ya siku tatu juu ya ujasiriamali katika kijiji cha Nungwi kwa vikundi 17 vya Mkoa wa Kaskazini, Unguja. Mafunzo hayo yatawasaidia wajasiriamali kuweza kuzalisha bidhaa zilizo na ubora na kuendesha miradi yao kwa ufanisi. Aidha, kwa upande wa utoaji wa misaada vikundi vya ushirika wa wasarifu wa embe Cheju na wajasiriamali walemavu wanaozalisha bidhaa za ngozi cha Mwembe Makumbi vilitembelewa kwa ajili ya kuangalia uwezekano wa kupewa misaada. Kufuatia ziara hiyo, wizara kwa ushirikiano na Wizara ya Uwezeshaji pamoja na Bodi ya Vyakula na Madawa imewasaidia wajasiriamali wa Cheju kuimarisha uzalishaji wa bidhaa zao kwa kuzingatia ubora.

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza lengo hili, Idara ilitoa mafunzo ya siku tatu (3) juu ya ujasiriamali kwa vikundi kumi na saba (17) vya Mkoa wa Kaskazini Unguja. Mafunzo hayo yalikuwa maalum kwa vikundi hivyo ambapo Idara ilishirikiana pia na Taasisi ya *Laybaika* ya huko Nungwi.

**viii. Majadiliano ya Kikanda na Kimataifa kuhusu Maendeleo ya Viwanda;**

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza lengo hili, Maofisa wa Idara walipata fursa ya kushiriki katika Matamasha, Makongamano, Semina, Warsha na Majadiliano yaliyofanyika katika nchi mbali mbali ikiwemo Botswana, Kenya, Rwanda,

Burundi, Tanzania Bara na Singapore. Majadiliano hayo yalisaidia katika kuwajengea uwezo washiriki na kubadilishana uzoefu baina ya washiriki na mataifa kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza lengo hili, Maofisa wa Idara walipata fursa ya kushiriki katika majadilianao mbali mbali yanayohusu maendeleo ya viwanda. Miongoni mwa majadiliano hayo ni *"East Africa Pack"* kuhusu masuala ya *packaging*, Kikao cha Kamati ya pande tatu za Kanda ya *EAC*, *SADC* na *COMESA* kuhusiana na maendeleo ya viwanda, kikao cha kuendeleza maeneo ya Viwanda (*Industrial Park Development and Industrial Policies Programme*) zilipatikana fursa hizo Mhe. Naibu Spika.

**ix. Taarifa ya Ushindani wa Kiviwanda ya mwaka 2014 (*Industrial Competitiveness Report*):**

Mhe. Naibu Spika, katika ushindani wa kiviwanda Kiviwanda ya mwaka 2014 *Industrial Competitiveness Report:*

Mhe. Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Kuendeleza Viwanda *UNIDO* inaendelea kutekeleza mradi wa kujenga uwezo wa wafanyakazi wake na wadau wakuu kwa kuandaa na kuchambua sera ya viwanda kwa ajili ya kuandaa taarifa ya ushindani kiviwanda kila mwaka *Tanzania Industrial Competitiveness Report*. Kwa mwaka huu Idara imekusanya taarifa za uzalishaji viwandani na kuzifanyia uchambuzi ambapo rasimu ya Ripoti kwa upande wa Zanzibar imetayarishwa na kuwasilishwa kwa *UNIDO* ili kujumuisha katika Ripoti moja ya Tanzania.

**OFISI KUU YA WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO – PEMBA**

Mhe. Naibu Spika, Ofisi kuu ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko iliopo Pemba pia iliendelea kufanya uratibu wa shughuli za wizara kwa upande wa Pemba zikiwemo shughuli zote za utawala, kuimarisha mazingira ya kufanya biashara na viwanda kwa upande wa Pemba, na kuratibu shughuli za wajasiriamali kisiwani humo.

Utekelezaji wa malengo ya Ofisi ya Pemba ni kama yalivyoelezwa katika taarifa zilizoelezwa hapo awali za utekelezaji wa Idara husika ambayo yatatekelezwa kwa upande wa Pemba.

## TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

**Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*):**

Mhe. Naibu Spika, Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015. Shirika limetekeleza malengo yake kama ifuatavyo:

**Ununuzi na usafirishaji wa Karafuu:**

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa ununuzi wa karafuu, Shirika la *ZSTC* lilijiwekea lengo la kununua tani 2,800 za karafuu zenye thamani ya TZS 39.2 bilioni. Hadi kufikia tarehe 12 Juni, 2015, jumla ya tani 2,822 zenye thamani ya TZS 39.48 bilioni zilinunuliwa kutoka kwa wakulima. Karafuu hizo zimenunuliwa kwa viwango vya bei vifuatavyo:-

Daraja la 1 - TZS14,0
Daraja la 2 - 00
Daraja la 3 - TZ12,0
- 00
-TZ10,0
-00

Mhe. Naibu Spika, Kwa upande wa usafirishaji jumla ya tani 2,772.2 ziliuzwa nje kwa thamani ya TZS 66.5 bilioni sawa na *USD* 30.95 milioni. Aidha, mwenendo wa bei ya karafuu kwa siku za karibuni unaonesha kuteremka kufikia *USD* 9,000 kwa tani kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa zao hilo kwa nchi za India na Indonesia.

**Kiwanda cha Mafuta ya Makonyo:**

Mhe. Naibu Spika, katika kuendeleza uimarishaji wa Kiwanda cha Makonyo, Shirika limefanya mambo yafuatayo:

i. Utengenezaji wa mitambo ya kiwanda na kuweka vifaa vyengine katika mashine hizo;

ii. Ununuzi wa mashine ya kupimia viwango vya mafuta yanayozalishwa;

iii. Upandaji wa miti katika hekta mbili (2) kwenye eneo la Shamba la Mtakata ili kuongeza uzalishaji wa malighafi inayohitajika katika kiwanda hicho; na

iv. Ushiriki wa maonesho ya Oman kwa ajili ya kuzitangaza bidhaa za mafuta ya mimea zinazozalishwa na Kiwanda hicho, na ushiriki katika Tamasha la Utamaduni nchini Ujarumani.

**Uzalishaji wa Mafuta ya Makonyo na Mimea:**

Mhe.Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2014/2015, kiwanda cha makonyo kiliweza kuzalisha jumla ya tani 10.24 za mafuta ya makonyo na mimea zenye thamani ya TZS 278.76 milioni. Hadi kufikia Machi 2015, jumla ya mafuta ya makonyo na mimea yenye thamani ya TZS 58.9 milioni yaliuzwa katika kipindi hicho.

**Ushirikiano wa *ZSTC* na *Land Company:***

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2014/2015 kuhusiana na ushirikiano wa kibiashara baina ya *ZSTC* na Kampuni ya *Land* ya Japan. Napenda kuliarifu Baraza lako kuwa ushirikiano huo bado unaendelea na hivi karibuni mtaalamu kutoka *ZSTC* anatarajiwa kwenda Japan kujifunza jinsi ya kutengeneza mafuta ya mimea.

**Mageuzi ya *ZSTC*:**

**a.Muundo wa Kitaasisi**

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa utekelezaji wa mageuzi ya *ZSTC*, Shirika limeajiri wafanyakazi wapya 13 katika fani ya *IT*, Masoko na Uongozi wa Biashara.

**b. Kuimarisha Masoko**

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa 2014/2015, Shirika liliendelea na kutekeleza majukumu mbali mbali kwa lengo la kuimarisha masoko ya idhaa zake ndani na nje ya nchi. Hatua zilizochukuliwa ni kama ifuatavyo:

i. Kushiriki maonesho ya biashara nje na ndani ya nchi;

ii. Kuimarisha ubora wa bidhaa za Shirika na vifungashio vyake;

iii. Kuanzisha mtandao wa maduka ya kuuzia bidhaa zake kwa ujazo mdogo mdogo;

iv. Kuweka kituo cha usarifu wa kilimo hai *Organic Farming* kwa

mazao ya mdalasini, pilipili hoho, karafuu na pilipili manga; na

v. Utafiti wa ubora na upekee wa karafuu za Zanzibar ikilinganishwana karafuu za nchi nyengine.

Mhe. Naibu Spika, uuzaji wa karafuu kwa ujazo mdogo mdogo kwa msimu wa 2014/2015 uliendelea vizuri ambapo mauzo yake yalifikia tani 1.1 yenye thamani ya TZS 40.9 milioni. Kwa upande wa uuzaji wa zao hilo kupitia tawi la Shirika la Dubai mauzo ya tani 255 yenye thamani ya *USD* 2.94 milioni sawa na TZS 5.1 bilioni yalifanyika.

Mhe. Naibu Spika, hatua nyengine zilizochukuliwa na Shirika kwa ajili ya kuimairisha masoko ni kuandaa maeneo maalum ya uuzaji wa karafuu na mazao mengine kwa kutumia tasnia ya malibunifu *branding* na karafuu hai (*Organic)*.

Ghala la Shirika liliopo katika eneo la Saateni limekarabatiwa kwa viwango vinavyokubalika na taasisi zinazosimamia ubora wa chakula kwa ajili ya utayarishaji wa bidhaa hizo. Kadhalika, wafanyakazi wote watakaohusika na kazi za usarifu huo wameshapimwa afya zao na kwamba Shirika limeshapatiwa ithibati (*certificate)* na Taasisi ya Afrika ya Mashariki inayohusika na utoaji ithibati ya mazao ya "*Organic*".

Mhe. Naibu Spika, kwa madhumuni ya kuimarisha ufanisi wa mfumo wake wa masoko, Shirika limeanzisha utafiti wa kulitathmini tawi la Dar es Salaam kwa lengo la kuliimarisha kibiashara ili liweze kuchangia utekelezaji wa shughuli za msingi *core functions* za Shirika. Utafiti huo unaendeshwa na wataalamu kutoka Chuo cha Uongozi wa Fedha, Zanzibar.

**Matokeo ya Mageuzi ya Shirika**

Mhe.Naibu Spika, Katika kipindi cha miaka minne sasa, Shirika liliendelea na utekelezaji wa mpango wa mageuzi katika maeneo yafuatayo:

i. Kuimarisha mifumo ya ndani ya utendaji kazi pamoja na misingiya kisheria;

ii. Kuimarisha wigo wa mfumo wa uendeshaji masoko;

iii. Kuimarisha mfumo wa fedha na udhibiti wa ndani; na

iv. Kuimarisha huduma za ununuzi wa karafuu na kujenga mahusiano mazuri ya Shirika kwa jamii.

Mhe. Naibu Spika, Utekelezaji wa mageuzi hayo, umeleta mabadiliko makubwa katika tija ya Shirika ambapo sasa limeweza kugeuza mwenendo wa miaka mingi wa kuwa na biashara yenye hasara na badala yake kuwa na faida *financial turn-round*. Hivi sasa Shirika linalipa kodi ya mapato na kulipa gawio kwa mwenye hisa (Serikali). Kwa mfano kwa hesabu zilizokaguliwa katika mwaka 2011/2012, 2012/2013 na makadirio kwa hesabu za 2013/2014, Shirika limelipa jumla ya TZS 1.8 bilioni kama kodi ya mapato na kulipa gawio *dividend* la TZS 500.0 milioni kwa mwaka wa 2013/2014.

Changamoto kubwa zinazoikabili Shirika, he. Naibu Spika, ni pamoja na uchafuzi Karafuu, ugumu wa soko la mafuta ya karafuu na mimea mengine na urudishaji mikopo wanayokopeshwa wakulima.

Mhe. Naibu Spika, Kwa upande wa uchafuzi wa karafuu, imejitokea tabia kwa baadhi ya wakulima kuchanganya karafuu na makonyo au vitu visivyostahiki kuwemo katika karafuu, jambo ambalo linaweza usababisha kuharibu sifa na ubora wa karafuu za Zanzibar. Hali hiyo imeonesha kuwa katika kipindi cha kuanzia mwezi Novemba, 2014 hadi mwezi Machi, 2015 jumla ya kilo 5,849 zilizowasilishwa vituoni zilikuwa na kilo 856.5 za takataka hizo. Kiwango hicho ni wastani wa tani moja ya karafuu imechanganywa na kilo 143 za makonyo na takataka nyengine zisizostahiki.

Uchanganyaji huu Mheshimiwa Spika, unaweza kuleta athari kubwa hasa kwa vile Serikali hivi sasa imo katika maandalizi ya kuilinda karafuu ya Zanzibar kwa kutumia Tasnia ya Malibunifu.

**Taasisi ya Viwango Zanzibar – *ZBS*:**

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2014/15 Taasisi ya viwango Zanzibar imetekeleza malengo yake iliyojiwekea kama ifuatayo:

**Kuandaa Viwango vya bidhaa**

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza lengo hili, Taasisi iliandaa jumla ya Viwango 24 ambavyo vilithibitishwa na kutangazwa rasmi. Aidha, Taasisi inaendelea na utayarishaji wa viwango 40 ambavyo vipo katika hatua ya mwisho.

**Kufanya Ukaguzi (*Inspection*), Uthibiti (*Certification*) na Upimaji (*Testing*) wa bidhaa**

Mhe. Naibu Spika, Katika utekelezaji wa majukumu yake ya msingi, Taasisi

ya Viwango ya Zanzibar imeanza kufanya shughuli ya uthibiti wa ubora wa bidhaa kukagua kiwanda cha uzalishaji wa maji cha *Aqua Blue* pamoja na kufanya ukaguzi wa bidhaa kwa wajasiriamali. Katika ukaguzi huo kasoro mbali mbali zinazohusiana na ufungashaji na usafi katika uzalishaji zilibainika katika hatua za uzalishaji, ambapo maelekezo ya marekebisho
kuhusiana na kasoro hizo yalitolewa kwa wahusika.

**Kubadilishana uzoefu wa Kitaalamu**

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza lengo hili, Taasisi ya Viwango ya Zanzibar ilifanya ziara za mafunzo zenye madhumuni ya kujifunza na kuimarisha mashirikiano baina yake na Taasisi kama hizo za kikanda. Mashirika yaliyotembelewa ni Shrika la Viwango la Botswana pamoja na Shirika la Viwango la Rwanda. Aidha, ziara zimesaidia kufahamu mbinu, mifumo na taratibu zilizopelekea mafanikio katika utekelezaji wa majukumu na shughuli za Taasisi hizo.

**Usaidizi kwa Wajasiriamali**

Mhe.Naibu Spika, kwa lengo la kutoa usaidizi kwa wajasiriamali, Taasisi imewapatia mafunzo wajasiriamali 74 wanaozalisha bidhaa za aina ya vyakula na vipodozi Unguja na Pemba. Mafunzo hayo ambayo yalihusiana na viwango, taratibu za uthibiti ubora na usafi katika uzalishaji na vifungashio, yalitolewa kwa ajili ya kuwawezesha kuzalisha bidhaa zenye ubora na zinazokubalika katika soko la ndani na nje.

**Mafunzo kwa Wafanyakazi**

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza lengo hili, jumla ya wafanyakazi 23 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi katika fani tofauti. Mafunzo hayo yalihusu fani za uandaaji wa viwango, upimaji katika maabara, mifumo ya ubora, ukaguzi na ugezi *calibration*.

**Kuimarisha Mazingira ya Kazi**

Mhe. Naibu Spika, Kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya mwaka wa fedha uliopita, Taasisi ilikamilisha hatua za maandalizi ya ujenzi wa Makao Makuu yake katika eneo la Maruhubi na kufanya ukarabati wa ofisi zake za muda katika eneo la Amani. Ujenzi katika jengo la Makao Makuu bado aujaanza kutokana na mahitaji makubwa ya kifedha za ujenzi. Hata hivyo, ili kuiwezesha Taasisi kuanza kazi zake, ujenzi wa vyumba vya maabara ya kupimia bidhaa za chakula na kemikali zimejengwa katika eneo la ofisi zake zilioko Amani.

Kwa upande wa uimarishaji wa ofisi, kazi ya ujenzi wa sehemu ya maabara inaendelea. Kazi hiyo itakapokamilika *ZBS* itakuwa na sehemu ya maabara mbili zitakazoshughulika na upimaji wa bidhaa za chakula na kemikali. Aidha, hatua za ununuzi wa vifaa kwa ajili ya maabara hizo zinatarajiwa kuchukuliwa baada ya kukamilika ujenzi huo.

**Elimu ya Matumizi ya Viwango na uthibiti ubora wa Bidhaa**

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza lengo hili, hatua za kutoa elimu juu ya matumizi ya viwango na bidhaa zenye ubora zinaendelea utekelezwa ambapo vipindi sita (6) vya redio vilirushwa hewani. Aidha, taaluma ilitolewa kwa wananchi mbali mbali waliofika katika banda la *ZBS* wakati wa tamasha la pili la Biashara mwezi wa Januari 2015.

**Wakala wa Vipimo na Kamisheni ya Ushindani**

Mhe. Naibu Spika, Kama nilivyoeleza hapo awali kuhusiana na juhudi za Wizara yangu katika kuandaa Sera ya Kumlinda Mtumiaji ambayo itapelekea kufanyiwa mapitio kwa Sheria ya Kumlinda Mtumiaji pamoja na Sheria ya Mezani na Vipimo ambazo zitaanzisha Taasisi hizi mbili. Utekelezaji wa malengo ambayo yalipangwa kutekelezwa chini ya Taasisi hizi mbili kwa mwaka 2014/2015. Umeelezwa katika Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko.

**Baraza la Biashara la Zanzibar (*ZNBC*)**

Mhe. Naibu Spika, Baraza la Biashara la Zanzibar lilijiwekea kutekelea majukumu yake kwa kutunga Sheria ya Baraza hilo, kuandaa mikutano ya Baraza pamoja na kuandaa vikao vya kamati Tendaji ya Baraza.

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu hayo, Mikutano miwili ya Baraza ilifanyika ambapo mada zinazohusiana na Uimarishaji wa Mazingira ya Biashara zilijadiliwa. Katika mikutano hiyo, wajumbe walikubaliana kuanzishwa kwa Kamati ndogo ndogo za kisekta ili kushughulikia changamoto za kibiashara ambazo zinajitokeza mara kwa mara bila ya kusubiri kikao cha Baraza kutatua changamoto hizo. Kamati hizo zitaongozwa na mawaziri wa Serikali ili kuharakisha utekelezaji wa maamuzi yake. Aidha, Baraza liliamua kuifanyia mapitio hati ya Kuanzisha Baraza hilo, ili iendane na mazingira ya uendeshaji wa Baraza badala ya kutunga Sheria mpya kwa ajili hiyo.
Mhe. Naibu Spika, Kwa upande wa uandaaji wa vikao vya Kamati Tendaji ya Baraza, jumla ya vikao sita (6) vilifanyika. Vikao hivyo vilikutana kwa lengo la kuandaa Mkutano wa nane wa Baraza hilo la Biashara la Zanzibar, ambao

ulifanyika tarehe 16 Disemba, 2014.

**Baraza la Usimamizi wa Mfumo wa Utoaji Leseni za Biashara**

Mhe. Naibu Spika, Baraza la Usimamizi wa Mfumo wa Utoaji Leseni (*Business Licensing Regulatory Council)* limeundwa chini ya Sheria Nam. 13 ya mwaka 2013, iliyopitishwa na Baraza lako tukufu. Madhumuni makubwa ya kutungwa kwa sheria hiyo ni kuweka mfumo mzuri na rahisi wa utoaji wa leseni, vibali na ruhusa nyengine za biashara.

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2014 - 2015 utekelezaji wa sheria hiyo umeanza kwa kufanya mambo yafuatayo:

i. Kuteua Mtendaji wa Baraza;
ii. Kutafuta jengo kwa ajili ya ofisi ya Baraza ambalo maandalizi ya ukarabati wake umeshaanza;

Aidha, nyaraka muhimu za kusimamia uendeshaji wa Baraza hilo kama vile Mpango Mkakati, muundo wa Baraza na kanuni zinaendelea kutayarishwa.

**PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA 2015/2016**

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko itatekeleza programu kuu nne (4) kama zifuatavyo:

i. Programu ya Utawala na Uendeshaji;
ii. Programu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali;
iii. Programu ya Ukuzaji na Uendelezaji Biashara; na
iv. Programu ya Viwango na Uthibiti *certification* Ubora wa Bidhaa.

**Programu ya Utawala na Uendeshaji**

Mhe.Naibu Spika, Programu hii itakuwa na programu ndogo zifuatazo:

i. Uendeshaji wa Shughuli.

ii. Mpango, Sera na Uafiti.

Mhe.Naibu Spika, programu ndogo ya Uendeshaji wa shughuli za Biashara, Viwanda na Masoko itakuwa na jukumu la kutoa huduma za kiutawala,

uendeshaji, ununuzi, fedha na maendeleo ya wafanyakazi. Ili kutekeleza majukumu yake, programu hii ndogo imepangiwa matumizi ya TZS 1,562.90 milioni kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Naibu Spika, Kwa upande wa program ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti ambayo itakuwa na jukumu la kutayarisha, kuchambua na kutathimini utekelezaji wa mipango na malengo maalum ya Wizara imepangiwa matumizi ya TZS 442.57 milioni kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016.

Kadhalika, programu ndogo ya Ofisi Kuu Pemba ambayo itasimamia uendeshaji wa shughuli za Biashara, Viwanda na Masoko kwa upande wa Pemba imepangiwa matumizi ya TZS 355.17 milioni kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016.

Mhe. Naibu Spika, Ili kuweza kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2015/2016, Programu ya Utawala na Uendeshaji imetengewa TZS 2,360.64 milioni.

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya ukuzaji Viwanda itakuwa na jukumu la kuandaa sera na mkakati wa maendeleo ya viwanda na kusimamia utekelezaji wake. Ili kutekeleza majukumu hayo, programu hii ndogo imepangiwa matumizi ya TZS 191.02 milioni kwa mwaka 2015/2016.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa programu ndogo ya Ukuzaji Ujasiriamali, ambayo itakuwa na jukumu la kuratibu utekelezaji wa mikakati ya maendeleo ya wazalishaji wadogo wadogo na wajasiriamali wengine imetengewa TZS 700.35 milioni kwa mwaka 2015/2016.

Mhe. Naibu Spika, Ili kutekeleza majukumu ya Programu ya Maendeleo ya Viwanda na Ukuzaji Ujasiriamali kwa mwaka 2015/2016 jumla ya TZS 891.37 milioni zimetengwa kwa ajili hiyo.

**Programu ya Ukuzaji na Uendelezaji Biashara**

Mhe.Naibu Spika, Programu ya tatu itakayotekelezwa na Wizara kwa mwaka 2015/2016 ni Ukuzaji na Uendelezaji Biashara. Kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa malengo yake, programu hii imegawanywa katika programu ndogo ndogo tatu kama ifuatavyo:

i. Ukuzaji Masoko na Usafirishaji bidhaa nje;

ii. Ushindani wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji; na

iii. Biashara ya Ndani na Urahisishaji Biashara.

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya Ukuzaji Masoko na usafirishaji bidhaa nje inahusika na uratibu wa maonesho ya biashara, takwimu za biashara za nje, utekelezaji wa Mkakati wa usafirishaji bidhaa na biashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara. Ili kutekeleza majukumu yake kwa mwaka 2015/2016 programu hii ndogo imetengewa TZS 423.93 milioni.

Kwa upande wa programu ndogo ya Ushindani wa Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji ambayo itakuwa na jukumu la kuandaa Sera na Sheria zitakazowezesha uwepo wa Ushindani wa biashara na kumlinda mtumiaji imetengewa jumla ya TZS 142.36 milioni kwa mwaka 2015/2016.

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo nyengine chini ya Programu ya Ukuzaji na Uendeshaji Biashara ni Biashara za ndani na Urahisishaji Biashara. Programu hii ndogo itakuwa na jukumu la kuweka taratibu rahisi za uendeshaji biashara kama vile upatikanaji wa nyaraka muhimu za usafirishaji au uagiziaji bidhaa zinazotolewa na taasisi za Serikali na kusimamia ushindani. Ili kutekeleza majukumu ya programu hii ndogo jumla ya TZS
690.04 milioni zimetengwa kwa ajili hiyo.

Mhe. Naibu Spika, Ili kutekeleza majukumu ya Programu ya Ukuzaji na Uendeshaji Biashara kwa mwaka 2015/2016 jumla ya TZS 1,256.33 milioni zimepangwa kwa ajili hiyo.

**Programu ya Viwango na Uthibiti (*Certification*) Ubora wa Bidhaa**

Mhe. Naibu Spika, Programu hii itakuwa na jukumu la kuweka viwango kwa bidhaa mbali mbali, kuthibitisha *certification* ubora wa bidhaa na upimaji wa bidhaa mbali mbali kwa lengo la kulinda afya na usalama wa watumiaji wa bidhaa hizo. Kwa ajili ya ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yake, Programu hiyo imeundiwa programu ndogo ndogo moja ya Uthibiti wa Bidhaa. Jumla ya TZS 2,100 milioni zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii ndogo.

Mhe. Naibu Spika, Taarifa kamili ya Wizara hii zimeelezwa kuanzia ukurasa wa 672 hadi ukurasa wa 700 wa kitabu cha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Bajeti inayotumia Programu (*PBB*) kwa mwaka wa fedha 2015/2016 – 2017/2018.

**SHUKURANI**

Mhe. Naibu Spika, Mafanikio ya Wizara niliyoyaeleza katika hotuba yangu ni matokeo ya mashirikiano makubwa niliyoyapata kutoka kwa Wajumbe wa

Baraza hili chini ya uongozi wako mahiri. Ninakushukuru wewe binafsi, Wenyeviti wa Kamati za kudumu za Baraza na Wajumbe wote kwa ushauri na michango yao mliyotupa katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti yetu.

Mhe. Naibu Spika, Sina budi kukiri vile vile kuwa mafanikio ya kiutendaji yaliyojitokeza katika kipindi cha mwaka 2014/2015 ni matokeo ya ushirikiano mkubwa ambao Wizara yangu iliupata kutoka kwa wadau mbali mbali wa ndani na nje ya nchi yetu. Kwa madhumuni ya kutambua mchango mkubwa wa Wadau hao kwa Wizara, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa nchi na taasisi za ndani na nje hususan zifuatazo:-

(i) Jamhuri ya watu wa China;
(ii) India;
(iii) Serikali ya Marekani;
(iv) Shirika la Kimataifa la Kusimamia Malibunifu *World Intellectual Property Organisation – WIPO*;
(v) Kituo cha Biashara cha Kimataifa *International Trade Centre ITC*
(vi) *UNDP*
(vii) Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda *UNIDO*
(viii) *World Bank*
(ix) *WTO*
(x) *JICA*
(xi) *Commonwhealth Secretariat*
(xii) *TNBC*
(xiii) Wafanyakazi wote wakubwa na wadogo na Wawekezaji wa Sekta ya Viwanda.

Mhe**.** Naibu Spika, napenda nichukue fursa hii kwa mara nyengine tena kuwapongeza kwa dhati wafanyakazi wote wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kazi kubwa yenye ufanisi mzuriwanayoifanya kila siku licha ya ukabiliwa na changamoto mbali mbali. Ni matarajio yangu kwamba wataongeza juhudi zao ili kuzidisha ufanisi kwa kuwahudumia wananchi na kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Kadhalika, napendakuwapongeza wafanyakazi wote walioshiriki katika maandalizi ya Hotuba hii kwa kazi nzuri waliyoifanya. Aidha, nawaombea dua njema katika kazi zao.

Mhe. Naibu Spika, Naomba kutumia nafasi hii pia kuwashukuru wafanyabiashara wote wakubwa, wakati na wadogo, mpaka Juakali na wengine kwa juhudi zao kubwa za kuwahudumia wananchi kwa kuwapatia bidhaa mbali mbali muhimu kama vile nguo, chakula, vyombo vya moto na vifaa vya ujenzi.

Nawaomba waendelee kushirikiana na Wizara yangu kwa kufanya kazi pamoja kwa lengo la kuimarisha biashara na kutoa huduma bora kwa wananchi na vile vile wawahurumie wananchi katika mwezi huu hasa wa Ramadhani.

Nawaomba wafanyabiashara wote kuwahurumia wananchi kwa kuwawekea bei nafuu za bidhaa ili waweze kumudu maisha yao. Aidha, nawaomba wafanyabiashara waelekeze nguvu zao katika uwekezaji wa viwanda na biashara ya viungo (*spices*) kama vile mdalasini, manjano na viungo vyengine, na usindikaji samaki ili kunyanyua usafirishaji bidhaa na kuongeza thamani ya bidhaa zetu na biashara. Kadhalika, kwa kutambua mchango mkubwa kwa wawekezaji wa viwanda, naomba pia Mhe. Naibu Spika, kuchukua nafasi hii kutoa pongezi za dhati kwa:

a. *Bakhressa Group of Companies;*
b. *Kiwanda cha Sukari Mahonda;*
c. *Zainab Bottlers;*
d. *Drop of Zanzibar*
e. *Super Pure*
f. *Zan Bottling*
g. *ZATEPA*
h. *Zenji Sky Cola.*
i. *Allawys Supplies;*

Mhe. Naibu Spika, Juhudi zao za kuimarisha viwanda nchini zinaweka njia kwa wafanyabiashara wengine kuwekeza katika viwanda.

Mhe. Naibu Spika, Hotuba yangu hii haitokamilika kama sijatoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wangu wa Jimbo la Mtoni kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipa na kunivumilia pale ninapokua mbali nao kutokana na majukumu mengine ya kitaifa yanayonikabili. Nakiri kwamba imani na heshima yao kwangu ni kubwa na ya kipekee na ninaithamini sana wala siwezi kuilipa. (*Makofi*)

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |

***(Hapa zinaingia tables za viambatanisho ambapo nimeviweka chini ya Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati kutokana na kuchapwa katika hali isiyo ya kawaida ya programu hii)***

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri, hoja imeungwa mkono. Waheshimiwa Wajumbe, kabla hatujaanza kuchangia tumepata wageni katika Baraza letu. Kwa hivyo, naomba niwatambulishe kwenu. Wageni hao wamekuja kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi na jumla yao ni 70 wanatoka Skuli inayoitwa *Alhidaya Islamic School* kutoka Chukwani, wanaongozwa na walimu watano na Mwalimu Mkuu Ndugu Mohamed Omar Mohamed.(*Makofi*).

Naomba wote wasimamie, wanafunzi na walimu. Karibuni sana mujifunze, leo tupo sisi kesho mutakuwa nyinyi, karibuni sana na ninawaomba wakae. (*Makofi*)

Waheshimiwa, tunaanza kuchangia, kwanza tunamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, baadae afuatie Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali afuatie.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**Mhe. Viwe Khamis Abdalla: (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na kilimo):** Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Naibu Spika, Awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu, Mwingi wa Rehema na Mwenye Kurehemu, ambaye ametujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo tukiwa ndani ya Baraza lako tukufu, tukitekeleza majukumu yetu mbali mbali ya kuwatumikia wananchi wetu ambapo leo tunajadili Bajeti ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Naibu Spika, kwa dhati kabisa, napenda pia kukushukuru wewe binafsi Mhe. Naibu Spika kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Naibu Spika, Nichukue nafasi hii pia kuishukuru na kuipongeza Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kuweza kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu Bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kwa ufanisi na umahiri mkubwa katika mfumo mpya wa bajeti unaozingatia programu *"Programme Based Budget"* (*PBB*).

Mhe. Naibu Spika, Kwa namna ya pekee sasa napenda kuwapongeza na kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa ushirikiano wao mkubwa wanaotupa wakati wa kuipitia bajeti ya Wizara hii. Naomba niwatambue kwa kuwataja kwa majina Waheshimiwa Wajumbe hao pamoja na Makatibu wake kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Hija Hassan Hija - Mwenyekiti
2. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Mjumbe
4. Mhe. Hamad Masoud Hamad - Mjumbe
5. Mhe. Raya Suleiman Hamad - Mjumbe
6. Mhe. Asha Abdu Haji - Mjumbe
7. Ndg. Fatma Omar Ali - Katibu
8. Ndg. Haji Khatib Haji - Katibu

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko ina jukumu la kusimamia masuala ya biashara na maendeleo ya viwanda nchini ikiwa ni pamoja na kuhakikisha tunakuwa na masoko ya uhakika ya bidhaa zetu ndani na nje ya nchi yetu. Majukumu haya sio madogo, ni makubwa kwa maendeleo ya nchi yetu na hasa ukizingatia kuwa sekta hii ya biashara na viwanda ni kichocheo kikubwa cha maendeleo ya uchumi popote pale duniani.

Mhe. Naibu Spika, taarifa zinaonesha kuwa mwenendo wa bei za bidhaa muhimu hapa nchini uliendelea kuwa wa utulivu kwa takriban kipindi chote cha mwaka wa fedha 2014/2015. Aidha, ni jambo la faraja kuona kuwa hali ya upatikanaji wa chakula muhimu (mchele, sukari na unga wa ngano) iliendelea kuwa nzuri kwa kipindi kirefu sasa. Pamoja na hali hiyo, Kamati inaitaka Wizara kufanya utafiti juu hali iliyojitokeza hivi karibuni ya kuwepo kwa tofauti kubwa ya bei za bidhaa kati ya Unguja na Pemba kwa bidhaa za Pemba kuuzwa kwa bei ya juu zaidi kuliko kawaida.

Mhe. Naibu Spika, Tathmini ya bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2014/2015 inaonesha kuwa uingizwaji wa fedha kwa Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko kama ni msimamizi mkuu wa kuziendeleza Sekta za biashara na viwanda si wa kuridhisha sana kwani hadi kufikia mwezi wa Marchi, 2015 fedha zote zilizopatikana ni asilimia 65% tu ya makadirio.

Mhe. Naibu Spika, Katika ukusanyaji wa mapato Wizara hii iliidhinishiwa kukusanya mapato ya Tshs. 100 milioni kutoka katika vianzio vyake mbali mbali ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2015, Wizara ilikuwa imeshakusanya Tshs. 71.4 milioni.

**SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (*ZSTC*)**

Mhe. Naibu Spika, Katika msimu wa mwaka 2014/2015, Shirika la Taifa *ZSTC* lilijiwekea lengo la kununua karafuu kati ya tani 3,400 hadi 3,600 zenye thamani ya Tshs. 54 bilioni ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2015, jumla ya tani 2,800 zenye thamani ya Tshs. 39.3 bilioni zilinunuliwa kutoka kwa wakulima.

Mhe. Naibu Spika, Pamoja na mafanikio makubwa yaliyofikiwa na Shirika hili katika biashara ya karafuu na kuliendeleza zao lenyewe la karafuu, bado kuna changamoto kadhaa zinazoendelea kuikabili biashara hii ikiwemo magendo ya karafuu pamoja na kujitokeza kwa baadhi ya watu wnaopita majumbani wakidai kuwa wametumwa na Shirika la *ZSTC* kupita miataani kununua karafuu. Lakini changamoto kubwa zaidi ni ile ya uchafuzi wa karafuu.

Mhe. Naibu Spika, Taarifa zinaonesha kuwa kuna baadhi ya wakulima wanachanganya karafuu na makonyo au vitu visivyostahiki kuwemo katika karafuu, jambo ambalo linaweza kusababisha kuharibu sifa na ubora wa karafuu za Zanzibar. Uchanganyaji huo unaweza kuleta athari kubwa hasa kwa kuwa Serikali hivi sasa imo katika mipango kabambe ya kuilinda karafuu ya Zanzibar kwa kutumia Tasnia ya Malibunifu pamoja kuifanyia utambulisho maalum (*Branding*). Hivyo, Kamati inaitaka Wizara pamoja na Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*) kufanya juhudi za ziada za kutoa elimu kwa wakulima na kukemea tabia hii, kwani licha ya kupelekea kushusha hadhi na soko la Karafuu ya Zanzibar, lakini pia itachafua mipango mizuri iliyowekwa ya kuimarisha biashara ya karafuu hapa nchini.

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara hii ya Biashara Viwanda na Masoko inaomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi Bilioni Mia Sita, Mia Sita na Nane Milioni Laki Tatu (Tshs.6,608,300,000) ambapo katika mfumo mpya wa bajeti unaozingatia Programu (*PBB*), matumizi hayo yamepangwa kugharamia Programu nne (4) ambazo ni Utawala na Uendeshaji, Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali, Ukuzaji na Uendelezaji Biashara na Progaramu ya Viwango na Udhibiti wa Ubora ambapo ndani ya Programu hizo kuu nne kuna Programu ndogo tisa (9) kama zilivyofafanuliwa katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara hii iliyowasilishwa mbele ya Baraza lako Tukufu hivi punde.

**PROGRAMU NDOGO YA MAENDELEO YA WAJASIRIAMALI**

Mhe. Naibu Spika, Kama ilivyoelezwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Programu hii inakusudia pamoja na mambo mengine kutoa misaada ya kitaalamu kwa wajasiriamali wapya katika kuanzisha viwanda vya uzalishaji pamoja na kuelimisha wajasiriamali kuhusiana na mifumo ya fedha na misaada mengine ya

kibiashara ambapo jumla ya Shilingi Mia Saba na Ishirini Milioni, Laki Nne na Hamsini na Moja Elfu (Tshs. 720,451,000) zimetengwa kwa ajili ya programu hiyo ndogo. Hata hivyo, Kamati inawasiwasi juu ya utekelezaji bora wa shughuli mbali mbali zilizopangwa ndani ya programu hii kwani hadi sasa Kamati yangu haijafahamu mustakbali wa uanzishwaji wa kituo cha mafunzo ya wajasiriamali ambacho kilikuwa kikizungumzwa kwa muda mrefu sasa.

Mhe. Naibu Spika,  Kwa mnasaba huu Kamati inaitaka Wizara kutoa maelezo ya kina juu ya hatua zilizofikiwa katika uanzishaji wa kituo cha mafunzo ya wajasiriamali ambapo hapo awali jengo lilokuwa likitumiwa na JKU hapo Saateni ndilo lililokusudiwa kufanyiwa kituo hicho.

**PROGRAMU NDOGO YA VIWANGO NA UDHIBITI WA UBORA**

Mhe. Naibu Spika, Kama ilivyoelezwa kuwa Programu hii ina Programu ndogo moja ya Viwango na Udhibiti wa Ubora. Programu hii inatarajiwa kutoa huduma za kutayarisha na kukuza viwango pamoja kushajiisha matumizi ya viwango, ni wazi kuwa utekelezaji wa Programu hii utakuwa chini ya Taasisi ya Viwango, Zanzibar  (*ZBS*).

Mhe. Naibu Spika, Kwa hivi sasa Taasisi hii imetakiwa kufanya shughuli zake kwa kutumia maabara mbali mbali zilizopo zikiwemo za Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi na Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Hata hivyo, Kamati inaona si vyema kwa Taasisi hii kutumia maabara hizo kwa vile vigezo na viwango (*parameters*) vinavyotumika katika maabara hizo ni tofauti na vigezo vinavyotakiwa kutumika katika maabara ya viwango.

Maabara za Taasisisi hizo zinakidhi vigezo kwa mujibu wa mahitaji ya Taasisi zao lakini hazikidhi vigezo vinavyostahiki katika maabara ya viwango.  Maabara zinazopima viwango vya ubora wa bidhaa zina sifa na vigezo vyake vyenye viwango vya Kimataifa. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kujitahidi kadri iwezavyo ili kuifanya Taasisi hii kuwa na maabara zake yenyewe zenye viwango vinavyokidhi mahitaji halisi ya Taasisi. Aidha, kwa kuwa kazi za Taasisi hii ni kubwa na nyeti zinazohitaji wataalamu wa sayansi na viwango ambao ni wachache hapa nchini, Serikali inapaswa kuyazingatia upya maslahi ya wataalamu waliopo wa Taasisi hii.

Mhe. Naibu Spika, Taasisi hii ya Viwango pia ina changamoto ya kuchelewa kwa majibu ya sampuli inazopeleka katika Taasisi ya Viwango Tanzania (*TBS*) huko Tanzania Bara kutokana na foleni kubwa ya sampuli za Taasisi mbali mbali

zinazohitaji kupimiwa sampuli zao. Hivyo, Kamati inaiomba Wizara kuizingatia changamoto hii kwa uzito unaostahili kwani huzorotesha sana kazi za Taasisi hii kwa hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imejadili na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka wa fedha 2015/2016, na inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wako wote waijadili, watoe mapendekezo yao na hatimae kuipitisha Bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza viongozi na watendaji wa wizara hii, kwa juhudi wanazochukua katika kutekeleza kazi zao pamoja na ushirikiano wao kwa Kamati hii.

Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa makini na utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba yangu.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi).*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Mhe. Viwe Khamis kwa niaba ya Mwenyekiti. Waheshimiwa Wajumbe, nina wachangiaji wawili naomba mwenye nia ya kuchangia alete mapema ili tuweze kujipanga vizuri katika kutoa michango. Kwa hivyo, mchangiaji wa mwanzo Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, afuatie Mhe. Mohammedraza, kama yuko nje aingie ndani.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi kwa leo asubuhi kama kawaida yangu namba moja, ili kuweza kuchangia Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye ukurasa 6 katika biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara. Mhe. Naibu Spika, hapa nitoe masikitiko makubwa sana. Wafanyabiashara wetu wadogo wanaopeleka bidhaa Bara bado hatujawatendea haki. Kama tunavyojua kuna njia nyingi za kuondoa umaskini, lakini wananchi wengi wameona njia ya kuondoa umakini ni kufanya biashara za kutoa vitu hapa na kuvipeleka kule Bara, lakini bado kodi imekuwa ni kubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, kama friji wanalipishwa kodi kubwa, honda wanalipishwa kodi kubwa na baadhi ya vitu vyengine. Halafu wanapekuliwa sana, wanasumbuliwa sana. Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano muachie kidogo Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko atusikilize kwanza maoni yetu.

Mhe. Naibu Spika, lazima hili suala waziri aweze kulifuatilia na afike pahali ambapo anaweza kuwasaidia wananchi wetu, kwa sababu wanasikitika sana, na tunawapuuza kama tunavyowapuuza sasa hivi hapa, maana yake Mhe. Waziri yule pale naona haandiki. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, naomba sana tuwasaidie wananchi kwa kuwasimamia hizi biashara ndogo kwa kuondoa umaskini, kwa sababu tunapowasaidia hata Mwenyezi Mungu na yeye anatusaidia kutupa riziki nzuri. Lakini bado hatujawatendea haki kina mama, hasa utakuta biashara hizi wanafanya kina mama pamoja na kina baba kwa asilimia ndogo. Kwa hivyo, mimi naomba kwa kuwa hawa ni wazee wetu kina mama, hivyo tuwatafutie utaratibu ambao tuwafuatilishie ili waondokane na usumbufu.

Mhe. Naibu Spika, biashara ya *TRA* ni moja, lakini la kushangaza hata friji lile, wanapeleka kina mama, basi hata viguo, ilimradi tunaomba sana hilo uweze kusimamia ili haki itendeke.

Mhe. Naibu Spika, hii ni Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, niseme wizara tajiri. Kwa nini nikasema ni wizara tajiri, kwa sababu Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ndio inayotenda biashara. Kwanza niwashukuru sana, tuna wafanyabiashara kwa mfano Mhe. Raza, Mhe. Jaku na waheshimiwa wengine, tuna vijana wengi sana ambao wanafanya biashara ambazo zenye tija na hapa kutuletea kodi nzuri katika kisiwa chetu.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na hayo bado hatujafikia kiasi kinachostahiki na sababu kubwa sasa hivi wafanyabiashara wengi wa Zanzibar wanakimbia na kodi, kodi zimekuwa kubwa. *Wallahi* Mhe. Naibu Spika, kodi za Zanzibar zinachekesha sana. Kila sekta inatengeneza kodi yake kwa wafanyabiashara hawa, wanapungua siku hadi siku. Suala hili linasikitisha sana, tena linasikitisha sana.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa huu wa 12 kuhusu maendeleo ya viwanda, pamoja na kuandikwa hapa kuonesha jinsi gani maendeleo ya viwanda, lakini bado hatujawasaidia hawa wafanyabiashara wa viwanda, hususan biashara ya maji. Maji kama tunavyojua Zanzibar na sisi tunatoa maji ya *drop* ambayo ni mazuri sana, lakini sijui kwa nini Mhe. Waziri hoja nzito, mwachie kwanza mheshimiwa huyo. Hoja nzito hii ya maji.

Kwa nini Zanzibar haturuhusiwi kupeleka maji yetu kule Dar es Salaam, ni suala la kusikitisha sana. Tunawaona hapa *AZAM*, Kilimanjaro na mengine, lakini yetu kule hayaendi. Bora ulivyoondoka Mhe. Waziri nitapata kusikilizwa vizuri sasa. Mhe. Waziri kwa nini hebu tuangalie tatizo liko wapi, tumeshachoka na kunywa *AZAM* tu, na kule angalau yaende. Kwa hivyo, naomba sana hili suala hebu

tulisimamie, kwa kweli yana *standard*, sasa hivi maji yao ni mazuri. Tunaambiwa maji kule machungu ni machungu, hayana uchungu wowote, lakini ile kuwa soko la maji lisiende kule Dar es Salaam, kwa sababu likiingia kule watu wakiyazoea basi ujue soko letu litakuwa kubwa zaidi.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba hili suala lifuatilie kwa makini na ulisimamie kwa umahiri wako, tunaomba sana hili suala lifanyike. Inasikitisha sana kuona kuwa kila siku kukicha Zanzibar tunafungua vitu hivi, kila kona sasa hivi *Alhamdulillah*.

Kwa hivyo, mimi naomba sana, sababu uzitafute na uje unijibu kwa nini kule hatuwezi kupeleka na sisi maji yetu, kama si hivyo Mhe. Waziri yazuie na yale yasije huku, kwa sababu huku yanaharibu soko, yanaangusha soko kwa nguvu sana maji yetu. Ukiangalia sasa hivi wanakula hasara watengenezaji wa maji hapa Zanzibar. Kwa hivyo, ili na sisi tuendelee vizuri basi tupewe hatua tupunguziwe kodi. Maana yake nasikia kodi inakuwa kubwa ukipeleka maji kule, lakini huku inakuwa *free*, kwa nini iwe hivyo na hawa watu wanalipa makodi hapa makubwa, halafu leo tunawazuia katika kujinafasi. Hilo mimi sikubaliani nalo, naomba sana.

Mhe. Naibu Spika, hapa kuna Kiwanda cha Sukari. Kwa kweli nasikitika sana pamoja na kuwa hili sio lako, lakini wewe ni mja wa huruma.

Mhe. Naibu Spika, Kiwanda cha Sukari kimeji-*establish* vizuri sana na kinajiandaa vizuri sana, lakini watendaji wake hawatendewi haki. Kwa hivyo, naomba sana tuwahurumieni wale binadamu, kiwanda hakiwi kizuri kama hakina wafanyakazi, kiwanda hakiwi kizuri kama hukuwatengeneza wafanyakazi wakawa wazuri katika ulipaji wao. Wanafukuzwa kiholela, mtu anafanya kazi siku ya tatu, ya tano anafukuzwa.

Mhe. Waziri, hili sio lako, lakini lako kwa sababu ni kiwanda kile, haiwezekani kiwanda kiwe kitupu. Mhe. Waziri naomba sana kwa huruma hii na hasa mwezi mtukufu wa Ramadhan. Naomba sana mwezi huu wa toba, mwezi wa kutafuta Rehma, twende zetu Peponi, naomba sana tuwafikirie hawa wafanyakazi wa Kiwanda cha Sukari Mhe. Waziri, hebu tukae nao jamani, nishirikishe na mimi, usione tabu, tukae na tuzungumze nao, ili waweze kufikia pahala pazuri. Wanasikitika kila siku maskini ya Mungu, twende ukawaone. Sio mwanamke sio mwanamme, wanasikitika kiguu na njia kila siku wanafukuzwa na haki zao hawapati, mikataba hawafungishwi. Jamani tunakwenda wapi na sisi tutachoka kusema, lakini hatuchoki kwa sababu tumeitaka kazi.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri nakuomba sana sikukamii naomba radhi, siwi mkali naomba radhi sana, lakini nakujua wewe ni mtendaji nakuaminia Mhe. Waziri,

pepo ndio hii kaka yangu, wala usipate tabu, hii ndio pepo. Watu hawajui pepo iko vipi, pepo yenyewe unaanzia hapa, huko unakokwenda unafanyiwa hesabu *Alhamdulillah*, unakwenda kula matunda ya huko. Tuanzieni hapa duniani, tuwasaidie wanyonge. *Wallahi* Mhe. Naibu Spika, ukiwaona wanapokuja wanasikitika na kulia machozi. Kwa hivyo, naomba sana tuwahurumie watu wa kiwandani ili kuweza kuwafikisha pahali pazuri sana, naomba sana.

Mhe. Naibu Spika, mimi huwa ni mtafiti wa mambo mengi, katika ukurasa huu wa 19. Kwanza Mhe. Waziri nikushukuru sana kuhusu ulinzi wa zao la karafuu. Hapa nakupa *credit* katika asilimia kubwa.

Mhe. Naibu Spika, ulinzi umeimarika vizuri sana, binadamu kasoro ndogo ndogo zimo. Mara nyingi sana wanalalamika kutokana na yale mafao ya hapa na pale, sio sana, lakini *of course* wanalalamika. Hapa sitaki niseme sana kwa sababu wanaifanya kazi vizuri. Kwa hivyo, naomba sana waboreshe vizuri zaidi hawa watu ili na mara hii zao la karafuu waweze kutusimamia vizuri. Mheshimiwa kwa hapa umefanya kitu cha msingi sana na kinafurahisha, lakini tatizo lao wanashindwa kupata mafao yao kwa wakati mzuri. Kutokana na ile motisha uliyoandaa wakikamatwa basi tunaomba iendelee vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nije katika suala la mafuta. Juzi moja nilichangia nikasema acha makonyo tu hata na majani nayo yanatoa mafuta tena *quality*. Kwa hivyo, ningeomba tukajaribu kutafuta viwanda ambavyo ni vya *local,* ambavyo vinaweza vikawasaidia wananchi wetu, kama vile viwanda vinavyotengeneza mafuta ya mchaichai vilivyokuwa *local,* vile ambavyo sio *expensive* tukawasaidia wananchi.

Mhe. Naibu Spika, tujaribu sana katika njia moja ya kukuza uchumi, na katika njia moja ya kumuondolea mtu umaskini, hasa katika mashamba yetu. Mhe. Naibu Spika, ningeomba sana hivi viwanda vidogo vidogo hivi ambavyo vinaweza vikatengeneza vitu vikasaidia vikundi, hebu twende kwenye vikundi. Tutafute mashine hizo ndogo ili kuweza kuwasaidia wananchi wetu kuweza kutengeneza mafuta ya mchaichai, majani ya karafuu.

Mhe. Naibu Spika, majani ya karafuu tunayo mengi kama makonyo tulivyokuwa tunayo, na kila siku yanapuputika. Mhe. Naibu Spika, mafuta yake nikikuletea huwezi kuamini kama mafuta haya ni ya majani ya mkarafuu, hilo naomba sana uweze kuwasaidia wananchi ili uweze kuwafikisha katika uchumi mzuri.

Vile vile, Mhe. Naibu Spika, niipongeze sana serikali katika jitihada zake za kusaidia upandaji wa karafuu. Miche ya mkarafuu hapa nashukuru sana na jitihada tunaziona jinsi gani watu na ile motisha uliosema.

Mhe. Waziri, mimi nikupe ushauri mmoja. Kwa kuwa hivi sasa kama wakati wa kutoa miche tayari, basi ungeandaa *time frame* ambayo ingejiridhisha kwa kila maeneo ambayo tayari wanataka ile miche iwakute kwa wakati, hilo moja, lakini jengine timu ile iwe inazunguka na kuweza kuwapa watu taaluma ya jinsi gani ya upandaji wa mikarafuu inayoendana na wakati wa sasa. Kwa sababu wengine wanapanda tu hivi hivi hawajui zile taaluma, yeye madhali umeshampa mche yeye anafanyia ile kazi ambayo haistahiki. Hilo moja nimeona nikwambie.

Mhe. Naibu Spika, wenzetu huko nchi za nje na wao wanatafuta karafuu hasa za kwetu, wanaona labda wakienda kuotesha kule itakuwa kali kama ya kwetu, kumbe hawajui inategemea na ile ardhi yenyewe ilivyo.

Pili, Mhe. Naibu Spika, ni ulinzi. Ulinzi huu wa karafuu, maana yake ulinzi niliokusudia ni kutokana na tiba yenyewe. Mhe. Naibu Spika, ulinzi wa tiba. Unajua huko nyuma kulikuwa na kile kikundi nimekisahau kidogo. Walikuwa wanatibu mikarafuu. Kwa hivyo, naomba sana ile irudishwe haraka sana ili kuweza kuinusuru ile mikarafuu ambayo imepata maradhi. Kwa sababu tukiipata tiba hiyo na lile lengo lako la kutaka kuendesha vizuri biashara hii basi iende kwa wakati.

Mhe. Naibu Spika, kuna wazo jengine, katika utoaji wa vibali vyako, ningependa sana twende na wakati, japo kilipiwe kidogo lakini vibali vile vinavyotoka vya sukari ni karatasi hali halisi. Kwa hivyo, ningeomba sana Mhe. Waziri uka-*frame* vizuri sana, kama wenzako wanavyotoa vibali vinakuwa vizuri na *International* kabisa. Kwa hivyo, naomba sana hili suala uweze kubuni gamba ambalo litaweza kutisha kuliko hili, kwa sababu mtu ukimpa karatasi ataona aah! hivi mimi naleta biashara kubwa hapa na karatasi yenyewe hii ya mchele. Kwa kweli inakuwa haistahiki sana.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa hivi viwanda vidogo vidogo, maana yake naona kama kule Gulioni. Mhe. Naibu Spika, na wale nao tungejaribu kuwatafutia teknolojia ya kisasa kwa zile mashine ambazo zinaweza zikawasaidia bila ya kutumia umeme, kuokoa ili wasipate hasara zaidi.

Mhe. Naibu Spika, wale watu wanaokuwa pale wanaji-*organize* vizuri sana, tena niwapongeze wanafanya kazi kwa jitihada zote ni wabunifu. Sasa watu kama wale wizara yako inatakiwa lazima iwe nao karibu na iweze kuwasaidia ili kuondosha umaskini kwa nguvu sana, lakini ukitizama pale sasa hivi ukimuuliza atakwambia aah! wizara pengine hajafika au nyengine.

Jengine Mhe. Naibu Spika, kuna suala la sasa hivi la kufanya *juice*. Zamani nilisikia Mchina, hebu nataka uniambie hapa. Mchina alitoa viwanda vya kutengeneza *juice*. Kwa kuwa sisi matunda tunayo mengi, hili limefikiwa wapi na

kama limelala lifufue Mhe. Waziri. Matunda tunayo ya kila aina na hili moja linaondoa umaskini.

Mhe. Naibu Spika, mimi nimshukuru sana Mhe. Waziri na ninakupa asilimia 100, kwa ninavyokujua ninakuunga mkono. Nampongeza sana Katibu na Naibu wake, Naibu Waziri, watendaji wote, na Wakurugenzi niwape na wao hongera kubwa sana Ramadhan Kariim. Ahsante sana nimeunga mkono kwa asilimia mia.

**Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali:** Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutupa hizi pumzi, na tumshukuru sote sisi kwa kuweza kufika katika hali ya uzima.

Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii vile vile sote leo ni Mwezi Mosi Ramadhani, sawa na tarehe 18 Juni, 2015, ambapo mwezi huu ni mwezi ambao unafundisha mambo mengi sana.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, nichukue nafasi hii kumshukuru Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, kaka yangu Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, pamoja na Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Masoko na Viwanda, Katibu Mkuu na watendaji wake wote, pamoja na kamati iliyokuwa imefika mbele yako hapo akitangulia Mhe. Waziri kuteremsha haya Makadirio ya Fedha ya mwaka 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika, kwanza mimi nichukue nafasi hii kumuomba kwa dhati kabisa, namuheshimu sana na sote wafanyabiashara tunamuheshimu, kaka yangu Mhe. Nassor Ahmed Mazrui.

Mhe. Naibu Spika, ningeomba leo hapa kwa heshima zote ungenipa kidogo muda, kwa sababu hii ni fani yangu, na fani ambayo itawasaidia Wazanzibari na Waheshimiwa Wawakilishi kufahamu hali ya uchumi na hali tuliyokuwa nayo ya kibiashara, kwa sababu wengi watazungumza sera na siasa, lakini mimi kwa sababu ni mmoja kati ya wafanyabiashara na suala la uchumi, ninaamini hapa wenzangu Waheshimiwa Wawakilishi na Wazanzibari wataelewa hali halisi iliyotufika hapa tulipofika na hasa kwa bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, alipokuja Mhe. Waziri wa Fedha, aliisoma hotuba yake tarehe 13 Mei, 2015 ilikuwa ni siku ya Jumatano jioni saa 11:00 Mhe. Omar Yussuf Mzee. Alitusomea bajeti na akasema katika kipindi hiki uchumi wa Zanzibar umeumia, yaani umeathirika, ni kwa sababu ya fedha zilizochotwa *Escrow*, kwa hivyo, haya ni maneno ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Namshukuru sana leo kaja Mhe. Waziri wa Biashara fani yake ya kibiashara namuheshimu sana, kaja na neno hilo hilo kuteremka kwa sarafu na kuathirika kwa uchumi wetu.

Mimi ningelimuomba Mhe. Waziri wa Biashara kwa sababu ni fani yake, maana ningeliona labda Mhe. Omar Yussuf, ni sera lakini naye ni mfanyabiashara atapokuja *in shaa Allah* Mungu atampa pumzi, atampa nguvu, atampa mambo yote *in shaa Allah* akija hapa asitafune maneno aje atueleze, na mimi ninamsaidia kumpa *evidence*. Mhe. Naibu Spika, Serikali yetu sikivu sana na mimi namshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na watendaji wake wote kwa huruma zao kwa wananchi wa Zanzibar Unguja na Pemba.Niishukuru Wizara na Serikali yenyewe.
Mhe. Naibu Spika, Serikali yetu ina huruma, imesamehe na inaendelea kusamehe baadhi ya vyakula; mchele, unga wa ngano, tende na vyengine mpaka hivi sasa lakini nataka litoke tamko la ziada ili Mhe. Waziri wa Biashara atwambie kwamba vitu hivi viendelee na aombe Serikali vile vile suala la sukari na mambo mengine vile vile kufikiria hali halisi ya kuweza kusamehe.

Mhe. Naibu Spika, wafanyabiashara mimi siku zote nilikuwa nikisema hapa pamoja na Waziri wa Biashara Mhe. Nassor Mazrui, nilisema kwamba kweli serikali haikupandisha kodi, na kweli serikali yetu ambayo inaongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein imekuwa na usikivu mkubwa katika kuwaonea huruma wananchi, hilo halina mjadala.

Napenda kukiri zaidi kwamba Serikali kodi ya vifaa vyote havikuwa vimepanda, sasa Mhe. Naibu Spika, katika mazingira tuliyokuwa nayo, na hili nawaomba Wawakilishi wenzangu, wazee wangu, kaka zangu, tuwe makini sana. Hali ya biashara kwa kuteremka kwa sarafu haijapata kutokea toka Mapinduzi yetu matukufu ya Mwaka 1964 ya Zanzibar na uchumi huu ambao umeanguka, na sarafu zetu hizi leo dola imezidi kuwa dola zaidi ya shilingi 2000, dirham karibu 500 haikuja kwa kubahatisha wala haikuhusishwa na Serikali zetu, ni watu wachache ambao nashukuru hakuna Mzanzibari humu.

Nashukuru kwamba watu hawa walichota pesa katika *account* ya *ESCROW*. Serikali ilikuwa na pesa zake za walipa kodi matokeo yake pesa zilichotwa wahisani wamezuia msaada kwa Tanzania nzima, ina maana mpaka kwa Zanzibar. Ni kikundi kidogo cha watu waliochukua *over three hundred billions*.

Sasa Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri kama *we have  a problem, we have to find the solution, and what's  is next?*

Nataka Mheshimiwa Waziri akija asiseme tu kwamba sarafu imeshuka, lazima Wazanzibari tuelewe kwamba watu hawa wenye asili ya Bara wameifanya Zanzibar nzima ikumbwe na umasikini, kwa sababu wenzetu Bara kama zile pesa zimechotwa hawakuathirika Mwenyezi Mungu awajaalie, kwa sababu hawa wana dhahabu, wana almasi, wana kahawa, wana kila kitu, sisi uchumi wetu kwa Zanzibar ni biashara, sasa *donors*, nchi za Scandinavian, nchi za Marekani wameweka *sanctions* ikiwemo na Zanzibar imezuiliwa misaada kwa sababu tunasema Tanzania. Mazingira haya kutokana na Benki Kuu hawana pesa, soko za kuzipeleka mitaani dhahabu imeshuka bei, soko la wafanyabiashara mahitaji ya dola yamekuwa makubwa Mhe. Naibu Spika, matokeo yake soko limekuwa dogo, fedha za dola hizi kwa miaka zaidi ya hamsini imepanda, sasa ninachotaka kuiambia Serikali sisi wafanyabiashara tutajitahidi mno kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu hasa kwa mwezi huu wa Ramadhani kuwaonea huruma wananchi wetu tutajitahidi.

Vile vile, kutokana na dola ilivyopanda Mhe. Naibu Spika, nataka nikwambie kwa mara ya kwanza wafanya biashara wa Zanzibar kuanzia mkulima mpaka wafanyabiashara wakubwa wameathirika, na haijapata  kutokea wafanyabiashara kuathirika Zanzibar.

Sasa Mhe. Naibu Spika, hichi ni kipindi cha lala salama, na tuko katika Mwezi mtukufu wa Ramadhani, sote tuna udhu kwa Mwenyezi Mungu, lakini kwa bahati Mhe. Spika, hawa waliochota pesa katika suala lile la Zanzibar kwa mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Mimi nashangaa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kushindwa kutoa kauli au kushindwa kusimama kusema nini tunachotaka, sasa sababu Mhe. Naibu Spika, fedha hizi zimechukuliwa kama nilivyosema sirejei na watu wachache, na kwa bahati wanaendelea kuingia bungeni mimi nashukuru, na *wallahi* Mhe. Naibu Spika  ingelikuwa humu pasingelikuwa CCM wala *CUF* humu ndani *wallahi* asingelitoka humu ndani, tungelimtia mikwaju hasa humu ndani. Haiwezekani sisi leo tumekaa hapa tunawakilisha wananchi, wananchi wanaendelea kuwa masikini wanazidi kuwa masikini wale watu wanakula mara nne, na sisi sote tunaweza kufutari, leo Wazanzibari wamekaa wanakunywa uji asubuhi hawana futari ya

mchana, hawana futari ya usiku halafu sisi tumebakia kusema. Hawa wenzetu wameendelea kutembea na magari makubwa.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka kuwaambia watendaji wangu pamoja na Mhe. Nassor, sote wamezipanga Prado pale ndio ilivyo, lakini lazima tumkumbuke Mungu, tunaringa na pumzi za Mungu, haiwezekani.

Mimi nafikiri Wawakilishi kwa neno la Mwenyezi Mungu neno la wazi tungelimuomba Mhe. Saleh Nassor, mimi niko tayari kuchukua ndege moja tukaonesha kilio chetu kwa wahisani, Marekani, Uingereza na Denmark tukasema jamani tumeathirika sisi, sisi tunawawakilisha wananchi, waliochota pesa ni hawa watano, Zanzibar imewekewa vikwazo, tufanyeni mara moja tuchukueni ndege hapa, hatufanyi maandamano.

Mhe. Naibu Spika, tunakwenda kwa niaba ya wananchi. Mimi nimekuja kwa niaba ya wananchi, hichi kiti na keshokutwa nakirejesha kwa wahusika, narejesha kwa wahusika ofisi kuu ya CCM pale, *they are not the losers, we are the losers,* haiwezekani watu wakae tu, Benki Kuu imekaa tu kwa sababu wana magari ya kutosha, wana mabilioni, majumba yao moja kila mtu ana milioni thalathini, arubaini nyumbani yake, mshahara wake unafika milioni tano pesa zinashuka thamani.

Mhe. Naibu Spika, halafu *people from grassroots* wamekuwa *infected*, tuendapo padogo, tumezaliwa na mchanga tutazikwa na mchanga, hatuwezi kukaa humu ndani leo wenzetu wanatafuta futari Ramadhani imeangukia leo mtu haijui hata mtu ataendelea kula mchele, ataendelea kufuturu kwa mchele bei vitapanda hivi Mheshimiwa.

Sasa mimi ninachotaka kusema nimwambie Mhe. Waziri wa Biashara kama kuna uwezekano tujikusanye wafanyabiashara kidogo pamoja na wananchi twendeni kwenye ubalozi wa Marekani Dar es Salaam, kwa heshima na taadhima tukawaambie bwana tumezuiliwa msaada.

Katika kipindi cha awamu iliyopita ya Dkt. Salmin Zanzibar tulipowekewa vikwazo wenzetu Bara wakafurahikia vikwazo vile, mimi nina ushahidi, na Mheshimiwa Naibu Spika, ukinambia nitoe ushahidi nitatoa ushahidi tuliwekewa vikwazo, Bara tulipowaendea jamani tumekuja tusaidieni Waziri wa Fedha wa Tanzania Bara chini ya Serikali ya Rais Mkapa tena kwa maandishi tena

tuliwekewa vikwazo mpaka chanjo za watoto wasiokuwa na hatia mbele ya Mungu malaika wakawekewa vikwazo.

Tukienda ndugu zetu Bara wakasema tumeambiwa na nchi za Marekani, nchi za ulaya, nchi za Scandinavia kwamba Zanzibar tusikupeni msaada hivi hivi tuko kwenye Muungano nchi mbili huru zimeungana.

Mhe. Naibu Spika, tukaambiwa hivyo ushahidi upo, nyaraka zipo, sasa mimi nashangaa watu wameiba pesa, wamechota pesa halafu na sisi tumekaa kimya Zanzibar tuna majukumu kwa Mwenyezi Mungu tusikae tukawa tumevaa koti, aliyevaa kaunda maana yake humu huruhusiwi kuvaa shati, halafu tukayapanga magari yetu pale yana thamani zaidi ya milioni mia *and then* ukasema aa basi.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninachotaka kuja kumuomba Mheshimiwa Waziri wa Biashara haya niliyoyasema akiri mbele ya Mwenyezi Mungu, ndio namuheshimu sana na nafikiri yeye ndio atakuwa shahidi kwa Mwenyezi Mungu, kwa sababu ni mfanyabiashara, tutaendelea kumuheshimu Mhe. Nassor na tunaendelea kumuheshimu.

Lakini lazima tujue tunachokifanya juzi hapa tuna mafuta yetu Fungu Mbaraka tunaambiwa si letu tena, sasa wenzetu wana dhahabu, wana shaba, wana gesi, wana kila kitu; wana kahawa ule haumo ndani ya Muungano.

Leo tuna mafuta ambayo hata Tanganyika haikuzaliwa, Fungu Mbaraka wanatwambia imo ndani ya Muungano, mimi simlaumu Dkt. Shein yeye kayakuta kayarithi, lakini *we are responsible* Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kayakuta, lakini tuna dhamana.

Leo wanaingia pale Fungu Mbaraka kesho watakwenda visiwa vya Pemba pale, mafuta nawaambia wenzangu tu, kesho watasema karafuu zetu vile vile, sasa Mhe. Naibu Spika, tunazungumza maslahi ya wananchi kwa kuwatetea wanyonge, tulifanya Mapinduzi ya Zanzibar ili tujinasue katika uchumi wetu tuwe na uhuru, ndio maana Mapinduzi haya tumekusanyika humu leo ndani kila rangi ya kabila, bila ya kujali rangi na dini ndio Mapinduzi yetu matukufu ya Zanzibar kuwaletea wananchi neema, kuwaletea wananchi maendeleo; maji, barabara, umeme na serikali yetu imefahamu lakini haiwezi kuchezewa.

Mhe. Naibu Spika, tutakapozungumza nyote Waheshimiwa Wawakilishi ukweli ni kwamba viongozi Wabunge eti wamejiuzulu Ujumbe Kamati Kuu au Ujumbe wa Halmashauri Kuu.

Leo anatembea na mabilioni anapanda ndege, hatuwezi, lazima dunia tuiambie, Rais Kikwete msikivu na dola zinaendelea, hivyo vitu vitapanda tutajitahidi mwezi wa Ramadhani.

Mimi nawaomba wafanyabiashara wenzangu na mimi Raza nikiwemo, tuwaonee huruma wananchi kwa sababu *they are innocent,* lakini akija Mhe. Jaku na Mhe. Saleh kama ana jambo nitamwambia nunua milioni tano hizi lakini akija mkulima wake naweza nikampa bure, kwa sababu namwambia wewe ulikuwemo ndani ulinyamaza kimya.

Kwa hivyo, mimi naomba na hii Serikali bado iendelee kuona namna gani ya kuweza kuondosha msamaha kwa vifaa.

Mhe. Naibu Spika, Serikali lazima iwe *serious* katika kuwasaidia wafanyabiashara wadogo wadogo wa mazao ya matunda, uvuvi, na mazao mengine ambayo yanasaidia Wizara moja. Haiwezi kufanya kazi peke yake, inataka Wizara ya Kilimo, Wizara ya Biashara, Wizara ya Fedha, Wizara ya Miundombinu maana yake kuwawekea.

Mhe. Naibu Spika, sasa matunda yetu bado wafanyabiashara wataendelea kuwa masikini, kwa sababu kubwa ni soko, na kama ni soko kunahitajika mipangilio mingi, kama Zanzibar tutajipanga na tutakuwa tunaelekea kwenye *swiratul mustaqiim.*

Mhe. Naibu Spika, nchi hii inaweza kuwa pepo, lakini kama tutakuwa tunazungumza, unazungumza na mwenzako nyuma ana jambia, *we can't reach anywhere,* hatuwezi kufika!

Kwa hivyo, ningeomba Waziri wa Biashara kuna watu wetu wengi bado hali zao masikini kutokana na soko, leo yamejaaa maembe, yamejaa tele mananasi, yamejaa mambo mengi kuna ma-*investors*, lazima tuwe *serious* kukusanya nguvu zetu, anakuja *investor* anataka kuanzisha jambo kunakuwa na vikwazo ambavyo havisaidii kuna vikwazo vya ule umimi umimi, hatuwezi kufika Mhe. Spika.

Kwa hivyo, katika vitu vyote hivi vya biashara na vitu vyote hivi vya wakulima lazima tujipange tuwasaidie, kuna zao la karafuu tujipange namna gani ya kuweza kuwasaidia walimishwe halafu tuwape somo la kutunza hizi biashara.

Mhe. Naibu Spika, kwani mimi, Jaku na Mhe. Nassor Mazrui, tulikuwa kule kule kwenye *grassroots* mimi nimefika hapa kwa nguvu za Mwenyezi Mungu na wananchi bila ya wananchi, mimi nisingelifika hapa *Alhamdulillahi* sasa kama tumefika hapa kwa nguvu za wananchi wa Zanzibar, kwa Serikali ya Mapinduzi yetu lazima tufike pahala, na sisi tuteremke huko kwenye *grassroots*, tuone jinsi gani wakulima tunaweza kuwasaidia katika hali duni ya maisha, huwezi kuondosha ukasema kupunguza umasikini au ukawa na *vision* 2020 bila ya kuwa na nia, kwa hivyo lazima kuwepo na mpangilio na hali ya fedha.

Mhe. Naibu Spika, haya yote tunayoyazungumza ni hali ya uchumi na bajeti yetu. Bajeti zote zimezungumza pesa hazitoshelezi wenzetu wanapanga ndio maana mimi juzi nikasema hapa Mhe. Naibu Spika, nilisema kipindi kilichopita jamani hizi bajeti tunazokuja nazo kila mwaka bajeti nyingi sana siilaumu, kwa sababu Serikali ndio inayopata imepewa utekelezaji wake asilimia thalathini, arubaini, kwa nini kama hatufiki hapa tusirejee na bajeti ile ile ya mwaka jana, ili tukapanga mpangilio maalum na matumizi Mheshimiwa mengine yanakuwa ni matumizi ambayo yanakuja.

Na kwa bahati Serikali yetu Mhe. Naibu Spika, vitu vyote inanunua kwa *cash* vyote inanunua kwa pesa, *cash*, hakuna Serikali ya Zanzibar inayonunua vitu kwa mkopo, jambo hilo hakuna.

Meli ile tumenunua kwa *cash*, vifaa vya umeme na vyengine tunanunua kwa *cash*. Sasa katika mazingira yote haya kama ufumbuzi wa kuweka Zanzibar vipi tunaweza kuondokana na matatizo haya yanayotokea.

Mhe. Naibu Spika, hili tatizo la *ESCROW* si la kwanza, *EPA* vile vile Tanzania ililetewa vikwazo Zanzibar ikaathirika nishati vile vile.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninachosema hili sio suala la Muungano. Lakini nasikitika kweli hawa Wabunge wetu wa Zanzibar waliopo Dodoma wamekaa kimya. Sio kila anayepepesuka ni mlevi, lakini kuna Wabunge wetu kule, mimi ningeona kwa hili wangelitoka Bungeni kuonesha heshima ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, mimi nafahamu bora tule sembe kuliko mtu kuja kutwamulia mambo yetu wenyewe, bora tule muhogo. Lakini leo ndugu zetu Wabunge wamekaa pale wanaona hali halisi lakini hakuna Mheshimiwa hata mmoja akasema jambo hili. Sasa na sisi wakati mwengine tunakuwa na muhali.

Mimi naamini kama nilivyosema kwa Waheshimiwa hawa, angelikuwa huyo mmoja yumo ndani tusingelimpa kukaa humu ndani, tungelianza kutoa maandamano jimbo lake, awe CCM awe UKAWA, *Wallahi* pasingelitosha hapa Zanzibar, kuanzia Micheweni mpaka Makunduchi, mpaka Nungwi.

Mhe. Naibu Spika, sasa mimi nimalizie athari ya dola tunaanza kuiona. Leo nimekwenda *Exim Bank* nilikwenda ku- *draw* pesa zangu dola elfu 40, nilikwenda jana, wakanambia Benki haina pesa. Nimekwenda asubuhi leo wanasema pesa hazijafika kutoka Bara, kwa sababu kuna jahazi upepo umekuwa mzito, kwa hiyo jahazi imechelewa.

Mhe. Naibu Spika, sasa usalama wetu na hali hii uko wapi. Nitampa Mhe. Nassor hii *cheque* yangu aitizame ai-*quote* halafu anirejeshee. Lazima inatupa *worry now* sio, ikiwa mtu anataka kusafiri, nataka kutoa zaka, nataka kutoa pesa zetu leo fedha hakuna. Iwe kila kitu kije na jahazi yenye upepo inayovuta. Sasa katika vitu kama hivi, na kwa bahati bajeti itawasaidia sana Wawakilishi.

Bajeti hii ndiyo itakayokuwa muongozo kwa Mhe. Waziri kwamba haya ninayoyazungumza yote ninayo ushahidi, sijanusa tumbaku. Nina hakika kaka yangu Mhe. Waziri atakuja kusimama mbele ya Mungu atueleze haya niliyokuwa nimeyasema.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi hapa kilichokuwepo ni watu wamechota pesa, Zanzibar imeathirika kiuchumi, huu ndio ukweli. Kwa hivyo, sarafu zimepanda, bidhaa imepanda humu ndani, tutaionea huruma bure serikali yetu. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Maana yake humu ndani sote ni wamoja, sote humu tumekaa kwa udugu, hakuna upinzani humu ndani. Tuna Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Nassor Mazrui (Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko) kaja pale na kitabu cha Ilani ya Chama cha Mapinduzi, si ndio tumewekeana utaratibu kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Kwa hivyo, mimi nafikiri Waheshimiwa Wawakilishi tunafanyaje kuiambia sasa dunia. Je, leo mkutano unakwisha saa 8:00 nitayarishe ndege twendezetuni kwenye Ubalozi wa Marekani kwa uzuri kabisa.

Mimi nipo tayari kugharamia, hatugombani tunakwenda kwa niaba ya wananchi, hatwendi kwa siasa; *We are not taking politics here.* Tunazungumzia Zanzibar kuathirika kwa watu wachache, hatuzungumzi tu. Kwa sababu u-*CUF* na CCM haumo humu ndani, humu kuna Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Naibu Spika, kama kuna uwezekano leo Ramadhani saa 8:00 kama itawezekana saa 9:00 niweke ndege japo watu wachache tukatoe, ili dunia ijue kama tumeathirika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Bajeti ya Wizara ya Fedha ilitamka na leo Mhe. Nassor Mazrui, na yeye kaja katamka, kwa bahati yeye ni mchumi anafahamu. Sasa tutafute njia ya kuweza kuwa-*subsidize* "mkuki kwa nguruwe kwa binadamu mchungu, hujafa hujaumbika!

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa kumalizia kusema kwamba nimefarijika na Wizara zote hizi zilizokuja. Tumekuwa tunakosoana, tunapendana hakuna bajeti isiyokuwa na kasoro, binadamu tunazungumza.

Mimi imani yangu Wawakilishi ili tumalize mapema mwezi huu wa Ramadhani tuwe na maswali machache ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, tupitishe bajeti yake hata sasa hivi saa 8:00 imalizike twende tukafanye mambo yetu Dar-es-Salam.

Mimi naunga mkono kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Uzini, kwa niaba yangu naiunga mkono Wizara nzima kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu hawa watendaji wetu vile vile, ningeliomba Mhe. Waziri wajaribu kutizama kama kuna mafao yao, hawa wafanyakazi wa chini.

Mhe. Nassor Mazrui (Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko) kwa sababu nakuweza ndio maana nakwambia hivyo, nakuweza nakuheshimu na nitaendelea kukuheshimu. Tutatofautiana kisiasa tu humu ndani, lakini mimi nitakuja kwako wewe utakuja kwangu, ndivyo tulivyo. Tutakosoana humu ndani kwenye kazi zetu, tutakosoana kwenye sera katika kujenga umoja wetu.

Mhe. Naibu Spika, ninachotaka kukwambia Mhe. Nassor Mazrui, tafadhali kama una pesa za hakiba ambazo unataka kwenda kupongezana hivi, maana siku hizi kuna watu wana madeni madogo madogo kwa wakulima huko masikini za Mungu, wanaona kuna milioni sita basi wanaona wacha tukapongezane, bajeti imepita *Alhamdulillah*.

Bajeti imepita lakini kuna masikini za Mungu wanakudai, kuna mtu anadai laki moja, kuna mwengine anadai elfu hamsini posho yake, unakwenda kutumia milioni sita, eti tunapongezena bajeti imepita. Huku umewaachia deni walala hoi, masikini za Mungu uwezo wao mdogo.

Kwa hivyo, Mhe. Nassor Mazrui, nakuomba usije ukafika kwenye futari ukaona una milioni kumi ukasema sasa Wizara ya Biashara *Ahamdulillah*, twendeni tukapongezane tupike futari. Pesa zile bora walipe wale watu waliokuwa wa chini walikuwa wana mahitaji ya elfu 50, laki moja kama wanadai, kama hakuna wale wafanyakazi waliokuwa hawana deni tena una haki ya kujipongeza, lakini kama una *mas-ul* kwa Mungu, mwezi Mtukufu wa Ramadhani basi bora ukawalipe wale wafanyakazi waliokuwa hawajalipwa pesa zao.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa heshima na nawashukuru Wawakilishi kwa kunipa heshima hii maalum, kama ni Wizara ya Biashara kama ni Mfanyabiashara, nakutakieni kila la kheri, Mhe. Waziri na Serikali kwa ujumla *Alhamdulillahi Rabil-Aalamin.*

Mungu aibariki Zanzibar, Mungu aibariki Ramadhani kwa wananchi wetu wa Unguja na Pemba na duniani kwa ujumla. Tukae katika hali ya kupendana, kusaidiana na kushikamana. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Mhe. Mohammedraza Hassanali tunakushukuru kwa kumalizia kwa dua. Sasa nafasi tunampa Mhe. Mohammed Mbwana Hamad, baadaye Mhe. Mussa Ali Hassan. Mwenye nia ya kuchangia alete jina.

**Mhe. Mohammed Mbwana Hamad:** *Bismillahi Rahmani Rahim*. Mhe. Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia asubuhi hii ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kuwepo katika Baraza kwa ajili ya kuzungumzia mambo yetu mbali mbali kwa ajili ya manufaa na maslahi ya wananchi wetu.

Pili, nichukue nafasi ya kukupongeza kwa kunipa nafasi hii angalau na mimi kuchangia machache katika Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Aidha, nimpongeze Waziri kwa uwasilishaji wake lakini niipongeze na timu yake yote ya watendaji wake kwa maelezo ya mwenendo wa Wizara yao katika masuala mazima ya biashara.

Vile vile, nimpongeze Mhe. Viwe Khamis Abdalla, kwa niaba ya Mwenyekiti, kwa uwasilishaji wake mzuri.

Mhe. Naibu Spika, niende na mchango wangu pale alipozungumza Mwenyekiti, kuhusiana na suala la kupanda bidhaa Kisiwani Pemba siku hadi siku.

Suala hili kwa kweli linawadhalilisha sana kimapato wananchi wanaoishi Kisiwa cha Pemba. Hili ni tatizo la muda mrefu, bidhaa zinakuwa tofauti kabisa baina ya Pemba na Unguja. Najua kuna vikwazo vingi ambavyo vinasababisha bidhaa pale Pemba kuwa na bei zaidi kuliko hapa Unguja. Lakini ningemuomba Mhe. Waziri, kutokana na matatizo yanayosababisha kupanda kwa bidhaa pale, basi angalau ndani ya huu Mwezi Mtukufu wa Ramadhani atoe ofa maalum kwa ajili ya upunguzaji wa vyakula kama vile mchele, sukari na unga, kwa kuwa wananchi pale hivi ndivyo vyakula ambavyo kwa kipindi hichi wananunua kwa bei ambazo ni kubwa.

Jengine niiombe serikali kwa ujumla wake kwamba tatizo la ongezeko la bidhaa za vyakula Pemba linahitaji lifanyiwe ufumbuzi sio wa muda mrefu. Kwani wananchi hawa wanapata tabu sana. Hii inatokana na ukosefu wa bandari kisiwani Pemba.

Pamoja na kwamba Wizara ya Miundombinu imepita na bajeti yake jana, lakini hata hivyo serikali ipo na haya ambayo tunayoyazungumza nafikiri wanatusikia. Kwa hivyo tunaomba kwamba suala hili lifanyiwe marekebisho ili wananchi wanaokaa Pemba wajisikie kwamba wananunua bidhaa hizi kwa ufanisi, sambamba na wenzao waliopo Unguja.

Kuteremsha bidhaa Unguja halafu zikapakiwa tena zikapelekwa Pemba. Hili ni suala zima ambalo linapandisha bidhaa hizi kwa kiwango kikubwa. Namuomba Mhe. Waziri ashirikiane na Wizara husika pamoja na serikali ili wananchi hawa wapungukiwe na gharama kubwa ya vyakula, kisiwa ambacho kimekuwa na hali ngumu ya uchumi kutokana ukosefu wa bandari na mengineyo.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika ukurasa wa 5 hali ya biashara Zanzibar. Hapa nataka nizungumzie tu, katikati ya kifungu cha 13 kinasema kwamba:

> "Usafirishaji huo umechangiwa kwa kiasi kikubwa na mazao ya mwani na karafuu ambayo usafirishaji wake umefikia TZS 103,979.2 milioni ..."

Mhe. Naibu Spika, zao la mwani ndilo ambalo nimekusudia kulizungumza hapa. Zao hili la mwani ni zao ambalo kwa kiasi kikubwa sana limewakomboa wananchi wengi ambao wanajishughulisha na zao hili hapa Zanzibar. Lakini inaonekana kwamba bado zao hili halijapata bei ambayo inalingana na kazi ngumu wanayoifanya wakulima wa mwani.

Mhe. Naibu Spika, ukulima ambao tunaona kwamba wengi katika wakulima wa mwani ni wanawake wanapata tabu kubwa katika ukulima huu, lakini kwa kweli bei yao bado haijalingana na kazi ambayo inafanyika.

Pamoja na kazi ngumu wanayoifanya lakini inaonekana kwamba zao hili ni miongoni mwa zao muhimu ambalo linaingiza mafao hapa Kisiwani petu Zanzibar.

Nimuombe Mheshimiwa mbio zake zote na mbinu zake zote hawa wanunuzi wa zao hili basi umefika wakati wa kuliboresha angalau wakulima na wao wakajisikia kwamba wanafanya kazi ngumu, lakini angalau malipo yao yanakuwa na muelekeo wenye kufaa.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika ukurasa wa 6 biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara. Hapa nataka tu kiufupi sana nielezwe ni bidhaa gani za Zanzibar ambazo zinapelekwa Tanzania Bara.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika ukurasa wa 9 mwenendo wa bei ya karafuu na mwani.

Mwani nimeshaeleza wakulima kuongezewa bei, lakini niende katika zao la karafuu. Zao la karafuu ni miongoni mwa zao kubwa sana hapa Zanzibar, ambalo limeifanya Zanzibar kuwa maarufu sana katika uchumi wake. Pamoja na ongezeko la bei ambalo tunaendelea nalo hivi sasa, lakini kutokana na kuanguka kwa dola basi namuomba Mhe. Waziri aangalie na kupandisha bei ya karafuu ili iende sambamba na bei iliyopo hivi sasa. Kuanguka kwa dola kumeangusha shilingi ya Tanzania, kwa hivyo kuanguka kwa shilingi ya Tanzania, ipo haja ya zao hili kuliangalia upya, kulifanyia bei mpya ili iendane na wakati.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika ukurasa wa 19 kifungu cha 48, ulinzi wa zao la Karafuu hapa naomba kununukuu;

> "Mhe. Spika, katika kuendelea na ulinzi wa zao la karafuu, Wizara imeratibu shughuli za Kikosi Kazi maalum kilichoanzishwa kwa ajili ya ulinzi dhidi ya magendo ya zao la karafuu. Mikakati hiyo ilikuwa ni pamoja na kuweka kambi za ulinzi (*detach*) katika maeneo yenye uwezekano mkubwa wa kutoroshea karafuu, kuweka vizuizi barabarani (*Roadblocks*), na kuendesha doria."

Mhe. Naibu Spika, kuzilinda karafuu zisipelekwe magendo ni jambo zuri na ni jambo zuri sana, lakini kwa kuwa wapelekaji wa magendo ya karafuu tujiulize kule wanakopeleka wanatafuta nini. Wanachotafuta ni bei. Kwa hivyo, ina maana

kwamba ulinzi wa karafuu pamoja na kuwekewa vizuizi, pamoja na kuwekewa doria, pamoja na kuweka kambi za kuzuia magendo hayo ya karafuu.

Usafirishaji wa karafuu kwa magendo nahisi njia pekee ambayo inaweza kulizuia zao hili lisipelekwe popote kimagendo ni ongezeko la bei, kwa sababu ikiwa karafuu zinapelekwa nchi yoyote kwa magendo, ikiwa serikali itajipanga upya kununua karafuu bei zaidi ya iliyopo, hakuna mkulima wala mfanyabiashara ambaye atachukua karafuu kuzipeleka nje kwa magendo. Kwa hivyo, niiombe sana Wizara iliangalie upya suala hili, na iangalie ile gharama ambayo wanaitumia kwa ajili ya kuweka vizuizi na kuweka *task force* ya kuzuia karafuu na kulipandisha bei zao hili la karafuu.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika ukurasa wa 40 kiwanda cha mafuta ya makonyo. Kiwanda hichi ni muhimu sana, ni kiwanda ambacho kilianzia na mafuta ya makonyo lakini baadaye kimeanzisha ubunifu mwengine, kuna mambo mbali mbali ambayo pale yanakamuliwa na yanapatikana mafuta kama vile ya mchaichai, mkaratusi na mengineyo. Lakini kwa sababu asili ya kiwanda ni ndio jina lake ni kiwanda cha mafuta ya makonyo.

Nimuombe Mhe. Waziri, kiwanda hichi cha makonyo kama ambavyo kimeimarishwa vizuri lakini na haya makonyo yaangaliwe upya kibei kwa sababu makonyo ni bidhaa ambayo inazalisha kwa wingi pale kiwandani lakini makonyo inaonekana kwamba mafao yake kwa wakulima ni madogo sana. Kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Waziri makonyo ayapandishe bei, ili kuhakikisha kwamba makonyo watu walio wengi katika wakulima hawayadharau na wasiyapeleke kiwandani kwa sababu ya ulazima wa kwamba hatuna vya kuyafanya, kwa hivyo bei ya makonyo ni muhimu ili yapelekwe pale kwa kasi sana na yapelekwe pale kwa vizuri sana.

Mwisho Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika duka la vioo pale Darajani. Tumeona katika gazeti la Zanzibar Leo la tarehe 17 Machi, kuna tangazo pale linalohusiana na mualiko wa zabuni, nimuulize Mhe. Waziri zabuni zile zimeshafunguliwa na kama hazijafunguliwa ni lini Serikali itazifungua zabuni zile ili kuendelea na majengo yale yanayotarajiwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa mchango huu mfupi na mimi niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**Mhe. Mussa Ali Hassan:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kuweza kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Biashara.

Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kutufikisha hapa tukiwa salama wa afya tukaweza kuendelea na shughuli zetu za kazi ambazo tulipangiwa kuziendeleza hivi leo. Zaidi ya yote nimshukuru Mhe. Waziri kwa kitabu chake kizuri cha bajeti hii ya biashara ambacho ametufikishia hapa akiwa yeye pamoja na watendaji wake wa wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naanza kuchangia ukurasa namba 5 kuhusu shughuli zetu za biashara. Kwa mwaka uliopita tulifanya biashara nzuri sana ya kupeleka nje biashara za Zanzibar hasa kwa nchi za India na Norway kwa kuhakikisha kwamba tumepeleka vifaa vingi kama karafuu pamoja na mwani. Kwa kweli tuliuza mwani mwingi Singapore pamoja na India.

Kwa kweli muda mrefu sana tulikuwa na tatizo la bei kwa ajili ya wananchi wetu hasa bei ya karafuu. Ninaishukuru Serikali ilifanya kila bidii pamoja na wizara hii ili kutafutia masoko kuweza kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata bei nzuri, ili waweze kujikimu katika maisha hasa kwa upande wa karafuu. Tulitoka katika bei ya shilingi elfu tano kwa kilo hadi tukafikia bei ya shilingi 14,000 kwa kilo, hivyo naipongeza sana Serikali pamoja na wizara hii kwa juhudi waliyofanya nzuri kwa ajili ya kusaidia nchi yetu pamoja na wananchi wetu.

Hii ni neema nzuri ambayo imewafikia wananchi wetu kijikimu katika maisha na kuhakikisha kwamba biashara hii ya karafuu imepanda vizuri sana, hadi leo wananchi wetu wengi wao wameweza kutajirika kwa zao la karafuu. Waliokuwa hawana usafiri wamepata usafiri, waliokuwa hawana nyumba wameweza kujitegemea kuweza kupata nyumba za kuishi, hiyo naipa sana hongera Serikali pamoja na Wizara ya Biashara kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanalingana sawa na mwananchi mwengine yeyote kwa nchi yoyote katika Afrika hii.

Mhe. Naibu Spika, zaidi ya kwamba tumefanikiwa na karafuu kwa sababu tulitoka nje ya nchi tukaenda kutafuta masoko katika nchi nyengine za nje, Ulaya na katika nchi za Afrika ya mbali.

Mhe. Naibu Spika, naomba tuhakikishe kwamba katika mazao mawili ambayo yanaipatia sana Serikali yetu maendeleo ni karafuu na mwani. Sasa ninamshauri Mhe. Waziri kama aliweza kufanikisha masuala haya pamoja na Serikali ili na yeye aweze kuwahurumia wananchi wetu kuhusu wakulima wa mwani.

Kwa kweli hivi sasa wananchi wengi wa zao la mwani au mkulima wa mwani wanaathirika sana kutokana na zao hili kwamba halina bei.

Kwa kweli kama karafuu imefika kilo shilingi 14,000 hadi shilingi elfu 10,000 kwa *quality* ya chini, sasa utashangaa sana kwamba na mwani una *quality* zake

lakini hadi dakika hii ninazungumza *quality* ya mwani haijafika shilingi 1,000 kwa kilo ambayo *first quality* ndio unaambiwa shilingi 700.

Sasa naomba Mhe. Waziri kuna chakula gani katika dunia ambacho kinauzwa shilingi 700 kwa kilo, utakuta tunawadhalilisha sana wananchi wetu na kuwafanyisha maisha magumu sana na kwamba kuwafanyisha wawe na maisha duni, kila siku wao wanaishia kukopa hata hiyo kilo ya mchele hawaipati, kwa sababu kilo ya mchele haitoshuka shilingi 1,000.

Kwa hivyo, uuze kilo mbili za mwani hiyo *first quality* ndio shilingi 700, *quality* ya chini ni shilingi 500 kwa hivyo uuze kilo mbili za mwani ndio uweze kufanikisha kupata kilo moja ya mchele tena mapembe.
Hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri akija anihakikishie ataanza lini safari kama ile aliyoipanga akaenda nchi za nje wakati 2010 nilimuona Mhe. Waziri alichacharika sana kwenda nje kutafuta bei ya karafuu wakati niko katika jumba hili hili.

Sasa nataka anihakikishie ni lini ataanza safari hiyo kuhakikisha wananchi wanapata bei ya mwani.

Nilizuzungumza sana na Mhe. Waziri vipindi vingi nilimdai hata namaliza muda huu wa miaka yangu 5 mpaka leo sijapata jibu zuri la kuhakikishiwa kwamba bei ya mwani itapanda angalau kufika shilingi 1000, nikaomba bei angalau ya pilipili hoho nayo iangaliwe, kwa sababu ndio vilimo vya watu wa chini ambao wanalima sana katika majimbo yetu.

Sasa naomba Mhe. Waziri, ahakikishe kwamba anawasaidia wananchi wa hali ya chini na wao kuweza kupata *quality* kama lilivyopata *quality* zao la karafuu; ambao wenzetu hivi sasa wamepata maendeleo ya kuweza kuwa na usafiri angalau kupata na nyumba.

Mhe. Naibu Spika, lakini utaona mtu wa mwani wengi wao hivi sasa wanalala katika vibanda ambavyo hohe hahe ambayo havina hata mlango. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri ahakikishe kwamba bidii kama ile ambayo aliitekeleza pamoja na Serikali airudie ili kuhakikisha wananchi wetu wanapata mahitaji mazuri ya kuhakikisha mwani nao unapanda bei kwa mwaka 2015/2016.

Mhe. Naibu Spika, hapo kutetea suala la mwani na bado sijapata jibu na nitahakikisha kwamba Mhe. Waziri amenipa jibu la suala la mwani ndio hapo inawezekana nikaunga mkono bajeti yake.

Nakuja ukurasa wa 8 kuhakikisha kwamba bei ya vyakula. Mhe. Naibu Spika, hivi sasa ukienda katika maduka yetu kila siku ukiuliza unataka mchele hata ule mapembe unaambiwa umeshazidi japo senti 10 au senti 20.

Ukienda kununua jasmine umetoka kwenye shilingi 35,000 hadi sasa unafika 38,000 au 40,000. Huko kwenye chakula kizuri zaidi ambacho siwezi kukiuliza kama kimepanda lakini nazungumzia hiki chakula cha watu ambao kama sisi wa chini kwa nini kinapanda bei kila siku.

Utaambiwa kwamba chakula kinapanda bei sababu ya dola imepanda, niulize Mhe. Naibu Spika, kila siku tunasikia kwamba chakula kimepunguzwa ushuru kwa chakula cha chini kama mapembe, jasmine, unga wa ngano pamoja na mafuta, ushuru umeondolewa kabisa, hiyo dola inatokea wapi ya kuweza tusiwasaidie wananchi kuhakikisha kwamba chakula hakipandi. Kama hivyo chakula kinapandishwa kila siku ninamuomba Mhe. Waziri basi aondoshe kabisa huu ushuru kupunguziwa. Kwa sababu tunasaidia sana matajiri wa hali za juu lakini tunawaumiza sana wananchi wanyonge kutokana na maisha ya kwamba dola tunaisingizia imepanda. Lakini katika dola mchele wa mapembe naona hauna dola ya kusema umepanda, sasa iweje dola inapandisha hata mchele wa mapembe wakati mchele wa mapembe huko nje tunasikia wanapikiwa farasi na wanyama wengine kwamba hapa Zanzibar tunakula sisi binadamu. Sasa iweje chakula hicho kipandishwe bei.

Ninamshauri Mhe. Waziri bei ya mapembe ishuke zaidi ya hapo ilipo hivi sasa, ili kuhakikisha wananchi wetu wanaweza kujilisha angalau milo mitatu kwa hicho chakula cha mapembe.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu mchele kuna aina nyingi sana; kuna huo mapembe, kuna mchele huo wa jasmine pamoja na huo mchele ambao wanakula wakubwa zaidi ambao haina haja wao kuutaja ambao wanakula mtu wa juu lakini hivi vyakula vya chini namuomba Mhe. Waziri, ahakikishe kwamba 2015/2016 mchele huu unashuka bei kutoka shilingi elfu moja unaoendelea uwe angalau shilingi 700 kama ilivyokuwa bei ya mwani, ili kupunguza matatizo ambayo wanayo wananchi wetu ambao wahakikishe na wao wanakula milo 3 hata kama mtu atakula asubuhi mchele, mchana ale mchele na usiku ale mchele, lakini atakuwa amejikimu na kuweza kula milo 3 kama inavyotakiwa na Serikali yetu, watu wahakikishe wanapata milo 3 katika nchi yetu. Akija hapa naomba Mhe. Waziri anihakikishie kwamba chakula anazungumza na matajiri kwamba ni lini chakula ambacho kimetolewa kwamba hakina ushuru kinashuka bei.

Mhe. Spika, nikiendelea naendelea na vifaa chakavu vinavyoletwa nchini. Hivi sasa nchi yetu kwa kweli haina viwanda lakini ni sawa kama tuna viwanda kwa

sababu tuna viatu vingi *used* vinaletwa hapa nchini tena viwanda hivyo vya kila aina. Unaletewa baiskeli kila *quality*, unaletewa *radio* kila *quality* unaletewa na vitu vyengine vya matumizi ya nyumbani.

Mhe. Naibu Spika, vitu hivyo sasa vimekuwa vingi nchini kwetu ambavyo vinahatarisha hatari hata katika pembe za kona za barabara. Ukitaka kujua hatari ya vitu hivyo pita barabara ya Muembeladu utahakikisha kwamba vitu hivyo vimefika hata maeneo ya barabara. Pita eneo la Kwamchina utahakikisha vitu hivyo ma-*freezer* na mafriji yapo hata maeneo ya barabara.

Mhe. Naibu Spika, ukweli vitu hivyo vinasababisha ajali mara nyingi sana kupondwa watoto ama kupondwa watu ambao wana ulemavu, kwa sababu akitaka kurudia sehemu nyengine utakuta pamewekwa ma-*freezer*. Ukitaka kurukia sehemu nyengine utakuta pamewekwa ma-*used* ya baiskeli hata wananchi wanashindwa kutembea katika maeneo ya barabara.

Mhe. Naibu Spika, ningelitoa ushauri kwamba kwa nchi zilizoendelea huko tulimotembea tembea tuliona sehemu maalum ambazo zinatengwa kuweza kuuza vitu kama hivi, na sisi kwa kweli maeneo tunayo mengi ya kuweza kuhakikisha kwamba *used* zinapofika nchini zipelekwe katika sehemu ambayo inaweza kufaa wananchi wakaenda kutafuta *used* katika hizo sehemu.

Si tatizo tukaona kwamba watu wanapanda magari kwenda hata Makunduchi kuna maeneo makubwa sana ya kuweza kuweka *used*, maeneo ya mapori mengi sana yakisafishwa tunaweza kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanakwenda kuchukua ma-used kwa ajili ya matumizi ya nyumbani au matumizi ya usafiri katika mji wetu.

Si vizuri vitu vile vinachanganywa na vitu *first quality* vinavyotoka Uingereza na sehemu nyengine ambavyo ni vipya vinachanganywa kuuzwa pamoja na ma-*used*, hiyo tunajitukanisha katika nchi yetu kwamba wakipita watu wanaotoka nje watahisi kwamba nchi yetu ni ya ombaomba, kumbe nchi yetu ni tajiri sana.

Kwa vile nchi yetu ni tajiri huwezi kufananisha na nchi nyengine ambazo zina ukame kama vile Burundi, Rwanda na sehemu nyengine, lakini utakuta ukienda huko huwezi kukuta ma-*used* yanauzwa ndani ya maduka katika mji ule vitu vyote vimetengwa nje ya mji na watu wanafuata huko kuweza kununua.

Hata ukienda hapo Tanzania Bara kuna sehemu maalum ambayo *SIDO* imetayarisha viwanda vyake vidogo vidogo unaweza kwenda pale kununua vifaa ambavyo vya *used*, na sio kwamba vinachanganywa katika maduka ya pale mjini. Yalikuwepo hapo kwanza lakini hivi sasa maduka mengi yamesafishwa na vitu

kama vile vya *used* tayari vimewekwa nje ya mji kuhakikisha kwamba ule mji unakuwa safi.

Mhe. Naibu Spika, sasa utaona kwamba mji wetu kila siku unasafishwa na haupatikani kuwa msafi kwa sababu vitu vyake vinachanganywa. Utakuta mitumba iko pale pale, utakuta *used* za baiskeli pale pale, utakuta ma-*freezer* na mafriji yapo katika sehemu moja ya mji mzima. Kutokana na kutaka mji wetu ulingane na nchi nyengine za Afrika ambazo zimeendelea kama vile Afrika ya Kusini na sehemu nyengine, napendekeza Mhe. Naibu Spika, vitu hivyo vyote vitoke nje ya mji ili kuhakikisha mji wetu unakuwa safi na usalama wa wananchi wetu kuhakikisha kutembea katika maeneo wanayotembea kwa usalama, na sio kupata madhara hasa kwa vile sehemu nyingi wapo walemavu, sehemu nyingi wapo watoto wanaokwenda skuli hawawezi kurukia sehemu ya usalama, unakuta watu wengi wanapondwa au wanapata maumivu kutokana na kuwa mji umebanwa sana na vitu vya *used*. Ninamuomba Mhe. Waziri ahakikishe kwamba hivi sasa wakati umefika kuhakikisha kwamba Zanzibar inalingana na nchi za Ulaya ama nchi nyengine za Afrika ambazo zimeendelea.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu usafirishaji wa magari ambao hivi sasa unaendelea katika nchi yetu, hivi sasa utakuta biashara ya magari imekuwa nyingi sana katika nchi yetu na magari yanayokuja hapa nchini yamepitwa na wakati, sasa imekuwa hili ni jaa la kuleta magari ambayo ukienda kule sehemu ya Maruhubi utakuta kuna magari ambayo yameletwa hivi sasa yana miaka 5, miaka 6 hayanunuliwi tena, imekuwa hivi sasa Zanzibar ni jaa la magari ambayo sio *quality*.

Ningelipendekeza Mhe. Waziri, ahakikishe yanaletwa magari ambayo yametoka miaka hii ya 2010 hadi 2015 lakini utakuta magari yanayoletwa ni yale ambayo yamepitwa na wakati tangu mwaka 1990, 2000 kutokana na watu wanapenda urahisi, na hapa wanapafanya jaa kwamba Zanzibar imekuwa jaa la magari na utakuta magari mengi hayanunuliwi kwamba ni *quality* yake yamepitwa na wakati.

Ningelimshauri kuwa magari yanayoingizwa yahakikishwe magari yanayokuja hivi sasa yapo *standard* kuweza kuletwa nchini kwetu na kuweza kuuzwa kwa wananchi wetu yakiwa safi na salama.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo mchango wangu mdogo ambao ninaichangia wizara hii, sitounga mkono sasa hivi asilimia kubwa hadi pale Mhe. Waziri ataponihakikishia kwamba wakulima wa mwani, ma-*used* pamoja na magari yamefanyiwa utaratibu mpya katika nchi yetu. Ahsante sana.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nitumie fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma sio tu kwa

kuendelea kutupa uhai lakini kutufikisha siku ya leo ya mwezi mosi Ramadhani, hii ni hazina kubwa aliyotujaalia *Allah,* na kwa vyovyote vile hatuna budi kumshukuru.

Ama baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu na hatimaye kumtakia rehma Mtume wetu *Muhammad (S. A. W),* nadhani vile vile nitakuwa sikufanya jambo jema kama sikutumia fursa hii kukushukuru Mhe. Naibu Spika, na wewe kunipatia fursa hii ya kuweza kutiatia nyalio.

Mimi si msemaji sana katika masuala haya ya biashara, kwa sababu mimi mara nyingi ni mkulima na mvuvi. Sasa inabidi hata michango yangu katika wizara hii nita-*regard* zaidi kwenye mambo haya ya *marine and agro-processing industries* kwa sababu ni mvuvi na ni mkulima tu.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, baada ya hayo nianze na pale alipopaacha mdogo wangu Mhe. Mohamed Mbwana Hamad, nianze pale alipomalizia yeye, alimalizia kwenye hili duka la vioo pale Darajani.

Mhe. Naibu Spika, *main role* ya Wabunge na Wawakilishi ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na matumizi mazuri ya *public assets* zikiwemo za walipakodi wa nchi, *public assets* ni pamoja na majengo. Sasa sisi hapa tuna *role* kubwa ya kuona kwamba majengo ya nchi, majengo ya serikali yanakuwa na matumizi mazuri.

Kwa hiyo, Mhe. Mohamed Mbwana alitaka maelezo tu, lakini mimi baada ya kusema Mhe. Mwakilishi pale niliangalia Gazeti la Zanzibar Leo la siku ya Jumanne 17 Machi, 2015.

Mhe. Naibu Spika, gazeti hili naomba uniruhusu ninukuu katika ukurasa wake huu wa 14 wa gazeti la siku hiyo la Zanzibar Leo, lilisema mualiko wa zabuni naomba uniruhusu kidogo hii *page* ya mwanzo tu hapa Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa nisome.

"Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inakusudia kukodisha jengo lake liliopo Darajani Unguja ambalo lina sehemu mbili. Jengo hili ni kubwa na lina ukubwa wa 177 *square meters,* hivi sasa sehemu moja inatumiwa na washirika wa masonara katika parandesi. Na sehemu ya pili inatumiwa na Kampuni ya *Vodacom* inayomaliza mkataba wake mwezi wa Juni, 2015".

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa ni Juni hakutaja tarehe huyu lakini ni kwamba *Vodacom* tayari tuchukulie hawapo tena katika lile jengo la serikali. Kwa hivyo, mapato wanayolipa yanasita, sasa nilitaka nimuulize Mhe. Waziri vipi *tender* hii, kwa nini hadi leo hii haijafunguliwa kuna sababu gani za msingi.

Kwa hivyo, naomba mwisho aje anieleze kwa nini haijafunguliwa *tender* hii, na mpangaji wa pale mmoja ameshamaliza muda wake, na lile jengo kwa mujibu wa taarifa hii hii ya kwenye *tender* ni kwamba panataka pajengwe ghorofa pale ili maslahi ya nchi yaongezeke. Ni sababu gani za msingi ambazo hii *tender* hadi leo hii imetiwa mfukoni tu haijafunguliwa?

Baada ya dibaji hiyo fupi Mheshimiwa sasa mimi naomba niende moja kwa moja katika ukurasa wa 32 wa hii hotuba.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 32 wa hotuba hii kuna Idara ya Maendeleo ya Viwanda na Ukuzaji Wajasiriamali.

Mhe. Naibu Spika, lazima tukubali kwamba Zanzibar tuko nyuma sana katika masuala ya viwanda, na mara nyingi Zanzibar inategemea zaidi uchumi wake mazingira yaliyotuzunguka. Asilimia karibu ya 80 katika watu wa vijijini tunawekeza maisha yetu katika uvuvi na kilimo.

Katika suala hili la uvuvi na kilimo sisi ni wavuvi wadogo wadogo tunavua kwa kutumia vyombo hivi vya kawaida, na takriban soko letu linabadilika badilika sana kutokana na msimu. Kwa hivyo, kipato tunachokipata katika uvuvi ni cha kujaribu na kubahatisha, kwa sababu hatuna soko ambalo ni *reliable*, soko letu ni la *fluctuate according to production* ya wale samaki, *we don't have fixed prices* katika soko la samaki linabadilika siku hadi siku.

Soko ambalo achilia mbali kutupatia kipato, lakini hata kutupunguzia njaa ambapo Mradi wetu wa MKUZA unasema unatilia mkazo zaidi kwa mambo haya; *poverty reduction and income generating*. Kwa hiyo, uvuvi tunaovua sasa hivi wa samaki na madagaa hautuongezei kipato wala hautupunguzii umasikini, inakuwa ni kama vile chuma ulete tu, unaenda zako pwani ukirudi kushauza unakimbilia dukani pesa zote unaziacha pale kwa ajili ya kula tu. Hiyo ndio *style* ya uvuvi tunaofanya kuanzia tangu 1964 *upto date we are going under trial and error fishing*, nchi tuliyozungukwa na bahari. Kwa hivyo, serikali yetu haiko *creative* katika kutupunguzia umasikini, inasikitisha sana kwamba serikali yenyewe haiko *creative* katika kuondoshea umasikini wavuvi, lakini wavuvi tunatokana kujikusanya katika makundi tukaweza kujipunguzia umasikini kwa kuvua na kujitafutia soko, vile vile serikali haitupi *support*.

Tumejikusanya wavuvi wa dagaa kwa wingi sana katika eneo la Maruhubi pale, tumejikusanya kwa sababu hakuna kiwanda ambacho ni *Canning Industry* ya kuweza kuuza hawa samaki wetu.

Tumejikusanya pale pale tunaanika madagaa katika *local style* kwa kutumia jua tu hili, na siku za mawingu (Masika) ina maana dagaa letu linaoza. Serikali itueleze imesaidia nini pale Maruhubi, imesaidia nini Nyanjale katika suala zima la hawa wajasiriamali munawaita *clusters entrepreneurs,* hawa ni *clusters* sio *individual entrepreneurs,* ni *clusters entrepreneurs*, wanatafuta wao wenyewe soko; *DRC*, Zambia, mumekuja kutuletea hivyo vifungasho, tunatumia haya haya mapolo ya kawaida ambayo hayana viwango.

Tunashukuru hilo soko letu huko kule *DRC* bado wanaendelea kutumia tu dagaa letu, tulifikiria kwamba mungekuja wataalamu katika suala hili mkatutafutia *special packages, scientific packages* kuweka madagaa yetu katika hali ya mapolo ya kilo 50, kilo 25, *plastic* la kawaida hakuna hata vifungasho, nyinyi hamuwezi kututafutia soko tumejitafutia wenyewe.
Leo mnasema mna vifungasho vya chupa, haa, jamani dagaa linatiwa kwenye chupa. Hili ni tatizo Mheshimiwa na embe mikebe kwenye chupa tulivyoambiwa vifungasho vinavyotafutwa.

Kwa hiyo, wauza dagaa wa Nyanjale, wauza dagaa waliopo pale Maruhubi wanataka *scientific packages,* tunaendelea kutumia mapolo haya haya ya mchele wa *Bopar Enterprises*, tulikuwa tunataka mtuletee *packages* ambazo zina majina *Maruhubi Entrepreneurs*. Leo tunatumia mapolo yenye nembo za kina *Bopar* ndugu yangu pale. Jamani tusaidieni wavuvi, hamuna uwezo wa kutupatia masoko nyinyi serikali, hamna uwezo wa kujenga viwanda hapa lakini angalau mtupe *support* za kitaalamu. Hilo la kwanza.

Mhe. Naibu Spika, mara nyingi huwa nasema hapa hebu jamani iangalie bahari kama hii Bahari ya Hindi, hatuna mafuta sisi hivi sasa, hatuna viwanda hivi sasa, basi sisi iweje Watanganyika waweze kuwa-*mobilize* wawekezaji wakubwa kwenda ku-*install* viwanda vya kusindika minofu ya sato na sangara. Sisi tushindwe kuwa-*mobilize* wawekezaji kuja kusindika minofu ya majodari ambayo ni mitamu sana, minofu ya papa ambayo ni mitamu sana, minofu ya changu ambayo ni mitamu sana.

Leo ina maana ile *convincing language* hapa Zanzibar viongozi wetu hamna. Mimi kama ni Vitongoji uvuvi wa kawaida siuwezi, lakini nyinyi serikali kwa nini Serikali ya Jamhuri imudu kuwa-*mobilize* watu kwenda kuwekeza kule Tanganyika katika Ziwa Victoria mushindwe kuwa-*mobilize* wawekezaji nyinyi hamna uwezo. Serikali yetu sisi ni kokoto, haikui, maana kokoto iko hapo hapo haikui, tangu 1964 mpaka sasa hivi serikali hii ni changa tu, basi ni kokoto! (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa mimi naomba sana katika hili ili umasikini upungue na tuweze kujiongezea kipato lazima muweke hizi *marine processing industries*, tuweze sisi kujikita sana katika upande huu, kwa sababu mazingira yetu tumezungukwa na bahari kubwa.

Mhe. Naibu Spika, inasikitisha sana kwamba mimi pale Vitongoji vile vile ni mkulima mkubwa wa tungule sisi tunaita tungule nyinyi huku mjini mnaita nyanya. Nalima tungule, nina miembe mingi kabisa aina ya mviringo sisi tunaita pembeni kule, nyinyi munaita mviringo.

Ukija msimu embe tunavuna mpaka zinaoza tunawapa ng'ombe manguruta kwa manguruta ya maembe yameozeana tunawapa ng'ombe. Inasikitisha sana kwamba tangu 1964 tulipopindua sisi hapa mpaka leo hii hakuna hata kiwanda kimoja cha ku-*can* embe, cha ku-*can tomato* tunashindwa, na Waomani wamekuja juzi wanatuuzia sisi tena kwenye jangwa bwana. Sultan Qaboos pale pamefanywa jangwa wanatuuzia *tomato paste,* eti Mzanzibari ananunua *tomato paste* kutoka Oman ni kwenye jangwa, wakati sisi huku kule Vitongoji zinaliwa na ng'ombe, jamani si aibu hiyo? Inasikitisha sana.

Sultan Qaboos kaja juzi juzi tu pale kawa *creative*, kaligeuza jangwa kuwa nchi ya mbolea, sisi nchi ya mbolea tunapata mvua kila siku hapa, lakini matungule tunazalisha lakini *there is no even single canning industry*, ni tatizo. Maembe yale Said Salim Bakhressa anatuletea *juice* ya maembe, sisi Vitongoji huwa nalia mimi sasa, kwamba maembe ya pembeni haya yapo yanaoza nanunua *juice* ya Said Salim Bakhressa, ni tatizo, hebu twambieni nini kikwazo? Serikali twambieni. Kama ni wataalamu wa kilimo tupo pamoja na siasa yetu tupo kabisa, mimi najua mambo haya ya *agro processing industry*, nimesema pale *Fidel Castro* ilikuwa ni Chuo cha Kilimo sikuendelea lakini kuanzia *form one* mpaka *form six* nimo nafanya mambo haya ya *agricultural*, sasa sijui nyinyi mnakwama wapi.

Waheshimiwa, mnatutia aibu, watu kama sisi tulioleta mapinduzi nchi hii, kwamba mpaka sasa serikali inashindwa kuwa na *single canning industry* tena *agro-processing industry* nchi yenyewe inapata mvua mara tatu kwa mwaka. Tunashindwa na watu wa jangwa kule, Waomani wanatuuzia *tomato paste*, sisi *tomato* zinaliwa na embe zinaoza. Said Salim Bakhressa anatuuzia *juice* ya embe sisi kule tunalia.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende katika suala zima la kile kiwanda chetu cha kafaruu. Mheshimiwa suala zima la ununuzi na usafirishaji wa karafuu nimeangalia ununuzi na usafirishaji. Unaona basi, mambo mliyoyaacha hapa ununuzi na usafirishaji. Huwezi kununua karafuu kusafirisha bila ya kuanza kuzilima, kuzibeba na kuzifikisha hapo *ZSTC*.

Mhe. Naibu Spika, nimeona bei humu za kilo safi, kilo iliyokuwa wastani na mpeta lakini mimi ninachotaka niwaambie Waheshimiwa ni kitu kimoja, kwamba nyinyi hamumuangalii mchumaji, hakuna mkataba baina ya tajiri mwenye mikarafuu na yule kibarua, hakuna mkataba huo. Sasa nyinyi mtafanya nini hii serikali kumuona na mchumaji pamoja na yule anayebeba gunia, maana hazifiki tu melini, nyinyi mkienda mkauza mkapata mapesa lazima kuna mpagazi pale mwanangu!

Sasa mpagazi mnamlipa je, huyu mchumaji ana-*risk* maisha, pishi shilingi elfu mbili achume mchana wa kutwa na wenyewe wengi wanawake na hii mikarafuu. Mimi kila nikisema hapa naonekana mbaya kuhusiana na mikarafuu, kwamba mikarafuu ni mirefu hii tutafuteni *species* nyengine ya mikarafuu, wachumaji wengi ni watoto wanawake hawa wanaona kiwewe sasa wakibanwa na mikarafuu mikubwa namna ile.
Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani kuna haja ya ku-*review species* ya mkarafuu kule Oman, sidhani kama tukiboresha huu mkarafuu kama uzalishaji utapungua, haupungui hata siku moja, labda *life span. Life span* ya mkarafuu ambayo ni chotara unaweza ukapungua ikawa ndogo, lakini uzalishaji unaweza ukazidi na ukifa utapanda mwengine una wasi wasi wa nini wewe na wakati wewe si Mungu kama utaufanya ufe ule, Mungu ndiye anayefanya uote.

Mhe. Naibu Spika, mimi nashauri sana kwamba kuna tatizo sasa la haya mabadiliko ya tabia nchi. Mkarafuu huu wa zamani unahitaji maji mengi, *variety* nyengine tukiileta hapa, tuleteni *variety* ambayo ina-*look like with our environment*. Yaani mabadiliko ya tabia nchi yanabadilisha hata *PH* ya *soil,* kwa sababu ili mkarafuu umee unahitaji *acidic soil.*

Sasa haya mabadiliko ya tabia hewa *acidic soil* kutokana na ongezeko la hewa ukawa, basi inabadilika kidogo inakuwa kitu *bicarbonate*. Sasa mimi nawaambieni kwamba hebu tufanye utafiti mwengine musiwe wakaidi katika ma-*scientist* wazuri, tuje tuangalie *variety* yetu ya mkarafuu, tuwaonee huruma na hawa kina mama wanaopanda mikarafuu mirefu sana na uzalishaji hautapungua.

Mhe. Naibu Spika, mimi niende kwenye hicho Kiwanda cha Makonyo baada ya pale karafuu nataka niruke kidogo pale Kiwanda cha Makonyo.

Mheshimiwa kama kuna kiwanda ambacho hakikufanywa utafiti wa kina ni kile Kiwanda cha Makonyo, kile kimejengwa kisiasa, hakikufanywa *Thorough Feasibility Study*, kile kiwanda kimejengwa kisiasa, katika miaka ile kwamba wakubwa wakae pale wajenge karibu kiwanda bila ya kujali madhara.

Waheshimiwa, nimeambiwa hapa kuna sijui shilingi milioni mia mbili na ngapi zitapatikana kwa kila mwaka kutokana na uzalishaji wa mafuta ya makonyo. Milioni mia mbili zina thamani bora zaidi kuliko afya za watu? Pale linalovutwa yaani mimi juzi nilikuwa natokea kwangu Makaani Vitongoji huko nikapita na kipindi hiki cha uzalishaji, kuna wingu la moshi mnalazimika kupumua; kuvuta pumzi, matokeo yake ukivuta pumzi ile *carbon monoxide* sijui ni *carbon dioxide* ni *oxide of carbon,* iwe *carbon dioxide,* iwe *carbon monoxide,* lakini ni *oxide* ya *carbon* ambayo ikiingia kwenye mwili inakutana na kitu kinaitwa *hemoglobin* mle ndani. *Hemoglobin* ni lile *reddish compound* katika damu.

Sasa *hemoglobin plus carbon monoxide* kinapata kitu kinaitwa *carbon zee hemoglobin* ambalo ni *toxic compound,* ni sumu ukiipumua mwaka wa mwanzo, ukiingia mwaka wa pili unavuta pumzi ile, ukipumua mwaka wa tatu mpaka miaka 20 una-*destroy body cells. Finally* unapata kitu kinaitwa *cancer,* mnataka sisi tufe kwa *cancer* watu wa Wawi kwa kiwanda kile? Hizo kodi mnazokusanya mkaendesha serikali mtazipata wapi tena, sisi tukishakuwa wagonjwa pale Wawi? Hili ni tatizo. Ama kiwanda kipandishwe juu lile nyororo la moshi au kihamishwe kabisa kile mtatuuwa. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Mheshimiwa, umemaliza?

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ndio, siungi mkono hoja mpaka nitakapokuja kuambiwa habari ya kiwanda cha makonyo kitafanywa vipi. Sisi wavuvi wa madagaa tulioko pale Maruhubi tunaletewa lini vifungasho na tungule zetu zinazoozeana pamoja na embe. Tutapatiwa lini *Agro-processing* na sisi kule, hapo ndio nitaunga mkono.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Mhe. Naibu Spika, na mimi nakushukuru sana kunipa nafasi hii kutoa mchango wangu mdogo kabisa, lakini ilimradi kwa vile tuko kazini nitoe mchango tu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu (*S.W*) aliyenijaalia mchana huu kuwa katika hali ya uzima na afya inaniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kuwawakilisha wananchi wangu.

Vile vile, nimpongeze Mhe. Waziri makini wa wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko pamoja na Naibu Waziri na watendaji wake wote kwa kazi nzuri wanayoifanya kutuletea hotuba hii ambayo tumeifahamu vya kutosha na sasa hivi tuko tayari kuifanyia kazi kwa michango yetu na baadae kuipitisha kwa vishindo kabisa.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu nitajikita katika ukurasa wa 9 kwenye kifungu cha 23, kwa ruhusa yako naomba ninukuu kama ifuatavyo:-

Kifungu cha 23 kinasema kwamba;

"Mwenendo wa Bei ya Karafuu na Mwani;

Mhe. Naibu Spika, wizara yangu imeendelea kufuatilia mwenendo wa bei ya mazao ya mwani na karafuu ambayo huzalishwa na kusafirishwa na Zanzibar..."

Mhe. Naibu Spika, hapa limetajwa zao la karafuu katika mwendo mzima wa bei na kusafirishwa. Mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu hili zao la karafuu kidogo *Alhamdulillah* msimu unapofika watu nao hufaidika mpaka watoto wadogo, watu wanaokota mpeta wanakwenda msimu mkubwa, wanaokota chini na wanapata sare za skuli. Lakini zao hili la karafuu ni zao linaloleta tija katika serikali yetu, hivyo ni jambo la kulienzi na kulifanyia kazi kwa kina.
Mhe. Naibu Spika, lakini tumuangalie kama alivyozungumza Mhe. Saleh Nassor, mchumaji wa karafuu tunamtizama vipi? Haziendi kwa kusafirishwa tu hizi tunaanza na chini katika kuliokoa hilo zao. Sasa huyu mchumaji wa karafuu tunamuangalia vipi katika kuliokoa zao la karafuu la serikali yetu kupata mapato hasa ya kigeni.

Ni ukweli usiopingika alizungumza mchangiaji aliyekaa kitako hapa kwamba wachumaji wa karafuu wanawake wanashamiri. Mimi nina ushahidi msimu uliopita wa karafuu mwaka jana kuna mwanamke mmoja ni mzaliwa wa Pemba lakini anaishi Dar es Salaam, katoka huko kuja kuokoa zao la karafuu (kuchuma). Kwa bahati mbaya katika kuchuma Mwenyezi Mungu kamjaalia kaanguka mkarafuu, mwanamke huyo kaanguka na mpaka hivi sasa nazungumza amekwenda kutibiwa kule Muhimbili lakini sasa hivi kesharudi Pemba ni kilema kabisa.

Sasa tunataka Mhe. Waziri atakapokuja hapa atwambie wanawatizama vipi wachumaji karafuu na wanaopata ajali wakati wakiliokoa lile zao la karafuu. Mheshimiwa tunamuomba kwa kina akija hapa atuelezee wanawatizama vipi hawa ni hatari kabisa, mtu anakwenda kwa madhumuni ya kipato lakini kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu anaanguka. Wizara au serikali imtazame kwa jicho la huruma *wallahi* sasa hivi kilema yuko pale kakaa tu hatujui serikali itamtizama vipi na mimi nimefanya kosa kwenda kumuulizia umesaidiwa vipi? Lakini *Inshaallah* nikienda nitamuangalia.

Mhe. Naibu Spika, zao la mwani ni moja katika mazao ya baharini. Serikali imefanya mpango huu kuwashajihisha wananchi kupanda zao la mwani, lakini inasikitisha bei hii kila siku waziri anakwambia anakwenda kutafuta masoko lakini

hayapatikani. Kwa sababu bei zake ziko pale pale 450 kwa wingi ni shilingi 500 ni tatizo, tunawaumiza wananchi wetu na wito huu umeitikiwa sana na wanawake kwa kule Pemba. Wanawake ndio wapandaji wakuu wa mwani lakini hii kazi ni ngumu na nzito na kipato chake ni kidogo sana.

Mhe. Naibu Spika, tunaomba waangaliwe kwa jicho la huruma angalau kama alivyozungumzia Mhe. Mussa Ali Hassan, hapa iende sambamba na hiyo kilo ya mchele, mtu akipata ile kilo ya mwani apate angalau kilo ya mchele, lakini leo shilingi 450 unapata nini na inachukua muda kupata mpaka kuukausha ule mwani ni kazi nzito ambayo haina tija. Tunamuomba Mhe. Waziri tunamuamini sana aende katika mienendo yake kuwatafutia soko hawa wapandaji wa mwani angalau upande bei, sio kila anapokuja kwenye bajeti tunakuta shilingi 450, 500 hairidhishi kabisa inatuvunja matumaini. Tukiendelea kama ilivyozungumzwa kila siku vyakula vinapanda bei hasa kisiwani Pemba kwa sababu ya mambo ya usafiri. Sasa kama angetutengenezea ile bandari ingekuwa bei za Unguja na za Pemba zinafanana, lakini huu usafirishaji wa mara kwa mara mchele ushushwe Unguja halafu usafirishwe utiwe botini uende Pemba ni matatizo. Kwa kuinusuru Pemba nayo kuwa katika kiwango kama cha Unguja basi zile bandari zetu zitengenezwe, mfanyabiashara yupo Said Salum Bakhressa hapa ana nia njema tu ya kuitengeneza bandari ya Wete, lakini mpaka leo sijui amekwama wapi. Hebu twambieni amekwama wapi katika kutengeneza bandari ya Wete ili watu wa Kaskazini na Pemba nzima na Zanzibar kwa ujumla wafaidike na lile jambo, tunataka kujua.

Mhe. Naibu Spika, unapoitengeneza bandari watu wengi watapata ajira na watu wengi watafika kufanya biashara ambazo ni nzuri na zenye tija.

Mhe. Naibu Spika, nikienda katika ukurasa wa 55 Mhe. Waziri huyu kawasifia sana wafanyabiashara wakubwa na wadogo, hili nimpongeze sana unapowasifia hao unawapa moyo. Lakini mimi nizungumze tu katika wafanyabiashara wadogo wadogo ambao na yeye kawataja hapa Juakali.

Mheshimiwa, wafanyabiashara wadogo wadogo wa Juakali ni watu wanaotoa huduma kama alivyowaelezea, lakini ni watu unapofika msimu wanapata adhabu kali kutwa wako mbioni, wanatiwa mbioni hawako makini katika kufanya biashara zao na biashara hizo muda mkubwa mtu anaweza kufanya ndani ya Mwezi mzima Mtukufu wa Ramadhani akaibukia hasara kwa kuchukuliwa biashara zake na yule ni mfanyabiashara mdogo anakwenda kukopa kwa wafanyabiashara wakubwa.

Hebu tuwaangalie kwa jicho la huruma hasa kwa huu mwezi wa Ramadhani, tuwaache wafanye biashara zao kwa umakini kabisa na kutafuta tija na kuhudumia wananchi kama alivyowaeleza, lakini *wallahi* inasikitisha sana kila siku mtu

anafanya biashara roho yake ikiwa katika ujiti hana umakini wa biashara ile, mapolo yanachukuliwa wanakimbizwa mbio.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba tuwaangalie kwa jicho la huruma na *Inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu katika mwezi huu mtukufu tutapata faida kubwa sana, hebu tuwaachie katika mwezi huu wa Ramadhani tusiwabughudhi wafanyabiashara wa Juakali. Najua kwamba yeye siye msimamizi wa jambo hili, yeye ni wafanyabiashara wake tu lakini kuna watu wanaosimamia wawaachie wale watu hasa Baraza la Manispaa, iwaachie wafanye kazi zao kwa umakini katika mwezi wa Ramadhani na wao watapata fungu au tuwatafutie mahali ambapo ndipo pa kufanyia biashara zao, lakini sio kila siku wafanyabiashara hawa tunawafukuza kama kuku. Haipendezi kabisa na haiwajengei hisia katika nchi yao.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea imeelezwa hapa katika ufanyaji wa biashara wa Bara na Zanzibar sijui ni biashara gani zinazofanyika, hebu Mhe. Waziri atuainishie ni biashara gani zinazotoka hapa Zanzibar na kusafirishwa kwenda Tanzania Bara na pale Tanzania Bara ni biashara gani zinazokuja hapa Zanzibar. Lakini inasikitisha sana katika haya mambo ya biashara hasa magari unapotoa gari Zanzibar kuipeleka Tanzania Bara, kunakuwa na ushuru kama ndio kwanza inatoka Dubai.

Mhe. Naibu Spika, hili ni tatizo aliangalie kila anayehusika na jambo hili *Inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu walifanyie kazi tunapata tabu sana. Gari unaitoa hapa Zanzibar nchi yenye muungano ambapo tunasema ni nchi moja wala haikubaliki, lakini ukiitoa hapa ni kama unaitoa Dubai ushuru wake ni mkubwa. Hii haipendezi katika nchi moja ushuru ukawa namna hiyo, hebu liangalieni jambo hili kwa kina. Tunaiambia serikali iangalie kwa kina jambo hili linawapa tabu wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu ni mdogo na hapa inatosha kupeleka *message* yangu, namuomba Mhe. Waziri anipe maelezo haya ili niweze kupitisha hotuba yake. Kwanza siungi mkono mpaka nitakapopata maelezo mazuri kwa yale niliyoyachangia nakushukuruni sana, ahsanteni.

**Mhe. Bikame Yussuf Hamad:** Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi kunipa fursa hii nikaweza kutoa mchango wangu mdogo sana katika Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko. Awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutujaalia tukaweza kufika hapa katika Baraza lako hili tukufu, lakini pia kutupatia uzima na kutujaalia ghalima yake ya uzima na tukaweza kufika katika Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie tuufunge kwa salama na amani, lakini pia atutakabalie ibada zetu sote kwa ujumla na wenzetu waliokuwa Mwenyezi Mungu hakuwajaalia kuwafikisha katika mwezi

huu, basi huko waliko awajaalie awape wepesi. Kama wako ndani ya adhabu basi Mwenyezi Mungu awaondoshee adhabu hizo na awape wepesi, *Inshaallah*.

Mhe. Naibu Spika, pili nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa ujumla katika kuleta kitabu chao hiki cha bajeti ambacho wamekieleza kwa ufasaha na ufanisi mkubwa.

Jengine mimi niseme naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja na nianze mchango wangu ukurasa huu wa 5 ambapo kitabu kimeeleza Hali ya Biashara Zanzibar na Usafirishaji wa Bidhaa.

Mhe. Naibu Spika, kitabu kimeeleza kuwa, "Kwa upande wa Zanzibar kwa mwaka 2014, mwenendo wa usafirishaji bidhaa uliendelea kuimarika kwa kuuza nje bidhaa zenye thamani...", kataja hapo kwenye kitabu chake. Lakini akiendelea kasema kuwa, mazao hayo ni pamoja na miongoni mwa bidhaa za mwani, karafuu ambazo husafirishwa na hupatia serikali yetu kipato.
Kwanza nichukue fursa hii kuwapongeza lakini nizungumzie suala hili la mazao ambayo yanaingiza kipato katika nchi yetu likiwemo uzalishaji wa mwani na karafuu. Mimi niende kwenye mwani kama na mimi ni mkulima mkuu au ni mdau wa suala hili la mwani.

Mhe. Naibu Spika, tunajua kwamba zao la mwani limeongezeka kidogo kutoka kule lilikokuwa, tusiondoe shukurani kwa kile ambacho kimefikia ile hatua kiasi fulani. Kwa hiyo, tuchukue fursa hii kushukuru hapo tulipofika. Lakini mimi ushauri wangu ni kuwa bado kutokana na kazi kubwa ya uzalishaji huu wa mwani namuomba Mhe. Waziri kama bado katika soko la dunia hakujaongezeka bei, basi twende na mwani wetu huu katika njia ya kuusarifu mambo mengine. Hiki mimi ndicho ninachokiomba kuwa tuondoke hapa katika kuuza mwani mkavu lakini badala yake twende katika kuusarifu mwani.

Hili linawezekana na wao serikali wanajua na Mhe. Waziri anajua kwamba mwani bado unaendelea kuwa ni zao zuri, lakini pia kuna namna nyengine za kuweza kuusarifu na wakulima kupata kipato zaidi. Kwa hiyo, nimuombe Mhe. Waziri wakulima wa mwani awaone katika uwanja huo sasa, ili mwani waweze kuusarifu na kuuza kwa bei nzuri.

Suala jengine ukurasa wa 12 pameandikwa maendeleo ya viwanda. Maendeleo ya viwanda ni moja ambapo ni viwanda katika bajeti iliyopita nakumbuka ya mwaka 2014/15 viwanda na ubanjaji wa kokoto, pia ni moja ya viwanda ambavyo vinaipatia serikali yetu pato. Lakini bado niseme kwamba watu hawa hawajaangaliwa bado kwa jicho la huruma.

Mhe. Naibu Spika, nirudi katika ukurasa wa pili kasemaje Mhe. Waziri:-

> "Matayarisho ya bajeti hii yamezingatia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020, Mpango wa Ukuzaji Uchumi na Kuondoa Umasikini Zanzibar".

Mhe Naibu Spika, bajeti ya mwaka jana nilizungumza sana kuhusu masuala ya viwanda na wananchi walio wanyonge ambao wanafanya shughuli hizi za ubanjaji wa kokoto hasa wanawake. Wanawake wanawekeza katika ubanjaji wa kokoto lakini bado serikali haijawaangalia na ikaweza kuwapatia angalau mafunzo fulani au kuwapatia vifaa kuondokana na kule kubanja kokoto kwa mikono.

Mhe. Naibu Spika, katika Mkoa wa Kaskazini Wilaya ya Micheweni ile Micheweni yenyewe watu wengi walio katika maeneo yale ni wabanjaji wa kokoto, wachongaji wa matofali, wachimbaji wa mawe, lakini nashangaa serikali na siku zote tunasema kwamba katika watu wanaoongoza walio na umasikini uliokithiri Wilaya ya Micheweni, lakini nashangaa zile shughuli wanazozifanya bado hawajapatiwa na wakaonekana kwamba lazima na wao waweze kushajihishwa.

Katika kitabu chake hiki Mhe. Waziri ameeleza kuwa katika maendeleo haya, kuna Idara hii ya Maendeleo na Viwanda na Ukuzaji wa Wajasiriamali, kuna viwanda hapa ambavyo vimetajwa kuna bekari ambazo zinatengeza biskuti ndivyo vinavyotembelewa, miradi ya kuchoma *chips* ndio inayojulikana. Kuna mradi wa kuzalisha *tomato*, lakini mradi huu ambao wananchi wamewekeza na wao tena wale walio wanyonge bado wizara haijawaona ikenda na wao wakawafanyia tathmini katika miradi yao mizima hii wanayofanya, ili na wao kuwawezesha kuondokana na ule ubanjaji wa kokoto kwa kutumia nyundo na mikono yao Mhe. Waziri.

Kwa kweli wale wananchi wanapata tabu sana, ni watu wanyonge wanawake wa wilaya ile karibuni kucha hawana tena. Kwa hiyo, nakuomba Mhe. Waziri basi na wao ufanye tathmini katika suala zima hili la idara yako hii ya maendeleo ya viwanda na ukuzaji wa wajasiriamali.

Nakuomba sana Mhe. Waziri muende mkafanyie tathmini kama mnavyosema kuwa wizara yenu hii inafuata sera ya kukuza Uchumi na kuondoa umasikini wa kipato. Kwa hiyo, naomba Mhe. Waziri wale watu uwaangalie kwa jicho la huruma.

Suala jengine nichukuwe fursa hii kuwapongeza wizara kwa ukusanyaji wao wa mapato ambayo kwa kiasi fulani basi wamekusanya mapato ambayo yanaridhisha

kabisa ambapo ni mchango mkubwa wanaotoa kuupeleka kwenye mfuko mkuu wa serikali. Hilo niwapongeze.

Jengine Mhe. Naibu Spika naomba Mhe. Waziri atakapokuja anieleze kwa sababu bajeti iliyopita tulielezwa kuwa katika maeneo huru moja liliyoko kule Micheweni kuwa kuna huyu muwekezaji wa Kiwanda cha Sukari; tulitiwa tamaa pale kuwa atakwenda pale katika kuekeza na tukapata matumaini makubwa kuwa huenda wananchi wa kijiji kile nao wakafaidika na mradi huu pindipo utawezekana kufika pale. Kwa hiyo, tunaomba Mhe. Waziri atwambie hili suala lipo bado, tutie matumaini au pengine muwekezaji huyu kesharudi nyuma.

Jengine Mhe. Naibu Spika, kuna wajasiriamali, piakuna na wafanyaji biashara. Hawa ni watu tafauti. Sasa miongoni mwa kilio kilichokuwepo Pemba moja ni wajasiriamali kukosa soko la kuweza kuuza biashara zao. Sasa cha kunishangaza ni kuwa lile soko pale lililowekwa haliuzwi na wajasiriamali, walioko pale ni wafanyabiashara. Kwa sababu wajasiriamali tuliotegemea waweko pale ni wale wanaozalisha biashara zao wenyewe na kuweza kuweka pale, ili kuzionesha au wakaweza kuuza. Lakini leo sasa hivi soko lile kuna hawa wafanyabiashara wanaokwenda kuchukua nguo wakija pale wakiuza.

Sasa Mhe. Waziri, anambie lile soko limebadilika kuwa sasa halikuwa tena soko la wajasiriamali au na wale wanaochukuwa bidhaa kama zile nguo za watoto sijui kanga nao pia wale wajasiriamali? Anipe ufafanuzi kwanza wajasiriamali ni wepi na wafanyabiashara ni wepi, ili tuweze kujua. Kwa sababu mimi ninavyojua wajasiriamali ni wale watu wanaozalisha biashara zao kama za vikundi ndio waliokuwa wakilalamikiwa kuwa hawana masoko.

Katika ukurasa wa 37 Mhe. Waziri alieleza changamoto ambazo moja ni mitaji midogo ya kuanzisha na kuendeleza miradi hiyo ya hao wajasiriamali. Sasa humu kwenye kitabu hatukuona kuwa pengine wajasiriamali hawa kwa sababu sasa hivi kuna maeneo mengi tu ya wanaokopeshwa kama hii Wizara ya Uwezeshaji, lakini kuna mifuko hiyo ya AK na JK. Sasa kwa nini bado tuendelee kuwa tunachangamoto hii ambayo mitaji bado ni midogo.

Naomba Mhe. Waziri akija atupe ufafanuzi hawa hawamo au ndio changamoto moja hii ya mwisho unayosema ni kiwango kikubwa cha riba na kama ni kiwango kikubwa cha riba kwa nini na mifuko ile ya AK na JK imekuja kwa kuendeleza wananchi kiuchumi. Kwa nini mpaka leo basi iweze kuwekwa na riba kubwa ambayo wananchi wasiweze kuichukuwa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache mimi naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

**Mhe. Abdalla Moh'd Ali:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi umenipa ujirani wa Barazani nashukuru kwa hilo na nashukuru kupata fursa adhuhuri hii ya kuzungumza machache katika wizara ambayo inamuhusu kila mmoja wetu. Kupanda bei ya mchele hakuna asietumia, chumvi ikiengezeka bei hakuna asietumia, kwa hiyo, kila mmoja inamuhusu. Mafuta ya kula japo tunakatazwa na madaktari lakini bado tunatumia.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze kidogo katika suala la mambo ya biashara na ukuzaji wa masoko. Idara hii imejitahidi na kwa ripoti hii inatuonesha kwamba imejaribu kuwasaidia vijana wetu wengi sana Wilaya ya Kaskazini "A" pamoja na Wilaya ya Mkoani katika kuwafundisha na kuwapa mafunzo mbali mbali kuhusu biashara, hasa wakitumia huu utaratibu sijui ndio wa Mkurabita.

Hilo hatuna budi kuwapongeza kwamba wamewapa mafunzo kwa vile upungufu wa kazi ni mkubwa katika nchi yetu, wengi wamenufaika na mafunzo haya. Lakini baada ya watu kunufaika, huwa wanatarajia wapate maeneo ya kufanyia biashara na serikali kuanzia awamu hii ya saba iliweka eneo moja na ikaliweka kuwa hili ni eneo kwa vile vijana wengi watapa kujiajiri ile sehemu ya Saateni.

Mhe. Naibu Spika, mengi yamesemwa kuhusu soko lile na imefikia wakati vijana wengi wamekimbia soko lile kutokana na kwamba halijaweka miundo mbinu ya kisasa, ili kufanya kwamba pale iwe ni soko kweli la kileo. Sasa sijui Mhe. Waziri kwa awamu hii ambayo anaimalizia yeye sijui anatuhaidi nini katika soko lile. Kwa sababu hivi sasa ukiangalia miundombinu ya maji haipo, ikinyesha mvua matope matupu. Likitoka jua ni vumbi tupu. Kwa hiyo hatujui hasa lililokusudiwa kwamba wananchi walihamishwa katika maeneo ya Darajani na wakapelekwa katika eneo la Saateni.

Lakini eneo lile hadi hivi sasa ni aibu kwa sababu halijafikia kiwango ambacho wafanyabishara wetu waweze kutulia sehemu ile na kuendeleza biashara zao. Sasa Mhe. Waziri, hebu kidogo tueleze kuna mpango gani kuhusu eneo lile la Saateni ili wafanyabiashara wetu wapate kutulia nafasi zao na kuendeleza biashara zao kama kawaida.

Mhe. Naibu Spika, jengine nililotaka kusema ni kuhusu Shirika letu la Karafuu yaani *ZSTC*. Kwanza mimi nipende kuwapongeza wale wenzetu wa Shirika hili walioko Mkoani kwamba walipoona ipo haja sasa ya kwamba Hospitali yetu ya Abdalla Mzee ndio inajengwa upya wakaona upo umuhimu sasa wa kutoa nafasi kwa ajili ya kukaribisha Hospitali ya Abdalla Mzee kuhamia katika maeneo yao. Hilo ni jambo zuri la uzalendo na kitendo walichokifanya kinastahiki kupigiwa mfano.

Shirika hili la *ZSTC* limefanyiwa mageuzi na baada ya kufanya mageuzi ripoti hii imetwambia kwamba sasa Shirika linaweza kusimama kwa miguu yake kwamba wameweza kupeleka gawio serikalini na wameweza kulipia kodi ya mapato kama walivyopangiwa. Lakini tukiangalia katika changamoto ambazo tumeambiwa huku la shirika hili ni wananchi kuharibu karafuu.

Pia, wananchi hao nafikiria kwamba wanafikia hatua hiyo kwa kujua kwamba kile wanacholipwa katika uuzaji wa karafuu ni kidogo na ripoti pia zinatwambia kwamba kabla ya shirika hili kufanyiwa mageuzi asimilia thamanini ilikuwa inakwenda kwa wananchi na asilimia ishirini ndio iliyokuwa inabakia kwenye shirika.

Sasa shirika ninavyolihisi linakwenda vizuri lakini kwa changamoto hizi tulizoelezwa na Shirika, nahisi hawafaidiki, labda niulize kwamba waziri ile asilimia thamanini ambayo inakwenda kwa mkulima sijui itabakia mpaka lini. Hatuoni kwamba ipo haja hivi sasa ya kuona hawa wakulima wa zao la karafuu ile asilimia thamanini inayobakia kwao tukaiongeza tukafikia asilimia angalau thamanini na tano, ili hizi changamoto zinazotokea kwenye shirika zinazosababishwa na hawa wakulima wa zao la karafuu tukaziondoa na labda kuwapa motisha zaidi wakulima wetu wa karafuu, ili baada ya msimu wa karafuu changamoto kubwa ile iliyopo ya kutorejesha mikopo labda sasa watakuwa na uwezo wa kurejesha ile mikopo.

Sasa sijui serikali imeliona vipi hili kwamba ile asilimia thamanini labda hakuna haja ya kufanya *review* labda na haya mageuzi yetu twende zaidi ili tupunguze mzigo zaidi kwenye shirika na hii faida imfikie moja kwa moja mwananchi baada ya kupitia mikono mingine ambayo labda yeye ameona hainufaishi na labda serikali ikasubiri tu pato lake moja kwa moja kutoka kwa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, jengine katika hii ni kwamba ripoti imetueleza kwamba bei ya karafuu imeshafikia kwa tani dola elfu tisa na hawakutueleza kwamba mauzaji ya karafuu huko nje yanakuwa yako vipi. Kwa maana hapa mauzo ya ndani wametueleza kwamba karafuu zina *grade;* zinakuwa zina *grade* ya kwanza ambayo inanunuliwa kwa shilingi elfu kumi na nne na *grade* ya pili ambayo inanunuliwa kwa elfu kumi na mbili kutoka kwa mkulima na *grade* ya tatu ambayo inanunuliwa kwa shilingi elfu kumi kutoka kwa mkulima.

Sasa huko tunakouza nako kunakuwa na *grade* au hii elfu tisa ni moja kwa moja tu, karafuu yoyote inayokwenda huko inakuwa *grade* yake ni dola elfu tisa kwa maana ya kuwa ikiwa karafuu zote basi zinauzwa kwa bei hiyo basi ipo haja sasa ya kuona kwamba hizi karafuu hii asilimia thamanini basi mwananchi angalau

asilimia tano aongezwe apate asilimia thamanini na tano na shirika libakie na asilimia kumi na tano, ili kuboresha zaidi na kuondosha ule utata kwamba mwananchi lazima akopeshwe ili aendeleze zao hili.

Tutakapofanya hivyo nafikiria sasa shirika changamoto moja itaiondoa ya kuwakopesha wale wananchi wakiwaekea bei ambayo itakuwa ni nzuri. Kila mmoja atafaidika na atakuwa hana haja tena sasa ya kwenda kuuza karafuu akenda akazichanganya na mataka mengine, wala kwenda kwenye shirika akaomba apewe mkopo wa kuendesha zao hili la karafuu.

Nafikiri serikali ingekaa sasa ikaona kwamba sasa ipo haja ya zao hili kuliongeza asilimia wanayonunuwa wananchi, ili serikali ikabaki na asilimia ndogo zaidi, mwanachi akafaidika zaidi na na serikali ikaondokana na kuanza kutoa pesa nyengine za kumkopesha mwananchi kuliendeleza zao hili.

Mhe. Naibu Spika, jengine nililokuwa nataka kusema ni kuhusiana na hii *branding;* ripoti imetueleza hapa kwamba tayari wameshafanya *branding,* lakini pia hili ni jambo zuri na litaitambulisha nchi yetu na litaupa uhakika wa karafuu tulizonazo. Lakini wametutisha kidogo kutwambia kwamba hivi sasa bei hiyo ya karafuu inataka kushuka au inatetereka na kutetereka kwake kunatokana na kwamba Indonesia ambao ni wazalishaji wakubwa wa karafuu hivi sasa tayari wameshaanza kuingiza karafuu katika soko la ulimwengu pamoja na visiwa vya Comoro.

Sasa haya yote tunayoyafanya ya *branding* na kutafuta masoko na kurasimisha watu watasaidiaje ikiwa soko hilo la dunia hivi sasa limeshaanza kutetereka kwa kujaa karafuu za nchi kama hiyo ya Indonesia ambaye ni mzalishaji mkubwa wa zao la karafuu.

Mhe. Spika, labda nimalizie kidogo tu kwamba kwenda katika hii maabara ya taifa, yaani taasisi ya *Zanzibar Bureau of Standard* (*ZBS*). Walichotueleza hapa ni kwamba wanamangamanga mpaka hivi sasa na ninachokijua kwamba sheria ya kuanzisha shirika hili ilipitishwa hapa tokea 2012 au 2013 mwanzo, sina uhakika.

Mhe. Spika, cha kushangaza hadi hivi sasa wanavyotueleza ni kwamba wao katika kufanya vipimo vyao wanadandia dandia mara wende kwenye chakula na vipodozi mara sijui waende Dar-es-Salaam. Sasa sijui kitengo hiki idara au wizara imejipanga vipi ili kukimalizia na kuwa na vipimo vya uhakika vitakavyotuwezesha kufanya tathmini ya bidhaa zetu.

Mhe. Naibu Spika, juu ya hayo nasema kwamba naiunga mkono hotuba hii na nakushukuru. (*Makofi*)

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Hija Hassan Hija na Mhe. Jaku Hashim Ayoub na Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa ujitayarishe.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru sana na naomba nitoe mchango wangu kwa ufupi kwenye Hotuba ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, Wizara ambayo mimi ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Mhe.Naibu Spika, naomba kwanza niseme tu kwamba si kawaida yangu kupongeza Wizara mbali mbali, lakini nimelazimika nifanye hivyo kwa sababu za msingi ambazo Wizara hii zipo. Kwa hivyo, nawaomba wenzangu Wawakilishi wenzangu pale nitakapopongeza, basi waangalie hoja ambayo ninapongezea na waniunge mkono kwa hilo, kwa sababu ukweli siku zote unakuwa haupingiki.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba niwapongeze sana Wizara siyo tu kwa sababu mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, lakini nina sababu ya kuipongeza Wizara hii. Kwa utafiti wangu niliofanya mdogo wa haraka haraka ni Wizara pekee ambayo imetuletea sheria nyingi kwa pamoja kwa mwaka 2010 mpaka 2015.

Hii ni nikiashiria kwamba watendaji wa Wizara hii chini ya Waziri walikuwa wakifanya kazi. Ni Wizara pekee ambayo imeleta sheria nyingi hapa niwakumbushe wenzangu; tumepitisha Sheria ya Karafuu, Sheria ya Biashara na Sheria nyengine. Ni tofauti kabisa na Wizara nyengine ambazo kwa tafsiri yangu mimi baadhi ya Wizara zimekuwa zikila mishahara na fedha za umma bila ya kufanya *kazi. (Makofi*)

Sasa Wizara ambayo imefanya kazi sana, imeleta sheria nyingi kwa maslahi ya taifa na wananchi wake, ninadhani Waheshimiwa Wajumbe hii ndiyo Wizara ambayo tungeipongeza kwa msingi huo. Sasa mimi niwaombe wenzangu kwamba wasisahau sana jinsi ambavyo Wizara hii imetuletea sheria nyingi zenye ufanisi mkubwa kwa wananchi kwa wakati mmoja kwenye kipindi cha miaka mitatu mfululizo ambazo ni sheria ambazo zimegusa sana maslahi ya wananchi wetu bila ya tatizo.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, hiyo ni hoja yangu ya kwanza ya kuipongeza Wizara kwa jinsi ambavyo wamefanya kazi kwa bidii na kwamba kwa muda mfupi tofauti na Wizara nyengine, wametuletea sheria nyingi lakini siyo nyingi ambazo zina ufanisi mkubwa kwa maslahi ya wananchi wetu na nchi yetu kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo ninataka niseme unaweza ukailumu Wizara lakini kwa msingi wa uwajibikaji, kwa maana ya udhaifu wa watendaji au udhaifu wa Wizara yenyewe. Lakini msingi mkubwa wa ulalamikaji wa utendaji kazi ni fedha ambazo zinazopatikana kwenye Wizara husika.

Sasa ninawaomba Mhe. Naibu Spika, niwarejeshe wenzangu kwenye ukurasa wa 60 katika jadweli nambari 6. Hapa ndipo unapopata picha hasa vipi Wizara imewajibika. Je, imefanya vizuri au imefanya vyenginevyo. Fedha ambazo zimeingizwa kwenye Wizara hii kwa mwaka 2014/2015, ni makisio ya mishahara. Hii ninataka niiwache kwa sababu ni mambo ya kawaida, lakini makisio ya bajeti ya mambo mengine au kazi za kawaida ni bilioni moja nukta mbili nne ya maombi ambayo Wizara iliomba hadi kufikia Machi, 2015 wameingiziwa milioni mia nane na kumi sawa na asilimia 65 ya *OC*.

Mhe. Naibu Spika, lakini kazi za maendeleo waliomba hadi bilioni mbili nukta tatu tatu tano hadi kufikia Machi wameingiziwa milioni mia tatu na tatu nukta tano sawa na asilimia 12.9. Sasa unapohoji kiwanda, unapohoji *branding*, unapohoji maendeleo ya Wizara angalia fedha iliyoingizwa. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, Wizara hii ukiachia mishahara ambayo ni haki ya msingi ya mfanyakazi, fedha ya *OC* ni asilimia 65 ni kiasi wastani nzuri, lakini fedha ya maendeleo ambayo ndiyo ingesababisha hivyo viwanda ni asilimia 12.9, huwezi kufikia lengo.

Mhe. Naibu Spika, jumla ya bajeti ya Wizara hii wastani ni bilioni mbili nukta sita sawa asilimia 26.2. Sasa umempa Waziri na Katibu Mkuu bajeti ya asilimia 26.2 kwenye asilimia 100, utegemee *branding* kwa wakati, utegemee viwanda kwa wakati, utegemee ujasiriamali kwa wakati. Kwa hivyo, kuulaumu kwa msingi wa hoja hiyo, kwa msingi wa hoja ya fedha na utendaji wa Wizara ninadhanii hawa tungewapunguzia kidogo makosa. Kwa sababu kwa kweli fedha haikuingizwa ipasavyo, imeingizwa asilimia 26 ya fedha yote ambayo tuidhinitisha mwaka jana.

Huu ninadhani ni wakati wa Wawakilishi sasa kuona kwamba kazi kubwa ambayo wanaifanya ya kuingizia fedha Wizara mbali mbali, Wizara haiingiziwi fedha, sisi ndiyo wa kulaumiwa. Kwa nini kazi inafanyika hapa lakini mwisho wa siku fedha haingizwa na tumekuwa hatuhoji hiyo Serikali, tumekuwa tukiridhika.

Sasa Mhe. Naibu Spika, kwa msingi wa hoja hii ya fedha ya Wizara ninadhani niwatetee na niwaombe wenzangu kwamba waliangalie hilo. Huwezi ukafikia maendeleo kwa asilimia 26 ya bajeti iliyotengwa. Kwa hivyo, tuombe tu mara hii Kaka Mhe. Omar Yussuf Mzee, tukijaaliwa fedha akiipata mapema basi waingiziwe mapema, ili malengo ya Wizara yaweze kwenda, tusiwe tu tukiwasulubu wataalamu na Mawaziri wetu kumbe sababu ni fedha. Pale ambapo kwa utendaji ni dhaifu tuseme wazi wazi kuwa ni udhaifu na hiyo mimi nitakuwa

mstari wa mbele hivyo, lakini kwa msingi wa fedha hapa ninadhani tuwatetee wenzetu kwamba asilimia 26 ya bajeti ya Wizara hii ni fedha ndogo sana.

Wizara iliyopita jana mfano ya Miundombinu na Mawasiliano, wao walipata asilimia zaidi ya 70. Kwa hivyo, unaona kwamba ni tofauti hizi Wizara; moja asilimia 70 na nyengine asilimia 26, huwezi kutenda kazi hiyo.

Mhe. Naibu Spika, hoja nyengine ya mwenendo wa biashara baina ya Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara. Utafiti mdogo nilioufanya, ni kwamba Wizara hii mpaka Mhe. Waziri anakabidhiwa Wizara mwaka 2010 pamoja na watendaji wake, walikuwa wanapeleka bidhaa Tanzania Bara za bilioni 24. Wizara ilikuwa inaratibu bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara za thamani ya bilioni 24, wakati bidhaa kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar ilikuwa ni bilioni 74 na 75. Sasa leo ukiangalia ukurasa 59 kwenye jadweli nambari 2, bidhaa za mwaka ambazo zimeenda Tanzania Bara kutoka Zanzibar ni bilioni 501. Sasa kutoka milioni 24 mwaka 2010 mpaka bilioni 501 mwaka jana, ninadhani Wizara tuipongeze kwamba Wizara imewashawishi wafanyabiashara wa ndani kusafirisha biashara zao kwenda Tanzania Bara kwa bilioni 501 mwaka jana kutoka bilioni 24 za mwaka 2010.

Mhe. Naibu Spika, mwaka huu hadi Machi Wizara inatwambia imesafirisha bidhaa za bilioni 366. Kwa hivyo, ukitoka bilioni 24 za mwaka 2010 mpaka bilioni 366 mpaka Machi, ninadhani Wizara hii inahitaji pongezi.

Nadhani kimahesabu hasa hili jambo lisingezungumzwa sana, kwa sababu inaonekana wazi kwamba bidhaa za Zanzibar kwenda Tanzania Bara ni nyingi kuliko Tanzania Bara kuja Zanzibar na kwa hivyo kibiashara maana yake Zanzibar tumefanya biashara kubwa ya kupeleka Tanzania Bara. (*Makofi*)

Ninajua Mhe. Naibu Spika, ni bidhaa nyingi za magari zimeongeza thamani hii ya fedha. Sasa hoja ni changamoto ya ushuru wa Tanzania Bara wa *double taxation* ni hoja nyengine ambayo ni Wizara ya Fedha, ambayo tutaizungumza kuanzia kesho. Lakini ninadhani Wizara hii tuipongeze kwa hilo na mimi naomba wenzangu kwamba tusiwasulubu kwa msingi huo, tuwapongeze kwamba bidhaa zimepanda na mapato yameongezeka kutoka bilioni 24 mwaka 2010 hadi bilioni 366 mpaka Machi, 2015.

Mhe. Naibu Spika, hoja nyengine ambayo ninataka niizungumze ni jadweli *number one* uingizaji wa mafuta. Ukiangalia uingizwaji wa mafuta mwaka 2012 mpaka 2014, unaona kuna tofauti ya mafuta yanayoingia na viwango vyake. Kwa mfano mafuta ya *jet* kwa mwaka 2012 yalikuwa na thamani ya bilioni 16; ninadhani bilioni 16 lakini mwaka 2013 ni bilioni 11. Kwa nini imeshuka. Wenyewe watajibu

lakini ninadhani ni kwa sababu ya ushuru. Unapokuwa na ushuru mkubwa wa mafuta, maana yake kasi ya uingiaji mafuta Zanzibar inapungua. Hivi ndivyo kigenzo ambacho ningeomba Mhe. Waziri wa Fedha, akione kwamba kadri unavyoweka ushuru mkubwa, maana yake unapunguza mapato ya nchi, unawasababisha wafanyabiashara kukimbia uingizaji wa biashara wa ndani.

Nadhani ni eneo ambalo Wizara ya Fedha ingeliangalia kupunguza ushuru ili kuwavutia wafanyabiashara mbali mbali kuleta bidhaa Zanzibar ili kuongeza kasi ya maendeleo kwa kodi ndogo lakini ambayo inaingia kwa wastani wa haraka haraka kiasi hicho.

Mhe. Naibu Spika, baada ya takwimu hizo za ufafanuzi ambazo ningeomba wenzangu waziangalie na tusiwasulubu wenzetu kwa hoja hiyo. Sasa niende kwenye hoja ya viwanda kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, hoja ya viwanda kwa ujumla, imeoneshwa hapa jadweli nambari sita kwamba fedha ile ambayo ilitengwa kwa ajili ya mambo hayo ya maendeleo, ikiwemo viwanda, na *ZBS* na mambo mengine ni fedha ndogo sana; ni asilimia 12.9. Kwa hivyo, huwezi ukamlaumu Waziri na watendaji wake kwa sababu hatukuwapa fedha, bila fedha hakuna kiwanda.

Mhe. Naibu Spika, wakati mwengine sisi wenyewe ni tatizo. Mimi niwakumbushe Wawakilishi wenzangu mwaka juzi hapa, yupo mwekezaji mmoja alikuja na wazo la kuwekeza Kiwanda cha Saruji, ninadhani Mhe. Turky, lakini kwa sababu ya sera na sisi wenyewe hatupo makini, huyu jamaa alishindwa kuwekeza, walisingizia vikwazo chungu nzima. Hatimae tukamkimbiza hapa, sasa hivi yupo Kisarawe.

Kwa hivyo, vikwazo ambavyo havina sababu na havina msingi wowote vinamfanya mfanyabiashara mwenye fedha yake akiimbie maeneo. Lazima yaandaliwe mazingira mazuri na salama ya wafanyabiashara ndiyo wawekeze. Kwa hivyo siyo kosa la Wizara *in such,* lakini ni kosa la sera na usimamizi wetu na hili ni kosa la Wawakilishi kwamba hatupo makini katika kusimamia mipango na sera za Serikali.

Mawaziri wanatushawishi kwa hoja nyepesi na tunaridhia hatimae wafanyabiashara wanaondoka, fedha za ndani zinaondoka kiasi hicho. Leo mfanyabiashara yule amewekeza Kisarawe, mapato yanaingia Tanzania Bara, baadae unamlaumu wakati wewe ulikuwa sehemu ya kumkandamiza mfanyabiashara yule akimbie. Leo unamlaumu Waziri kwamba hakuweka viwanda. Lazima tuwe makini na tusimamie maendeleo ya nchi kwa kusimamia sera za nchi za mapato na matumizi ya Serikali.

Mhe. Naibu Spika, mfano mwengine tuangalie Kiwanda cha Sukari. Ni sisi wenyewe ambao tumeamua kumpa mwekezaji Kiwanda cha Sukari, lakini Serikali imeshindwa kumkabidhi nyumba zake. Serikali imeshindwa kumkabidhi mashamba. Mashamba mengine wamepewa Vikosi bila ya sababu. Kwa hivyo, unalaumu Wizara wakati Wizara unainyang'anya nguvu za kusimamia mambo. Kwa hivyo, unampa mtu dhamana, umpe dhamana yote, unamwambia asimamie Kiwanda cha Sukari lakini nyumba hujamkabidhi mwekezaji, mashamba unampokonya. Kwa hivyo, unamfanyia mambo mengi ambayo yanavunja moyo, hatimae yule ataondoka mutailaumu Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ni Wizara ambayo kwa kweli ingehitaji kuwashawishi wafanyabiashara kwa kasi hiyo.

Mhe. Naibu Spika, mimi niwaombe wenzangu kwamba sera ya uchumi iwe uchumi na Sera ya Siasa iwe siasa. Huwezi kuingiza siasa kwenye uchumi ukasema unakwenda mbele, lazima siasa isimamie uchumi na siyo uchumi usimamie siasa. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, hoja nyengine ambayo ninataka nichangie ni hoja ya karafuu. Mimi ninadhani niwe muwazi kwamba kama kuna wakati wa kulipongeza Shirika la *ZSTC* ni wakati huu wa 2010 hadi 2015. Mimi binafsi ninampongeza sana Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la *ZSTC* kwa jinsi ambavyo anafanya kazi. Miongoni mwa sheria ambazo amezileta hapa ni Mfuko wa Karafuu. Niwakumbushe wenzangu kwamba Mfuko wa Karafuu huu, Wawakilishi waliingiza kifungu kamili cha kuwalinda wanaoanguka mikarafuu kwa kuweka Bima ya wachumaji wa karafuu. Hilo limetekelezwa na lipo na linasimamiwa.

Sasa ni wajibu wetu kuwaelimisha wananchi wetu kwamba Mfuko wa Karafuu kuna kifungu cha Bima wanaoanguka mikarafuu waende kule kujiorodhesha na Sheria ile ya Biashara ninadhani limeweka daftari la kusajili wafanyabiashara mbali mbali, ili kwa malengo hayo ya kuwahifadhi watu wetu wanapoanguka na kupata madhara mengine.

Kwa hivyo, mimi ninadhani Mhe. Naibu Spika, tumpongeze sana Mkurugenzi wa Shirika la *ZSTC* kwa jinsi ambavyo *ZSTC* ameikuza. Mimi ninadhani nimekuwa safarini na wenzangu kwenda Dubai, tumeona Dubai kwamba karafuu ya Zanzibar inahitajika sana. Maana yake unafika Dubai pale unahitaji gunia moja la karafuu la Zanzibar hakuna. Kwa hivyo, uzalishaji uongezwe ili mapato ya karafuu yaweze kuongezeka. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ninasema hivyo kwa sababu nimeona mwenyewe kwamba karafuu inahitajika sana, licha ya kuongezeka kwa wazalishaji wa Indonesia, lakini

bado karafuu ya Zanzibar ina viwango, lazima tusimamie karafuu yetu. Lazima tuboreshe karafuu yetu na tuliwezeshe Shirika hili, ili liweze kusimamia karafuu hizo kwa ujasiri mkubwa sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, na hapa nichukue nafasi kuwaomba wananchi wenzangu kwamba ujanja wa kuuza karafuu hausadii, kwamba huwezi ukachanganya karafuu na makonyo, ukachanganya karafuu na mchanga baadae ukataka *branding*; *branding* hiyo, lazima tuweke karafuu safi ili *branding* ifanyike kwa viwango vinavyohitajika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ninadhani mimi niwaambie wenzangu tu kwamba Mfuko huu wa Karafuu ndiyo mkombozi wa wananchi wetu wa Zanzibar. Shirika hili chini ya mwana mama yule kwa kweli amelipeleka pahali pakubwa sana, amefanya bidii kubwa kupunguza wafanyakazi. Leo Shirika linakwenda kwa faida, linakwenda kwa viwango. Ninatumia lugha hapa kwamba kila shilingi mia ya karafuu, shilingi thamanini inaenda kwa mkulima mwenyewe. Sasa kama hatujaweza wakulima wetu kuwaelimisha, kwa mfano mwaka jana ninadhani kama sikosei Mhe. Waziri, atanisaidia, karafuu imetozwa bilioni 70, lakini wafanyabiashara wengi bilioni 70 kwa macho faida hatuzioni.

Ninadhani tuwahamasishe wakulima wetu wakaweza Benki ya Wakulima wao wenyewe kwa bilioni 70, ninadhani benki inaanzishwa kwa bilioni 15 unaweza ukaanzisha, lakini karafuu peke yake imezalisha bilioni 70, zipo wapi.

Sasa Mhe. Naibu Spika, tuwapongeze sana watu wa karafuu kwa jinsi ambavyo wamesaidia kuimarisha mapato ya wakulima wetu na mikarafuu kwa jumla. Kosa moja ambalo lipo ni kosa la utafiti wa mikarafuu. Ni kweli Kamati yangu imeshuhudia kwamba Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Kizimbani imeshindwa kufanya utafiti wa mikarafuu na hii ambayo Mhe. Saleh, amezungumza juu ya kupata mbegu mpya ni kosa la Taasisi ya Kilimo chini ya Wizara ya Kilimo. Sasa ninadhani huu Mfuko uangalie kuwasaidia na kuwakumbusha kwamba ni jambo ambalo tushirikiane kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko na Taasisi ya Kizimbani tuweze kuwapatia utafiti wa kina.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo mimi niwaombe wenzangu chonde chonde sana, hakuna Wizara ambayo tungeipa nafasi ya kwanza au ya pili kama si Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa utendaji. Ninasema hivyo nikiwa na msingi wa hoja na nitasema hivyo nikiwa na msingi wa hoja kwa Wizara ya Fedha, nitasema hivyo kwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na sikusema haya kwa Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa sababu ninaona kuna mambo ambayo si mazuri. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, naomba wenzangu tuunge mkono hii. (*Makofi*)

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Hija Hassan Hija kwa mchango wako mzuri. Sasa tunampa nafasi Mhe. Jaku Hashim Ayoub, baadae Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa na kama muda utakuwepo Mhe. Panya Ali Abdalla.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi mwanzo kabla ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu *Allah Subuna Wataala* aliyeniwezesha kuwa hai hii leo kuishuhudia Ramadhani ya kwanza na kuweza kuifunga.

Pia, nichukue fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa umakini wako wa hali ya juu, hekma na busara unapoendesha kikao kwa ufundi na ustadi wa hali juu. Nikushukuru sana.

Vile vile, nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa umakini, kama alivyotangulia kusema Mwenyekiti wangu Mhe. Hija Hassan Hija, ni miongoni mwa Kamati ya Biashara, Fedha na Kilimo. Mashirikiano makubwa wametupa wakati wa kipindi cha miaka miwili na nusu mpaka tunamaliza, tumeona utendaji wao, ni ukweli usiofichika chini ya Kamanda Mhe.Waziri.

Mhe. Naibu Spika, hii bajeti imekuja wakati sijui tuseme muafaka au mbaya kwa wananchi, maana yake ndiyo Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko huku wananchi tukiona wanaendelea kuumia kwa ukali wa maisha. Sizungumzi kwa kubahatisha, ninazungumza na mifano nitaitoa lakini sijui huyu paka wa uso tutamtupia nani.

Mhe. Naibu Spika, mwezi huu leo ndiyo Ramadhani Mosi, tunaita Kumi la Rehma, tukitoka hapo tunaingia Maghfira na la mwisho kusalimika na kuachiwa huru na moto; ndiyo ya mwisho.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, niikosoe Kamati yangu maana yake ilipoeleza taarifa zinaonesha kwamba mwenendo wa bei za bidhaa muhimu hapa nchini unaendelea kuwa na utulivu kwa takriban kipindi cha mwaka 2014/2015.

Aidha, ni jambo la faraja kuona kuwa hali ya upatikanaji wa chakula muhimu; mchele, sukari na unga ngano inaendelea kuwa nzuri kwa kipindi kirefu sasa. Pamoja na hali hiyo Kamati imeitaka Wizara kufanya utafiti juu ya hali iliyojitokeza hivi karibuni kuwepo kwa utofauti mkubwa kwa bei za Unguja na Pemba, kwa bei za Pemba kuuzwa kwa bei ya juu kuliko Zanzibar, hili swali ni kweli. Lakini ilikuwa aieleze na Zanzibar hivi sasa mchele sukari na unga wa

ngano, dawa ya mbu; vitu vyote vimepanda. Hivyo havihitaji tochi wala kama ule uwacho wa mwenge unasuka makuti makavu ukawasha, hivi vitu vimepanda na vinamuumiza nani.

Mhe. Naibu Spika, vinamuumiza mwananchi wa chini, kupanda kwa vitu hivi kwa mwezi huu mtukufu wa Ramadhani na nini chanzo chake. Mhe. Waziri kaeleza humu katika kitabu chake, hotuba ya Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko.

Hata hivyo, katika kipindi cha mwezi wa Mei, 2015 kujitokeza upandaji wa bidhaa muhimu za chakula kulikosababishwa na kupanda kwa thamani ya dola za Kimarekani ambayo ilichangiwa na kushuka kwa shilingi ya Tanzania. Mimi nafikiri sasa imefika wakati labda tuishauri serikali wakakae Marais wawili. Tuchukuwe mfano wa Zimbambwe kutumia dola kwa dola, mfano huu upo Zimbambwe.

Mhe. Naibu Spika, kila siku shilingi inaporomoka kwa shilingi 600, 700 au 800 mtaji wa mwananchi unakufa. Kwa hivyo, *total* kitu anachokwenda kununua ni lazima apandishe bei tu hakuna ujanja wowote, lakini mwisho wa siku anayeumia ni mwananchi, badala ya kupata milo mitatu kwa siku mwisho atakula mmoja, kama hivi ilivyo mwezi wa Ramadhani. Kwa hapa serikali ijipange na iliangalie suala hili anazidi kuumia mwananchi. Kodi kila siku na kila leo zinapanda anayekamuliwa ni mwananchi. Leo pengine mzee ana watoto wake sita na ana wake wawili, itakuwa mtihani. Kwa hivyo, serikali iliangalie.

Mhe. Naibu Spika, lakini isiwe kisingizio cha dola tu kupanda. Kuna mifano hai hapo nyuma tofauti, soko unalokwenda kununua vifaa vile vile kama Dubai au China duka ni lile lile moja na bei ni ile ile moja, *rate* ya dola hapa Tanzania iko bei ile ile, ushuru ni ule ule. Mhe. Waziri nisikilize kwa makini hapa.

Katoka hapa mtu kenda kununua bidhaa Dubai, kenda China, kenda Uturuki thamani ya dola bei ile ile, kama 1,650 anakwenda kununua kitu kile kile na Mhe. Hija Hassan anakwenda kununua kitu kile, bei ile ile na ushuru tunalipa ule ule.

Ni sababu gani inasababisha maduka kuwa bei tofauti, yapo haya. Hapa wizara kidogo mkae mliangalie kwa makini na hili nitahitaji maelezo, ili nipate kutoa baraka kupitisha bajeti hii, ni vitu ambavyo viko totauti, bidhaa ile ile lakini maduka tofauti kuuzwa. Kwa hivyo, kuwe na utaratibu maalum wa bidhaa kuuzwa. Nafikiri mfano hai upo Mhe. Waziri uende ukayaone mambo kama haya maduka karibu yote unakuta bei yote moja inakuwa *stable*.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo niombe kidogo Mhe. Haji Omar Kheir, leo hayupo, imetangulia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, mwezi mtukufu wa

Ramadhani umeanza kama tunavyojua ajira zimekuwa ngumu; vijana wetu wanazidi kuumia, Baraza la Mji juzi nilishuhudia mimi na Mhe. Abdalla hayupo hapa, Ofisi ya Baraza la Wawakilishi la zamani wamechukuliwa watu vyombo vyao vya *plastic* kwenye gari, mtu pengine anataraji kuuza chombo kile pengine kisitoke na hakijui kimekwenda wapi.

Kwa hivyo, nafikiri mawaziri wawili nyinyi mkae na wa vikosi vya SMZ na wewe kwa hali hii mtu mwisho wake atakwenda kuiba. Mkae mfikiri ajira zenyewe ziko wapi. Leo mtu anapanga vitu vyake kama nyanya zake au tungule, mabiringani mtu unakwenda kuchukua, ni kitu cha aibu. Kwa hivyo, hilo nalo mwezi huu mtukufu mkae mzingatie na kulifikira.

Mhe. Naibu Spika, nije na kumuomba Mhe. Waziri wa Fedha, ambaye yupo, ingawa hili ni suala la biashara vile vile wizara zinakutana. Kuna huu msamaha wa kodi ya mchele, unga wa ngano na tende. Mimi ningemuomba waziri na waziri wangu, mimi naamini ni msikivu sana miongoni mwa mawaziri wa Rais Dkt. Ali Mohammed Shein, Waziri wa Fedha, hilo siwezi kuficha popote nitamzungumza. Kuwa huu msamaha uendelee mpaka mwezi wa Ramadhani, umalize mwezi wa Ramadhani huu msamaha angalau kujaribu.

Narudia tena kwa mara ya tatu kujaribu kupunguza ukali wa maisha. Kwa hivyo, msamaha huu uendelee mpaka uishe mwezi wa Ramadhani huu, ili wananchi wajaribu kupunguza ukali wa maisha kwa sukari. Hapana, samahani sio sukari. Tende, unga wa ngano na mchele. Mhe. Waziri hili liangalieni hali kweli hairidhishi. Kwa hivyo, nafikiri Mhe. Waziri wa Fedha kwa umakini wake na anavyomuamini Mhe. Rais, nafikiri hakuna tatizo.

Mhe. Naibu Spika, tuje kwenye ukurasa wa 9 kwa upande wa zao la mwani, bei katika soko la dunia imekuwa katika *USD*. 0.5 hadi 2.5 dola kilo moja kwa soko la dunia. Aidha, bei ya zao hilo katika soko la ndani imekuwa ikiuzwa kwa shilingi 455/-. Nimshukuru Mhe. Waziri kwa kuzungumza ukweli kwenye kitabu. Lakini tuangalie dola 2. 5 ni shilingi ngapi kwa thamani ya sasa hivi, ni karibu shilingi 5,000/- kwa kilo. Mwananchi mnyonge ana neemeka nini na shilingi 450/- hizi na baya zaidi lililotokea mwani mwingi umeharibika.

Sijui kuna elimu gani inaweza kutolewa au kuna dawa gani ya ku-*treat* mwani ule. Watu wameumia sana kwa kipando cha mwani vibaya mno, mwani umeharibika na mateso yake ni makubwa na kwa bei hii ya shilingi 450/-. Mimi nafikiri Mhe. Waziri kwa jitihada zako na ninavyo kuamini mimi katika waziri wa mwanzo uliyepandisha bei ya karafuu, haki yako upewe kwa jitihada ulizofanya, nikupongeze kwa dhati kabisa.

Mhe. Naibu Spika, suala hili nafikiri Mhe. Rais keshatoa agizo, nafikiri hii ni mara yangu ya nne kuhimiza humu ndani katika kikao hiki, nimeambiwa wizara nne mkae. Ikae Wizara ya Fedha, Wizara ya Kilimo na Maliasili, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko nafikiri na Wizara ya Afya kama sikosei na kama nitakosea mnaweza kunikosoa, lakini hakuna hatua yoyote mpaka muda huu iliyochukuliwa, wananchi wanazidi kuumia na hawana biashara nyengine ya kufanya.

Kwa hili nafikiri kama ulivyofanya kwenye karafuu na umesema katika kitabu chako kwamba mwani umesafirishwa kwa wingi, kwa maana hiyo *total* hiki kitu kinataka kupanda bei, kwa hivyo kina-*demand* kinatakiwa. Kwa hivyo, hili nalo liangalieni angalau wananchi waepuke na mashaka haya.

Mhe. Naibu Spika, jengine nimpongeze Mhe. Waziri katika huu huu ukurasa wa 10, kutoka ukurasa wa 9, 10. Kuandaa mpango wa kuanzisha mitaala ya ujasiriamali katika maskuli. Hiki ni kitu cha kupigiwa mfano Mhe. Waziri nikupongeze kwa dhati, nafikiri ni mitaala unapeleka skuli. Ni somo la biashara nilivyofahamu mimi kwa haraka ni kitu cha kupigiwa mfano, ni umakini uliouonesha Mhe. Waziri.

Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, nafikiri nimalizie na kama Wajumbe wenzangu walivyozungumza kuhusu *tender* mliyoitoa katika duka la viyoo Mhe. Waziri. Kwanza nichukuwe fursa hii kumpongeza katibu, siwezi kuliwekea *interest* mheshimiwa. Nichukuwe fursa hii kumpongeza Katibu Mkuu wa Wizara hii na vyenginevyo vyovyote ingekuja kuonekana kafanya sivyo, lakini kaweka kitu wazi kabisa. Katangaza *tender,* ingawa kuna mheshimiwa mmoja hapa kaniambia nimefanya, ni-*declare interest.* Hii *tender* ilitangazwa, hata yeye anaweza akaenda akajaza, hata mtu yeyote angekwenda kujaza, mtu yeyote anaweza kwenda ni huru. Haikufichwa iko wazi, yaani mtu yeyote ana uhuru.

Mhe. Naibu Spika, ilitangazwa mwaliko wa zabuni, ukodishwaji wa jengo la duka la viyoo liliopo Darajani. Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inakusudia kukodisha jengo lake liliopo Darajani Unguja, ambalo lina sehemu mbili. Jengo hilo kubwa *square metre* 177 na hivi sasa moja inatumiwa na ushirika wa sonara na ya pili inatumiwa na kampuni ya vodacom duka la viyoo, inayomaliza mkataba Juni hii ndio mwisho inamaliza. Hilo la mwanzo.

La pili, lengo la wizara kulijenga upya duka hilo na kulifanya liwe la ghorofa, ni jambo zuri na la kupongezwa. Anayetaka kukodishwa sharti akubali kushiriki katika kufanikisha ujenzi unaokusudiwa na kufuata michoro maalum itakayotayarishwa na wizara, pamoja na maelekezo mengine yatakayotolewa na ujenzi huo.

Tatu, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inawaalika wazabuni wote wanaopenda kukodi na kushiriki katika ujenzi wa jengo hilo uliopo Darajani Zanzibar, kuwasilisha maombi yao.

Nne, zabuni itafanyika kwa utaratibu wa *quotation*, kama unavyofafanuliwa katika sheria ya manunuzi au mauzaji ya mali ya umma namba 9 ya 15 pamoja na kanuni zake.

Tano, jengo hilo linaweza kukaguliwa Darajani kuanzia tarehe ya tangazo hili katika nyakati za kazi kuanzia saa 2:00 asubuhi mpaka saa 8:00 mchana, mtu anayetaka kukagua jengo hilo lazima apate ruksa ya kufanya hivyo kupitia kwa katibu wa bodi ya *tender* ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Mkutano kwa ajili ya ufunguzi utafanyika tarehe 30 Machi, saa 8:00 mchana katika ukumbi wa mikutano ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Sita, mzabuni yeyote anayehitaji maelezo zaidi kuhusiana na zabuni hizo anaweza kufika Ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, Malindi Zanzibar kuanzia saa 1:30 mpaka saa 9:30 mchana siku ya Jumatatu.

Saba, maombi yote yanafungwa. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, hii ni *tender* imetangazwa iko wazi, vyengine vyovyote katibu angetafuta mtu kumpa, nafikiri angepata mtihani mkubwa. Katibu nikupongeze kwa hili, lakini vyengine vyovyote katibu ungekuja kuwa katika mtihani mkubwa, ungeonekana umempa mtu kwa upendeleo.

Kwa hivyo, mimi nimuombe Mhe. Waziri nafikiri muda anao kabla ya kupitia bajeti, waliojaza wakafunguwe waliobahatika kupata ndio kabahatika riziki yake. Ni jambo zuri, duka lile liko chini na niliwahi kumuuliza Mhe. Waziri katika kamati, lakini sababu yake ya msingi aliyonipa mimi haikulingana. Tulikuwa kwenye kamati, nikamwambia mtu anataka kujitolea kujenga duka kama lile. Akajakuniambia kuna ramani maalum pale. Ukanda ule sio, nafikiri yeye anaingia BLM, mimi siingii. Lakini barabara ya kwenda Mchangani kuanzia pale kwenda mbele, sio kule. Kule tayari kumeshajengwa.

Kwa hivyo, hoja hii ya Mhe. Waziri ni waziri makini, hapa palipobaki tena. Kuna msemo unasema "mgema akisifiwa tembo hutia maji". Mhe. Waziri nafikiri hapa usijekujivunjia heshima yako, kazifunguwe *tender*, aliyeweza kubahatika ndio riziki yake na maliiliyobaki ya serikali ni lile duka tu. Hakuna sababu, watu wameshajaza karibu watu sita sijui saba, zikafunguliwe *tender* zile hakuna sababu ya msingi kuweka.

Ingekuwa Katibu Mkuu katoka tu kenda kumpa mtu mwengine, hakufanya hivyo, lakini Mwenyezi Mungu kamlinda katibu. Si inajengwa mali ya serikali kuna ubaya gani, au imekuwa kama nyoka wa mdimu. Nyoka wa mdimu alisema Mhe. Hamza Hassan pia, hukaa kwenye mdimu yeye hana kazi nazo ndimu, ukenda kuzichuma atakurukia. Kitu kizuri kinataka kuleta maendeleo kwa wawekezaji wakizalendo, kwani tunafanya nini.

Mhe. Waziri, nikushukuru, isije kufika hapa ikaja kuwa aah! kama ilivyosera yenu, haki sawa kwa wote. Mimi nafikiri mkae mliangalie kama haki sawa kwa wote basi fungua, wewe ni Naibu Katibu Mkuu wa Chama wasije wakakuathiri watu. Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, naomba uniruhusu nikae chini.

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa ya kuweza kuchangia mawili matatu katika kitabu chetu hiki cha bajeti, cha Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijaingia katika kitabu hiki, kwanza nichukuwe nafasi hii kumpongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, lakini pia akiwa ni Makamu Mwenyekiti, wa Chama cha Mapinduzi Taifa kwa upande wa Zanzibar kwa kwenda kuchukua fomu siku hii ya leo, katika kugombea nafasi ya Urais wa Zanzibar. Tunamuambia tu kwamba tunampongeza sana na tuko naye bega kwa bega mpaka kuhakikisha kwamba anashinda katika kinyang'anyiro hiki cha Urais wa Zanzibar kwa mara nyengine tena. *(Makofi)*

Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, sasa niende katika wizara hii ambapo pia nawapongeza sana Mhe. Waziri katika wizara hii, pia akisaidiana na mwanamama shupavu, makini na asiyeyumba ndugu yangu Mhe. Thuwaybah Edington Kisasi ambaye anamsaidia Mhe. Waziri kwa karibu sana. *(Makofi)*

Pia, niwashukuru kaka yangu Julian Raphael Katibu Mkuu wa Wizara hii, pamoja na watendaji wote katika wizara hii, kwa kazi kubwa, makini na mahiri ambayo wanaendelea kuifanya katika wizara hii katika kumsaidia Mhe. Waziri kutimiza utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi katika Zanzibar yetu.

Mhe. Naibu Spika, nikimaliza hapo sasa naingia katika kitabu chetu hiki, nakuja katika maeneo yale ambayo yanazungumzia suala zima la upatikanaji wa mikopo katika Shirika letu hili la *ZSTC*.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri atakapokuja hapa nianze kwa kumuomba anisaidie ule utaratibu wa kuwakopesha watu fedha katika wizara yake, bado upo unaendelea na kama unaendelea, hadi sasa hivi unakwendaje. Unakwenda katika

utaratibu wa mafanikio, au unakwenda katika utaratibu wa kusuasua na kama kuna watu ambao wanabahatika kupata fedha hizi.

Je, kuna fedha yoyote ambayo bado iko nje inahitajika kurejeshwa, au wale ambao walikuwa wamepewa mikopo hii tayari wamekwisharejesha. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, atakapokuja hapa anisaidie katika eneo hilo.

Mhe. Naibu Spika, pia katika changamoto ambazo zinafahamika katika suala zima la karafuu katika nchi yetu, bado kuna taratibu hizi za magendo ya karafuu. Je, Mhe. Waziri sijui kwa sasa suala hili la magendo ya karafuu tumefanikiwa kwa kiasi gani katika taasisi yako hii na kwa nchi yetu, kutokana na wimbi ambalo hapo mwanzoni tulianza nalo na lilikuwa ni la kutisha mno.

Vile vile, Mhe. Waziri, utakapokuja hapa naomba unisaidie wizara yako imejipangaje katika utaratibu mzima wa uchanganyaji wa karafuu na makonyo, kitu ambacho kinapoteza hadhi ya soko la karafuu zetu zinapopelekwa nje kwa ajili ya mauzo. Kwa hivyo, ningeomba kufahamu Mhe. Waziri umejipangaje na timu yako katika hilo.

Mhe. Naibu Spika, pia ningependa kufahamu udanganyifu unaoendelezwa na baadhi ya watu kupita katika majumba na kudai kwamba wametumwa na Shirika la *ZSTC*, katika suala zima la kununua karafuu, wakati zao hili linanunuliwa na Serikali Kuu na mipango iko wazi na matangazo kila siku ya Mungu huwa yanatolewa, ili watu waweze kuelewa utaratibu wa serikali katika suala zima la kununua hizi karafuu.

Nikiondoka hapo Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa vile vile anisaidie. Katika maelezo yake humu alizungumzia suala zima la kuwasaidia hawa wajasiriamali. Ninavyofaham

Sasa je, wizara yako imefikia hatua gani katika kuhakikisha kwamba suala hili linamalizika na hatimae wizara iweze kufanya yale malengo ambayo ilikuwa imejipangia kuhusiana na chombo hiki ambacho bado tuna tatizo katika eneo hili.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ningeomba pia kufahamu mipango ya wizara na serikali juu ya suala zima la zao hili la karafuu, ambalo kwa namna moja au nyengine imeonekana kuwa ni zao ambalo linatumia pato kubwa kubwa sana la taifa, sio chini ya bilioni zaidi ya 70 zinatumika katika nchi kwa ajili ya ununuzi wa zao hili.

Je, serikali kuna *income* yoyote ambayo inapata kutokana na mauzo haya ya karafuu hizi, au kama hakuna. Je, serikali imejipangaje katika kuhakikisha kwamba

mbali ya wananchi wanaoneemeka na zao hili, lakini na serikali vile vile katika kutatua matatizo ambayo yanaikabili kwa mambo yetu na yale makusanyo yetu ambayo tunatarajia kuyapata ndani. Wizara yako imejipangaje katika hili, ili tufahamu kwamba na serikali inapata nini katika zao hili ambalo inakusanya pato kubwa sana au inatumia pato kubwa sana ya matumzi yetu.

Vile vile, Mhe. Naibu Spika, nikiangalia katika programu yako ndogo ya viwango na udhibiti bora, kuna suala letu hili la viwango la *TBS*. Hebu Mhe. Waziri utakapokuja hapa unisaidie, kwa sababu mwaka 2011 tulipitisha sheria hapa namba moja, katika suala zima la taasisi hii ya kuangalia ubora kwa bidhaa zetu.

Je, pamoja na sheria ile wizara yako mpaka sasa hivi inawajibika kwa kiasi gani katika suala zima la kuangalia viwango kwa upande wa Zanzibar. Kwa sababu bado naona badala ya kutumia taasisi yetu ambayo tayari sheria yetu tumeshaipitisha na jengo tumekwenda kulikagua, lakini bado naona tunaendelea kutumia taasisi ya *TBS* katika kupata tathmini ya vitu hivi, au thamani ya vitu hivi ambavyo tunakuwa tunavihitajia. Ningekuomba Mhe. Waziri utakapokuja hapa unisaidie ili niweze kufahamu ni namna gani mnatumia taasisi ile katika kuhakikisha kwamba tunafanikisha yale mambo ambayo tulikuwa tumejiwekea na kujipangia kwa mustakbali wa kuhakikisha kwamba Zanzibar yetu inaendelea vizuri.

Mhe. Naibu Spika, jengine pamoja na jitihada na juhudi zote zinazoendelea katika kuhakikisha kwamba uhaulishaji wa mizigo baina ya Tanzania Bara na Zanzibar zinafanikiwa na kuona kwamba mizigo ile inakwenda bila ya usumbufu wa aina yoyote, ningelimuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa kwa sasa atuelezee ni hatua gani tuliyonayo au mikakati gani iliyopangwa katika Wizara yake kuhakikisha kwamba wafanya biashara wanaoendelea kupeleka mizigo yao upande wa pili wa Muungano hawasumbuliwi na bidhaa zao zinakwenda kule pamoja na kutoka, pasi na kuwepo na mambo mengine mengine yanayosababisha usumbufu wa wafanya biashara wa Zanzibar.

Hususan ukiangalia nilipokuwa nikiangalia bajeti ya mara hii ya mwaka 2015/16 nilipokuwa ninamsikiliza Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alizungumza katika Bunge kule kwamba katika suala la kuhaulisha mizigo hii ya upande wa Zanzibar na Tanzania Bara Waziri wetu wa fedha wa Zanzibar na Waziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuna mambo ya msingi walikubaliana katika kuhakikisha kwamba uwezekano wa kuwa malipo ya bidhaa pamoja na uhaulishaji wa mizigo kutoka eneo moja kwenda eneo jengine, umepatiwa ufumbuzi na kuona kwamba tatizo lile halitotokezea tena katika visiwa vyetu vya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Baada ya maelezo hayo sasa kwa sababu wenzangu wengi wamekwisha kuchangia katika bajeti ya Wizara hii, mimi kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni na kwa niaba ya Wananchi wote wa Zanzibar nimalizie kwa kuwatakia Ramadhani Mubarak, Ramadhan njema na Mwenyezi Mungu akubali Ramadhani zetu tutakazozifunga pamoja na ibada zetu tunazozidi kuzifanya katika mwezi huu wa Ramadhani. Baada ya hapo naunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote na mimi nichukue fursa hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *subhana wataala* ambae ameweza kutuamsha katika mchana wa kwanza wa Ramadhani, tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa hilo, na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atuwezeshe kutupa afya, tuweze kuifunga Ramadhani hii kwa salama na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atulipe yale mema yote ambayo ametupangia katika mwezi huu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nichukue fursa hii kukushukuru wewe kunipa na mimi nafasi niseme machache katika Wizara hii, pamoja na hayo naomba kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri wa Biashara na naibu wake na watendaji wao wote kwa kazi nzuri, na mashirikiano mazuri ambayo wameweza kufanya ili Wizara hii iendelee na majukumu yake vizuri.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze ukurasa wa saba (7) ambapo unaeleza hali ya masoko; kitabu hiki kinaeleza Zanzibar imekuwa inafanya biashara na nchi mbali mbali zikiwemo zile za kikanda na za kimataifa. Mimi naomba niulize katika nchi hizi labda ni biashara gani Zanzibar ambayo inapeleka au ni bidhaa gani ambazo sisi Wazanzibari tunapeleka katika nchi hizi na kipato gani ambacho tumeweza kunufaika nacho.

Mhe. Naibu Spika, niende katika ukurasa wa 12 kwenye Maendeleo ya Viwanda; Mheshimiwa kaeleza vizuri katika kitabu chake hiki ambacho kinaeleza jinsi viwanda vilivyoongezeka na pato lile ambalo linaonekana hapa kuongezeka kwa Tanzania Shs. 128.9 bilioni. Hii ni sawa na ongezeko la nukta 5.5.

Mheshimiwa, ni kweli ongezeko hili hapa linaonekana ikiwemo hivi viwanda ambavyo Mheshimiwa amevitaja; viwanda vidogo vidogo hapa vya uzalishaji mali, sukari na mambo mengine, lakini mimi hapa nilikuwa na swali katika hiki kiwanda cha Sukari kwa sababu ni muda mwingi kiwanda hiki kipo na tunasikia lakini tafsiri hasa labda ya uzalishaji rasmi tutaanza kunufaika na sukari ya kiwanda hiki labda mnamo mwaka gani, ili tuweze kuona wananchi wetu wanafaidika kupata sukari pale, lakini pia wafanyakazi kuendelea kupata ajira nzuri ambayo itaendelea kuwapunguzia umasikini.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na hatua hii lakini bado niombe sekta ya viwanda tuendelee kuongeza ujenzi huu wa viwanda ambao utaweza kuleta ajira nyingi kwa vijana wetu na kuondokana na ule unyonge labda wa kukaa vibarazani na tunajua vijana wetu au wananchi kwa jumla wataweza kupata ajira, na wataondokana na umasikini lakini pia Serikali itaongeza pato lake.

Kwa hivyo, mimi naomba kwani bado wananchi wa Zanzibar kwa sasa wamehamasika sana; wanalima sana matunda, kwa hivyo tunahitaji viwanda vya matunda viwepo. Sasa kuna machungwa yanalimwa kwa wingi, utakuta mananasi sasa yanalimwa kwa wingi, lakini pia eneo letu la Matemwe pia linalima tungule kwa wingi. Mheshimiwa kupata viwanda vidogo vidogo ambavyo vitaweza kusindika mazao haya ni jambo la faraja na nadhani umasikini utaendelea kutupungukia.

Mhe. Naibu Spika, niende katika mradi huu wa mkakati wa kuendeleza zao la karafuu; ni kweli Mhe. Waziri, amejitahidi kujipanga kwa kuonesha yale malengo yake ambayo anakusudia kuyafanya, lakini mimi nimpongeze kwa kifungu kile cha nne cha kirumi ambapo imeeleza kwamba tayari hili eneo la ufungashaji wa biadhaa za viungo limekuwa tayari, hii ni faraja kubwa na naomba nichukue fursa hii kuipongeza sana Wizara, kwa sababu hapa itapatikana sasa elimu ya ufunganishaji wa bidhaa hii ya viungo ambapo wafanyabiashara wetu bado wanakosa ile *quality* nzuri ya ufungashaji. Kwa hivyo hii itakapokuwa tayari itatupa moyo na tunahakikisha wananchi wetu wataweza kufanya vizuri.

Niende katika ulinzi wa zao la karafuu; pia hapa nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa juhudi kubwa ambayo imeifanya kuunda kile kikosi kazi ambacho kimeweza kudhibiti ule wizi wa magendo wa karafuu, lakini bado Mheshimiwa tunasumbuliwa sasa wizi ule wa kule umefanya kupungua, lakini tuna wizi sasa wa katika mashamba yetu. Sasa zikizaliwa karafuu watu wanakwenda kukata tawi zima au kigogo kizima cha mkarafuu, halafu mtu anakwenda kuchambulia mbali.

Kwa hivyo, hiyo sasa inatusumbua wakulima, kwa hivyo Serikali pia tunaiomba hapa iweze kupanga mkakati mzuri wa kutusaidia wakulima kuona wizi huu tunanusurika nao.

Mhe. Naibu Spika, mimi niende katika masoko haya ya wajasiriamali wetu wadogo wadogo, pamoja na jitihada Serikali inayofanya lakini bado tuna kazi ya ziada ya kutafuta masoko kwa wafanyabiashara wetu hawa wadogo wadogo hali ambayo itazidi kuleta maendeleo na kuwapunguzia umasikini wananchi wetu. Bado wafanyabiashara wadogo wadogo wanasumbuka na masoko na hata yale maeneo yao wenyewe ya kufanyia biashara.

Tuangalie wanawake jinsi gani walivyojitokeza katika uuzaji wa samaki, tunawaona kila chochoro utakayopita utakuta wafanya biashara wanawake wanauza samaki, lakini bado wanawake wale hawapo sehemu rasmi ambayo ingeweza kuwaweka wao wakafanya biashara yao vizuri kwa utulivu, wanaweza wakavamiwa wakati wowote na watu wa manispaa. Kwa sababu wanafanya biashara mwahala msimokuwa rasmi.

Kwa hivyo, mimi niiombe Serikali iwangaalie wanawake, ni watu ambao sasa hivi wamechangamka sana katika kujiajiri na kujipunguzia umasikini na kuzidi kuendeleza familia zao. Kwa hivyo hili tulione, si viruzi kinamama wale wakaendelea kusumbuka na kutanga tanga huku na huku ni lazima Serikali ijipange, basi kuona wafanyabiashara wake wana sehemu maalum za kufanyia biashara na wanafanya biashara kwa utulivu na kujiongezea kipato.
Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu utakuwa si mkubwa. Nilitaka tu na mimi niungane na wenzangu katika Wizara hii kwa sababu ni Wizara muhimu kabisa ambayo ndio inayosaidia kuleta uchumi kwa wananchi wetu. Kwa hivyo nilisema na mimi niseme machache kwa niaba yangu na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, naomba kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. *Inshaallah* naomba Mwenyezi Mungu na wenzangu waiunge mkono hotuba hii ili ukijua wenzetu wakiweza kufanikiwa kuongeza viwanda, wakiweza kufanikiwa kulishughulikia zao hili la karafuu na kweli nimeacha mchango mmoja.

Mhe. Naibu Spika, zao la karafuu ni muhimu sana, hata juzi mimi nilisema hapa zao la karafuu ni muhimu sana. Karafuu ina matumizi mengi. Karafuu ni dawa kwa kila aina ya maradhi niseme, kwa hivyo, tuna umuhimu mkubwa sana wa kuhakikisha karafuu tunaishughulikia na inatuongezea soko kwa kupitia bidhaa zetu mbali mbali, baada ya kusema hayo naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja, ahsante. *(Makofi)*

**Mhe. Abdi Mosi Kombo:** Mhe. Naibu Spika, na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake na nakupongeza kwa kunigaia dakika kumi lakini sitotimiza, nitatumia dakika kidogo tu ili na mimi nitoe mchango wagu huu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitatoa mchango wangu katika ukurasa wa 16 unaosema kwamba wajasiriamali wadogo wadogo. Nchi yetu ya Zanzibar ina wajasiriamali wengi sana hasa vijana, lakini bado wajasiriamali hawa ukiwatizama ndani ya sehemu zao za kufanyia biashara bado haziridhishi kimazingira. Mhe. Panya, hapa alisema kwamba kuna kinamama wanauza samaki, lakini ukitizama samaki hao wanavyouzwa si mwahala muzuri na kweli; ni mwahala ambamo hata magari yakipita mavumbi, wengine wanang'ong'wa na manzii, wengine kama wale

wanaouza samaki wabichi wanawekwa chini tu barabarani, kwa hali ya kiafya hasa sio nzuri.

Kwa hivyo, naiomba Seirkali, wajasiriamali hawa watengewe sehemu nzuri kwa sababu tunatembea katika nchi za wenzetu tunaona jinsi biashara zinavyouzwa, na jinsi biashara zinazovyohifadhiwa. Kwa sababu wajasiriamali hawa wanalipa michango pale wanapokaa kuuza biashara, sasa kama wanalipa basi Wizara iwahifadhi vizuri, lakini samaki leo unakwenda kumuona barabarani pale anabururwa maana yake akitolewa kwenye gari anabururwa, akishabururwa anawekwa chini, baadae tunakwenda kununua halafu tunasema tujenge afya, afya yenyewe haijengeki kama ile biashara inauzwa uchafuni. Kwa hivyo naiomba Serikali kupitia Wizara ya Biashara wajasiriamali wajengewe pazuri.

Mhe. Spika, nakuja kwenye wajasiriamali hawa hawa wadogo wadogo walioko sehemu ya Juakali na kwengineko; tuna mtindo hapa, mtindo tuliokuwa nao sasa hivi wafanya biashara ndogo ndogo huwa wanalalamika sana wanaweka biashara baadae wanakuja Manispaa wanazichukua zile biashara, sasa wao wanalipa na biashara zinachukuliwa, sasa Serikali kupitia Wizara ya Biashara iwajengee sehemu au iwatafutie sehemu iliyokuwa yauhakika.

Hapo wahakikishiwe kwamba wanauza biashara zao wakishauza biashara zao hawanyang'anywi fedha wala hawapokonywi chochote, kwa sababu leo kwa mfano mfanya biashara mradi wake wa Shilingi laki moja na shilingi laki moja hiyo akiuza biashara pale anakuja Manispaa anaichukua, anakuja mwengine anaichukua hata ikifika jioni kile alichokiuza hapana kitu na yule analipa pale. Kwa hivyo naiomba Serikali kupitia Wizara ya Biashara, kwamba ihakikishe wale watu wanawekewa sehemu ambayo wapate huduma.

Mhe. Naibu Spika, kuna sehemu kule Pindamgongo Saateni pale vile vile napo wafanyiwe uhakika wakujengewa sehemu za uhakika hizi sehemu za kudumu kama wenzetu nchi nyengine kule wana *super market.* Utaikuta *super market* imejengwa vizuri tena ya roshani kila mmoja anakwenda kule ameridhika, lakini hapa sasa utamkuta mfanya biashara huyo huyo kaweka chini pale lakini analipa pamoja na kulipa kwake akija Manispaa wanachukua pesa, sasa analipa nini na kitu gani anachokipata. Kwa hivyo, tupunguze hizi sheria tulizozitunga tuzifanyie utafiti baadae tuwajengee wajasiriamali wetu ili wapate sehemu nzuri za kuuza biashara.

Mhe. Naibu Spika, nikimalizia dakika ulizonipa nakwenda sehemu ya viwanda, tunavyo viwanda vimetajwa vingi sana lakini sasa kuna kiwanda cha sukari na kipo zamani tokea Marehemu Mzee Karume, lakini mimi ningelimuomba Mhe. Waziri, hiki kiwanda cha sukari kinatoa sukari tunaipata na kama inasafirishwa

inasafirishwa nchi gani. Kwa hivyo, Mhe. Waziri akija hapa mimi namuomba atueleze kwamba ikiwa sukari inapatikana hapa tujue, kama inasafirishwa nchi za nje tujue. Ili wananchi wawe na uhakika kwamba sukari ya Zanzibar inapatikana.

Mhe. Naibu Spika, nikimalizia naiomba wizara ikuze viwanda kama alivyosema Mhe. Panya pale, alivyosema Matemwe kunatoka tungule, ni kweli. Kwa hivyo, iko haja ya kujengwa viwanda vya kusindika tungule ili Matemwe nayo inufaike. Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe kwanza niwashukuru kwa ushirikiano mlionipa tokea asubuhi hadi sasa hivi. Nina tangazo nimepewa na Katibu wa Baraza niwatangazie Kamati ya Uongozi kesho tukijaaliwa Saa 8.00 ukumbi wetu wa juu kutakuwa na kikao.

Pia, nisisitize kwamba mahudhurio asubuhi yanakuwa si mazuri, wengi wanategemea kwamba wangoje mpaka masuala yaishe ndio mtu aje. Basi kwa taarifa yenu, masuala yamekwisha tukifika hapa baada ya dua tunaingia kwenye mijadala. Kwa hivyo tunaomba kesho tufike mapema, Wizara yetu tunataka tufanye majumuisho asubuhi ili tumalize. Huku juu sina mchangiaji hata mmoja, akitokezea asubuhi mmoja, wawili tutawapa nafasi.

Kwa hivyo, naomba tuje mapema ili tuweze kumaliza hii kazi. Baada ya hayo naahirisha kikao chetu hadi kesho siku ya Ijumaa, tarehe 19/6/2015 Saa. 3.00 za asubuhi.

*(Saa 8.02 Baraza liliahirishwa hadi tarehe 19/06/2015 Saa 3.00 asubuhi)*